BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	Mhe.	Zubeir Ali Maulid	-	SPIKA
2.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
5.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
6.	Mhe.	Issa Haji Ussi Gavu	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
7.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais
10.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
11.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais
14.	Mhe.	Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais
15.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani

16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**

34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Pili – Tarehe 10 Mei, 2018

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 231

Athari za Mabadiliko ya Tabia ya Nchi

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa mwaka wa fedha unaoishia June, 2018 Serikali ilipanga kutumia jumla ya Tshs. 654.2 milioni kwa ajili ya kujenga uwezo wa kitaifa kwa ajili ya kuhimili athari za mabadiliko ya Tabia Nchi. Sambamba na hilo Tsh. 1.7 bilioni ambazo zilikadiriwa kutumika kwa ajili ya usimamizi wa mazingira, maliasili na mabadiliko ya Tabia ya Nchi katika pwani ya bahari ya Hindi yaliyotokana na tetemeko la ardhi chini ya bahari (*Tsunami*) lililotokea mwanzoni mwa mwaka 2000, lilisababisha mabadiliko makubwa sana ya ardhi hasa kwa maeneo ya kaskazini mwa bahari ya Msuka kiasi ambacho bahari imekula eneo la bahari karibu mita 200 na kuanza kusababisha hofu kubwa kwa wananchi kuhusiana na namna gani bahari inavyomega ardhi siku hadi siku.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulihifadhi eneo la Kaskazini mwa vijiji vya Msuka kutokana na uvamizi huo wa bahari ambao umekuwa na athari kubwa

(b) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo la uharibifu mkubwa wa kimazingira ambao unatokea kwa eneo hilo.

(c) Je, kuna mpango gani kwa Serikali kutumia rasilimali kidogo zilizopo kushajihisha wananchi ili kuanza kudhibiti athari hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 231 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2017/2018 Serikali ilipanga kutumia jumla Sh.804,733,000 kwa mradi wa maendeleo kwa kukuza uwezo wa Kitaifa wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu ulipangwa kufadhiliwa na Benki ya maendeleo ya Afrika (*ADB*) hata hivyo

fedha zote za Mradi huo kutoka Benki hiyo hazikupatikana katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 inategemewa fedha hizo kuingizwa katika kipindi hiki cha mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi yapo mengi Zanzibar na sio rahisi kwa Serikali kuyashughulikia yote kwa wakati mmoja. Hivyo, kwa upande wa eneo la Msuka, Serikali imejipanga kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 kuyashughulikia kwa kukusanya taarifa za kina za eneo hilo zitakazowezesha kufahamu hatua mbali mbali za kitaalamu zinazopaswa kuchukuliwa na kuondoa tatizo lililojitokeza.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali inafahamu tatizo lililopo katika eneo la Msuka la uharibifu wa mazingira unaosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, taarifa za kina zitakazokusanywa ndio zitakazotoa dira ya nini hasa kinachopaswa kufanyika kwa ajili ya kukabiliana na athari ziliopo. Hata hivyo, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Mazingira inaendelea kutoa elimu ya Mazingira kwa wananchi wa Msuka ili kuendelea kushiriki katika kulinda na kuhifadhi mazingira katika eneo hilo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mheshimiwa pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri kwanza nafurahi nilisikia alikwenda mwenyewe akaliona lile eneo na hali halisi ilivyo amejionea, lakini kwa kuwa matatizo yanapitana, shida zinapitana shida iliyopo Msuka ya uharibifu ni mkubwa kulinganisha na maeneo mengine mengi.

Je, Wizara ina mpango gani au imejipanga vipi angalau kwa hatua za awali wakati tunasubiri huo utafiti wa kina ufanyike kuweza kulihifadhi eneo hilo ili lisiendelee kuathirika kwa haraka kama ilivyokuwa inaendelea hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, katika mwaka huu wa fedha 2018/2019 tumetenga fedha karibu Dola Shilingi Laki Tatu ambazo tutazipata kutoka katika Benki ya *ADB* na endapo tutakapofanikiwa hili tayari tutakuja na mpango wa kudumu wakuhakikisha tunaweza kurithi ile hali iliyokuwepo katika eneo la Msuka.

Kweli kama anavyosema na sisi serikali tunakubaliana nae ile athari kubwa iliyokuwepo katika eneo la Msuka. Kwa macho yetu tumejionea lakini tayari Ofisi yangu imeshatoa maagizo na maelekezo kwa Idara ya Mazingira na ZEMA kushirikiana kwa kina na watendaji wa Tawala za

Mikoa, maana bahati nzuri katika sehemu kubwa ya eneo lile lililoathirika ni katika eneo ambao tuna kituo chetu cha kambi KMKM, kwa maana hiyo lazima idara zetu mbili zishirikiane ili kuweza kupata kwa hatuwa za dharura na tumhakikishie Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Konde kwamba katika kipindi hichi cha Mei mpaka Juni tunategemea kwenda kupeleka mawe kwa hatua ya kwanza ili kuweza kupunguza ile athari ambayo inatokana na mtiririko mkubwa wa maji yanayotoka juu na kuweza kula ile ardhi tunakubaliana nae katika kipindi hiki tu cha mvua tangu zimeanza tunatakriban mita 10 mpaka 15 zimeshapotea na zimeenda baharini.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza kuhusiana na swala mama alilouliza Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nilikuwa na swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri katika kujibu swali lake kwamba ule mradi wa kujenga uwezo wa kitaifa kwa ajili ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi haukuweza kutekelezeka kutokana na kutopata pesa kutoka kwa *ADB* na matarajio fedha hiyo kupatika katika kipindi hichi, lakini hili ni tatizo ambalo linaikumba nchi yetu iwapo *ADB* na mwaka huu haikuingiza pesa hizo. Serikali ina njia gani mbadala wa kuweza kukabiliana na hali hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza kama yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tulitegemea fedha hizi kutoka kwa wenzetu wa *ADB* katika mwaka wa fedha 2017/2018 lakini hatukuzipata kwa wakati huo, lakini kwa mwaka huo huo 2017/2018 ipo miradi na maandiko ambayo tayari Idara ya Mazingira na ZEMA iliandika na ilifanikiwa kutekelezwa katika kipindi hicho, tuna hii *project* ambayo bado inaendelea pale katika eneo la Kizingo ni hali hiyo hiyo katika hali ya ku-*risk* mazingira, lakini ipo ambayo imefanyika katika eneo la Kisiwa Panza yote tukiwa katika hali ya ku-*risk.* Kwa hivyo ilicheleweshwa kutoka hii lakini tulifanikiwa kupata katika maeneo mengine. Hivyo tunaamini katika mwaka huu sambamba kwamba tutakuwa tayari tunaandaa maandiko mengine lakini na hili tunategemea tutafanikiwa katika mwaka huu wa fedha wa 2018/2019.

Nam. 4

Kufikishwa kwa Utaalamu wa Viwanda
katika Kikosi cha JKU Pemba

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:

Kwa kuwa JKU ni chombo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambacho kimeundwa kwa ajili ya kuwafunza vijana wetu na pia kutoa mafunzo mbali mbali ya kujenga uchumi kupitia kilimo na viwanda. Lakini hadi sasa JKU Pemba bado hawajafikishiwa utaalamu wa viwanda ili nao waweze kujiendeleza wanapomaliza muda wao wa kukaa JKU.

(a) Je, ni kwanini hadi leo Kikosi cha JKU Zanzibar hakijaanzisha mafunzo ya viwanda huko Kisiwani Pemba.

(b) Je, ni lini JKU wataanzisha viwanda mbali mbali huko Pemba ili vijana walioko huko wafaidike na taaluma hiyo wakati wakiwepo kambini na hata pale wanapomaliza muda wao wa kuwa kambini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kutoa mafunzo kwa vijana ni miongoni mwa majukumu ya msingi wa JKU katika fani za kilimo, mifugo, kazi za ufundi pamoja na viwanda vidogo vidogo, ulinzi, ujasiri na ukakamavu.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo mafunzo ya kazi za amali hayaendeshwi Kisiwani Pemba kutokana na miongoni mwa sababu zifuatazo:-

1. Ukosefu wa majengo ya makaazi kwa ajili ya vijana watakaojiunga na mafunzo ya amali Kisiwani Pemba.
2. Ukosefu wa zana za ufundishaji vijana watakaojiunga na mafunzo hayo.
3. Mwamko mdogo kwa vijana wa Kisiwa cha Pemba kujiunga na kambi zetu za JKU.

(b) Mhe. Mwenyekiti, licha ya changamoto zilizoorodheshwa katika jibu (a), JKU inaendelea kutoa mafunzo ya amali kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba inatoa mafunzo ya ushoni. Hata hivyo JKU ina mpango wa kuanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi katika Kambi ya JKU Chokocho pale itakapopata uwezo wa kifedha kwa ajili ya kuchukua vijana katika fani ya ushoni, umeme, useremala, ufundi magari na kuendelea kutoa fani nyinginezo kidogo kidogo ambazo zinatolewa hapa Unguja.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye mwelekeo lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa amesema kwamba Pemba hawana makazi na ameshaonesha dhamira ya kufanya hivyo hapo baadae.

(a) Je, kwa wale wa Unguja ambao kuwa tayari sasa hivi wameanza kupata mafunzo haya kuna shahada yoyote au *certificate* ambayo kuwa inaonesha kwamba vijana hawa waliotoka hapa wana fani fulani ili iweze kuwasaidia katika ajira wanapotoka nje ya chuo.

(b) Kwa upande wa Pemba wamesema kwamba vijana wana mwamko mdogo lakini je, hatuoni kwamba sasa mabadiliko yako hata ukitaka nafasi ya ulinzi ni lazima uwe na cheti cha JKU au Mgambo. Je, ni hatua gani ambazo zitakuwa za kupaumbele wameziweka katika kuhakikisha makaazi yanakuwepo katika kambi hizo kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba Mhe. Mwakilishi swali (a) alirejee tena.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, narejea kwa sasa hivi amesema Pemba masuala ya mafunzo hayapo kwa ajili ya vijana wetu lakini kwa Unguja yanaendelea ushoni, useremala na umeme. Je, hapa Unguja wanatoa shahada ambazo kuonesha kwamba wanafunzi hawa au vijana hawa walioko JKU baada ya kutoka pale wanayo shahada ya kuonyesha wamepata mafunzo fulani ili iwasaidie katika ajira ambapo kuwa watakuwa nje ya JKU.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(b) Mhe. Mwenyekiti, naomba nianzie na la mwisho kwamba kutokana na umuhimu huo kama ambavyo nimetangulia kusema kwamba juhudi zinaendelea na tutahakikisha kwamba jambo hili linafanikiwa katika Kisiwa cha Pemba pamoja na zile fani nyengine ambazo vijana wetu wanahitaji kuzipata tuone kwamba azma hiyo tunaendeleza kuitekeleza siku hadi siku.

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika majibu vijana hawa ambao wamepata fani mbali mbali katika Kisiwa cha hapa Unguja katika kambi zetu umuhimu wa vijana wale na shahada zao zile ambazo wamezipata kule ni moja ya msingi na hizi zinatolewa kwa sababu maalum kwamba moja katika kutoa fani zile ni vijana wetu kuweza kujiajiri wenyewe pale ambapo watapata fursa za kufanya hivyo na lengo ni kwamba wazitumie. Lakni na zile za serikali zinazotolewa basi kwa mujibu ya matangazo na mahitaji mbali mbali ya taasisi mbali mbali vijana hawa nadhani hakuna kikwazo chochote ambacho wanaweza kukipata baada kwa kuwa serikali inahitaji vijana ambao wenye ujuzi zaidi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria zetu za nchi yetu tumeweka kwamba vijana washiriki katika Jeshi la Kujenga Uchumi ili waweze kujua kwanza uchungu wa nchi yao ili wanapoajiriwa katika sekta yoyote wawe makini kuheshimu taratibu zilizowekwa katika kazi zao. Swali langu lipo hapa.

(a) Kwa kuwa jibu lake Mhe. Waziri amesema tu kwamba vijana kutoka Pemba au vijana wa Pemba hawana uchangamfu au hawapendi kushiriki katika kujiunga na JKU. Ni wito gani wanaoutoa kama serikali na hilo la nchi nzima si Unguja wala si Pemba, ili vijana hao waweze kushiriki kwa mujibu wa sheria katika kujenga taifa katika JKU.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba mwamko huo kama nilivyotangulia kusema ni mdogo lakini pia juhudi za serikali ni kwamba kwa sasa hivi nadhani ni mashuhuda karibuni hivi kwamba sasa hivi serikali imerudisha tena mpango ule wa kuhakikisha kwamba vijana wale ambao wanataka kujiunga katika vikosi mbali mbali au taasisi za kiulinzi basi ni lazima wapitie JKU ama JKT. Kwa upande wa Zanzibar ni kwamba ni JKU, hivyo basi hiyo ni hatuwa ya mwanzo na ni juhudi za kwanza au ni wito wa mwanzo.

Hivyo vile vile niombe tu kwa kupitia kwa kuwa chombo hichi ni chombo cha wananchi na Wawakilishi wa wananchi wamo humu ndani. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe watusaidie katika kuwaelimisha vijana wetu ili sio lengo la kupata hizo fursa pekee lakini vile vile azma ya serikali ambayo imekusudiwa katika kupata vijana wazalendo, wakakamavu waipende nchi yao basi tuanzie huko majimboni kwetu tuwahamasishe. Sisi kama serikali tuko tayari kuhakikisha kwamba vijana hao tunawapokea kwa lengo lile lile serikali ambalo imejipangia.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na swali dogo sana la nyongeza lakini niombe radhi kwamba Mhe. Mwenyekiti macho yako yalikuwa upande mmoja, lakini nilikuwa na haki ya kuuliza swali la nyongeza, Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri juu ya swali hili mama mimi nililikuwa na maswali ya nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Swala la muamko mdogo kwa vijana Kisiwani Pemba limeelezewa lakini niulize tu kwamba je, Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya utafiti kwa sababu huwezi ukaondosha

tatizo bila ya kujua *source* ya tatizo, limefanya utafiti wa kuweza kubaini sababu zinazopelekea vijana wa Pemba kuwa muamko mdogo wa kujiunga na UKU.

(b) Swala la majengo na Vyuo vya Ufundi kwa Jeshi la JKU. Je, JKU kutokana na uwezo wake mdogo imefikiria kuweza kuwaandikia wahisani mbali mbali wa maendeleo juu ya suala hili la kujenga majengo au vyuo vya ufundi katika jeshi lake katika kisiwa cha Pemba au hata Zanzibar kwa sababu huwezi kufanya mambo hayo peke yako wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwaombe sana minong'ono imekuwa mingi kwa hiyo tunampa shida Waziri wakati anasikiliza swali kutoka kwa Mjumbe. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe minong'ono imekuwa mikubwa tupunguze. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri naomba niendelee kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni suala lake (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu tafiti kwa nini vijana kisiwani Pemba kuwa na muamko mdogo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kiufupi ni kwamba hatujafanya utafiti wa kina ambao unapelekea katika hali kama hiyo. Lakini kwa kuwa suala la utafiti ni moja katika mipango tunaingiza katika mipango yetu ya serikali, nadhani hili tutaweza kuchukua kama ni ushauri ili hatimae tuweze kufanya utafiti tuone hasa ni kwa namna gani vijana wetu hawa hawapendi kujiunga na JKU katika kisiwa kile cha Pemba.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu juhu di za kutafuta namna wafadhili katika suala zima la miundombinu ya majengo haya ya viwanda na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa serikali imeshachukua hatua kwa sasa na kama tulivyosikia hapa karibuni ni kwamba kuna mpango mkuu wa serikali ambao umeanza kazi ya hatua ya ujenzi wa majengo mbali mbali katika vikosi vyetu vya Idara Maalum kwa sasa hivi tumeendelea na vikosi vyengine lakini tutakapofika JKU basi nadhani hayo haya mambo tutaweza kuyaangalia.

Kwa hivyo nadhani Mhe. Mwakilishi ni kwamba tukumbuke juhudi za serikali zinaendelea na kwa sasa hivi hakujaonekana kwamba kwa hatua ya sasa kwamba tuende kutafuta wafadhili kwa hatua ambayo tuliyofikia kwa sasa hivi.

Nam. 33

Ujenzi wa Soko huko Chumbuni

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa– Aliuliza**:**

Wananchi wa Jimbo la Chumbuni na majimbo jirani hasa wanawake wamekuwa wakipata shida sana kutokana na kutokuwa na soko katika eneo lao.

(a) Kwa kuwa jimbo la Chumbuni lina wananchi zaidi ya 30,000 na kwa kuwa jimbo hilo bado lina maeneo ya wazi, ni lini Serikali kupitia Manispaa ya Mjini itawajengea soko wananchi hao.

(b) Ni vigezo gani vinavyotumiwa kufikia uamuzi wa kujenga soko katika maeneo ya kijamii.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 33 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa kwa sasa lina masoko makubwa matatu (3) na mengine madogo matatu (3) yanayotoa huduma kwa wananchi. Kwa kawaida ujenzi wa miundombinu ya kutoa huduma kwa wananchi katika Manispaa ikiwemo hii ya soko unafanyika kwa kuzingatia Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi (*Land Use Master Plan)*. Hivyo basi pamoja na kuweko kwa eneo la wazi katika eneo la Chumbuni na sio lazima sana kujengwa soko, lakini itategemea pia mipango iliyopo sasa na ile ya baadae. Hata hivyo, pale itakapoonekana kwamba ipo haja ya lazima ya ujenzi wa aina yoyote basi jambo kama hilo linaweza kuzingatiwa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu langu la kifungu (a), kigezo kikubwa katika ujenzi kama huo wa soko ni maelekezo ya mpango mkuu wa matumizi ya ardhi na hasa ujenzi wa soko ambao unahitaji eneo kubwa la ardhi. Hii ni kwa sababu ujenzi wa soko una mahitaji ya huduma mbali mbali zinazoendana na shughuli za soko. Miongoni mwa vigezo hivyo ni pamoja na barabara kuu zinazoingia na kutoka katika maeneo ya soko, nafasi kubwa za maegesho ya gari, sehemu za kukusanyia taka pamoja na miundombinu ya maji ya mvua na maji machafu.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nimesikia majibu ya Mhe. Naibu Waziri ya kuvunja moyo kwa wanawake hasa hususan waliokuwa wajasiriamali wanajitegemea wanaotafuta maendeleo na maisha yao kuendesha kutokana na kuwa kazi ni ndogo katika nchi yetu. Lakini wanawake wanajitafutia kazi ya kufanya maendeleo.(*Makofi*).

Nilitaka kumuuliza tu Mhe. Naibu Waziri ni kweli kwanza nakubaliana na hoja yake ni kweli masoko Manispaa ya Mjini ni matatu, lakini aangalie na hatua yaliko na Chumbuni iliko. Lakini nataka kumuuliza.

Je, yuko tayari Mhe. Waziri kukaa na wananchi na viongozi wa Jimbo la Chumbuni ili kuliangalia hili suala la kulisawazisha ili yaweze kupatikana uhakika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa dada yangu Mwakilishi wa viti Maalum wa wanawake Mkoa wa Mjini kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nitamke kwamba serikali haiko tayari kuwavunja moyo au haina mpango wa kuwavunja moyo wanawake katika mipango mbali mbali ya serikali na ushahidi ni huo. Bali bado iko katika kuangalia kutafuta namna kuona wanawake wa Zanzibar wanaendelea kuzitumia kupata fursa mbali mbali zinazotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jibu kwamba tuko tayari au niko tayari. Mheshimiwa serikali kwa kuwa serikali ya wananchi, hivyo basi hakuna kikwazo chochote cha kukaa na wananchi wa Jimbo la Chumbuni katika kuangalia uwezekano wa kuimarisha au kuanzisha jambo lolote la kimaendeleao ambalo linatakiwa litolewe kwa na serikali kwa upande wa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kutokana na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi nilikuwa naomba kumuuliza swali dogo tu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Kusini walileta maombi na kutaka kujengewa soko iwe kama kiunganishi kama ilivyo Mkoa wa Kaskazini na mpaka sasa hatujaona hatua wala majibu ya serikali. Sasa nilikuwa namuomba Mhe. Waziri wamefikia hatua gani ya kuweza kuwafikiria wananchi wa Mkoa wa Kusini na wao kufanyiwa kiunganishi kama ilivyokuwa mikoa mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma kwa namna ambavyo anapambana katika kuona kwamba ni namna gani wananchi wa Mkoa wa Kusini hususan vijana wanapata huduma za soko katika Mkoa ule kama ni kiunganishi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli jambo hili lilijitokeza ambalo pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mwakilishi pia wa Jimbo la Tunguu na yeye alipigana sana katika kuona kwamba wananchi wanapata soko katika eneo lile.

Lakini jibu ni kwamba serikali kwa upande wake kupitia Afisi ya Rais Tawala za Mikoa hatuna tatizo na hilo. Lakini ikumbukwe kwamba hata Mhe. Waziri alipokuja na majibu alitoa ushauri na maelekezo kwa kuwa jambo lile ni la kiutaratibu zifuatwe zile taratibu za kisheria na kwa kuwa tulipata taarifa kwamba eneo lile si eneo la wananchi na ni eneo la wanajeshi au la Jeshi. Kwa hivyo pale endapo Waheshimiwa watakamilisha zile *process* au hatua moja baada ya nyengine baada ya kukamilika. Mhe. Waziri akaagiza wakae serikali ya Mkoa pamoja na Halmashauri husika kuona ni namna gani linaweza lile jambo likaweza kufanyika.

Kwa maana hiyo hatuna tatizo kwa hilo na tumeona ni jambo muhimu na tuko tayari pale ambapo patafikiwa katika zile hatua, basi na sisi kuingiza juhudi zetu kufanikisha azma hiyo Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kusini.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba niulize maswali mawili (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika suala la msingi wananchi wa Chumbuni walidai kujengewa soko. Majibu ya Mhe. Waziri tumeyasikia lakini historia inasema kwamba lengo kubwa la kujenga soko Chumbuni mwanzo ilikuwa kuwaondoa wananchi wanauza bidhaa pale Maruhubi barabarani na kuwapeleka kwenye soko. Je, serikali imeangalia hilo.

(b) Kwa mujibu wa vigezo ambavyo vimetajwa katika majibu yake Mhe. Waziri Wilaya ya Magharibi A ina vigezo vyote vya kujenga soko la kileo na la kisasa kwa sababu tuna eneo kubwa Chuini tunaweza kujenga kituo cha magari lakini na soko na mambo mengine yote.

Je, serikali inatoa kauli gani kuhusu kujenga soko katika eneo la Chuini Wilaya ya Magharibi "A".

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika eneo la Chuini kwa Nyanya eneo lile tayari limeonekana kwamba lina sifa kama vile Mheshimiwa ambavyo ameainisha. Lakini vile vile nitakuwa shuhuda mkubwa kwamba Mhe. Mwakilishi amekuwa akipambana sana katika kuona ni namna gani azma hiyo inaweza kufikiwa katika ujenzi wa soko, lengo ni kuondosha kero kwa wananchi wa maeneo yale na maeneo mengine kwa ujumla.

Lakini nataka kusema kwamba Mhe. Mwenyekiti, juhudi za serikali kupitia Afisi ya Rais Tawala za Mikoa zimeshachukuliwa na hatua ya sasa ni kwamba tunashirikisha wahusika wengine kama ni watalaamu katika suala zima la kufuata zile taratibu nyengine za kisheria ili kusudi itakapokamilika shughuli hii ziweze kufanyika. Kwa hatua ya sasa hata karibuni tumeshaagiza kupitia Manispaa ya Magharibi A kwamba kutenga kwa kuangalia makusanyo kuweza kuona kwamba tunaelekeza nguvu zetu katika kipindi hichi tunachoelekea katika kukamilisha au kutimizi ile ndoto ambayo imekusudiwa.

Lakini kwa kuwa vile vile tukumbuke kwamba mambo haya au utaratibu ujenzi ule utatokana na matakwa ya mpango wetu kama nilivyotangulia kusema mpango wa Matumizi ya *Master Plan*. Inaonesha kwamba tunachokusudia ni kuhakikisha kwamba mji ule utakapofanikiwa magari yanayotoka Kaskazini yafikie pale ili kusudi tupunguze msongamano katika Mji huu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niombe niseme kwamba kazi hiyo inaendelea na ni imani yangu kwamba jambo hili litafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Haya Mhe. Waziri kwa majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nitoe majibu ya nyongeza na kabla sijafanya hivyo, naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba serikali inatambua wazo lake la kuwaondosha watu wanaofanya biashara barabarani Maruhubi na kuwatafutia eneo muafaka ili waweze kujiendesha katika maisha yako na ndio maana Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba serikali imelizingatia hilo jambo na inashauriana na wataalamu mbali mbali katika kuona eneo gani linaweza kufaa katika kufanya jambo hilo.

Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wavute subira ili serikali iweze kufanya jambo hilo kupitia mipango yake mbali mbali ambayo itakuwpo chini ya Manispaa zetu za Mjini, Magharibi "A" na Magharibi "B".

Lakini kuhusu suala la wananchi wa Magharibi A kupata eneo la soko nadhani serikali tayari kupitia Idara ya Mipango Miji na kupitia Wizara ya Ardhi imeshakamilisha ramani na michoro ya awali na imeshakabidhi kwa afisi zetu ili tuweze kufuata hatua nyengine ambazo ramani hizo zitakuwa zinaonesha wapi patakuwa kituo na wapi patakuwa soko, wapi patakuwa *shopping mall*. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi aanze tu kuwahamasisha wananchi wake wajimbo wa Mfenesini na kwengineko wale wanaotaka kuekeza katika maeneo hayo basi ni vizuri wajiandae lakini mpango huo upo tayari. (*Makofi*).

Nam. 5

Haki ya Mshtakiwa Aliyeachiwa na Mahakama baada ya Kutopatikana na Hatia

Mhe. Shehe Hamad Mattar– Aliuliza**:**

Kwa kuwa wananchi wanaposhtakiwa ama huenda Mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa kesi hadi kumalizika au kuwekwa ndani (rumande) kwa usalama wao au kwa upelelezi wa kesi nyengine.

Na kwa kuwa baadhi ya wakati mshtakiwa huwekwa rumande kwa mwaka na baada ya kusomewa hukumu baadhi ya wakati mshtakiwa hufungwa au kuachiwa huru ama kufutiwa kesi kwa mujibu wa sheria.

(a) Je, ni hatua gani za kisheria zinazostahiki kuchukuliwa na mwananchi ambaye amefutiwa kesi au kuachiwa huru baada ya kukaa rumande kwa muda wote huo.
(b) Je, ni lini serikali itaanza kutoa fidia au stahiki nyengine kwa mshtakiwa aliyekuwa rumande na kuachiwa baada ya kuonekana kuwa hana makosa na tayari ameshasumbuka na kudhalilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya watuhumiwa wa kosa huenda Mahakamani kusikiliza kesi zao na wengine huwekwa rumande. Lakini kuwekwa rumande mtuhumiwa ni kwa mujibu wa Sheria na si kwa utashi wa mtu. Na kwa mujibu wa kifungu cha 12(6)(b) cha Katiba ya Zanzibar 1984 kimeeleza kwamba naomba kunukuu:

> "Mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai hatatendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitishwa kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo".

Mhe. Mwenyekiti, hivyo kwa mujibu wa Katiba mtu anaweza kutuhumiwa na kosa na akawekwa kizuizini na pamoja na kuwekwa rumande, lakini kutokana na ama ushahidi kuwa dhaifu au upungufu mwengine wa Sheria na Mahakama ikashindwa kuthibitisha kosa na Mahakama inaweza kumuachia huru mtu huyo. Kitendo cha kumuachia huru mtu huyo si kwamba hajatenda kosa lakini inawezekana ushahidi haujakidhi vigezo au matakwa ya Sheria. Hivyo mtu aliyeachiwa huru hawezi kuchukua hatua zozote za kisheria isipokuwa kwamba kuwekwa kwake kizuizini au rumande kunaambatana na makosa ya uongo au kusingiziwa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Kwa kawaida Serikali haitoi fidia au stahiki nyengine kwa mshtakiwa aliyewekwa rumande na kuachiwa huru baada ya kuonekana kuwa hana makosa isipokuwa kwamba mtu mwenyewe anaweza kufungua kesi ya madai ya kudai fidia iwapo itatokea kuwekwa kwake rumande au kizuizini kunatokana na makosa ya udanganyifu au kusingiziwa kesi au kubambikiziwa kosa hilo.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba nimuulize maswala mawili (a) na (b) la nyongeza.

Kwa kuwa majibu yake yanasema kwamba mtuhumiwa hawezi kudai aliyeachiwa huru.

(a) Naomba anambie ni sheria gani ambayo inamzuia huyo mtuhumiwa aliyeachiwa huru asiweze kuchukuwa hatua nyengine yoyote wakati tayari ameshadhalilika.

(b) Kwa kuwa sababu moja wapo inayofanya kesi kukaa muda mrefu na watuhumiwa kukaa rumande hasa kwa upande wa Pemba ni kukosekana kwa Jaji Mkuu. Kukosekana kwa Jaji Mkuu inasemekana ni kwamba safari zinakuwa ni nyingi na mara nyingi kulidaiwa kuwa na Jaji Mkaazi Pemba. Je, ni lini hatua hii ya kupata Jaji Mkaazi kuweko Pemba ili kupunguza watu kukaa rumande kwa muda mrefu walioko katika Chuo chetu cha Mafunzo. Ni lini nyumba ya Jaji Mkaazi ambayo inazungumzwa kwa muda mrefu itakuwepo ili Jaji Mkaazi awepo kupunguza kesi ambazo kuwa hazistahiki kuwepo kwa muda mefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, suala la sheria gani ni vyema tukaelewa kwamba masuala yote ambayo yanayohusiana na makosa ya jinai sheria ambayo inayosimamia makosa haya ni ile sheria ambayo muda mfupi au kipindi kilichopita ililetwa Barazani kuifanyia marekebisho na alhamdulillah sheria hiyo tayari imeshasainiwa na sio sheria nyengine yoyote isipokuwa ile Sheria inayohusiana na Mwenendo wa Jinai ya Namba 7 ya mwaka 2018.

Sasa sheria hii ndiyo ambayo ilielezea masuala yote ya jinai. Kwa hivyo kama huyu hana nafasi ya kushitaki ya kutoa fidia basi ni sheria hii hii ambayo haikutambua suala hilo.

(b) Lakini Jaji Mkaazi atapelekwa Pemba. Mhe. Mwenyekiti, nimuhakikishie kwamba Mhe. Shehe Hamad Mattar utaratibu wa kupeleka Jaji Mkaazi Pemba unaendelea na uko katika hatua za mwisho. Kwa hivyo aendelee kusubiri wakati wowote masuala haya yatakaa sawa.

Nam. 57

Kukosekana Kwa Asilimia 30 Kwenda Kwa Wavuvi Zinazopatikana Kutokana Na Maeneo Tegefu Ya Bahari

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi wanazozichukua za kuanzisha maeneo tegefu ya Uvuvi ambayo yameonesha mafanikio makubwa kwa uvuvi wetu.

(a) Kwa nini 30% ya michango inayopatikana kutokana na maeneo hayo haiwafikii Wavuvi kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 19(3)(b) ya Kanuni ya Uhifadhi wa Bahari.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha maeneo mengine kama hayo katika vijiji vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifungo na Uvuvi – Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwanza kabla ya kujibu swali linalohusika naomba niseme yafuatayo:-

Kwanza tunapokea sana pongezi kwa serikali na tunamshukuru sana Mhe. Mwanaidi kwa kuona kwamba kweli serikali inajitahidi kufanya mambo mengi na kwa hivyo tunamuomba azidi kuwaambia wale ambao hawataki kujua kwamba serikali inafanya mengi, awaambie ili sote tujue kwamba serikali inafanya mengi ambayo yanaonekana. (*Makofi*)

Nikiingia kwenye jibu sasa kwa ruhusa yako naomba kwa kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa swali Nam.57 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwepo kwa kifungu Na.19(3)(b) cha kanuni ya maeneo ya hifadhi (*MCU*) kirefu chake ni *marine conservation unit* kinachotoa asilimia 30 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya wanajamii. Utaratibu wake ni kwamba asilimia 30 inatakiwa ithibitishwe na kukubaliwa na Kamati Tendaji ya eneo husika (*MIMCA* ina vijiji 31), (Menai vijiji 27) na (Pecca vijiji 31).

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulithibitisha Baraza lako kwamba asilimia 30 inawafikia wananchi kwa utaratibu uliowekwa na kanuni ya *MCU* kutokana na sababu ya kuwa kazi ya Wizara yangu kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ni kuratibu tu mahitaji ya asilimia 30 kwa mwaka baada ya makubaliano yanayofikiwa baina ya wenyeviti wenyewe wa kamati nilizozitaja hapo juu na kuhakikisha kuwa hakuna migogoro ya mgawanyo wa asilimia hiyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ina mpango wa kuanzisha maeneo mawili mapya ya hifadhi za baharini ambayo ni kama yafuatavyo:-
   (i) TUMCA – *Tumbatu Marine Conservation Area* litakalokuwepo Kisiwa cha Tumbatu Unguja.

   (ii) CHABAMCA – *Changuu, Bawe Marine Conservation Area* litalokuwepo katika bahari ya Wilaya ya Mjini Unguja.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii kuweza kumuliza Mhe. Naibu Waziri maswali madogo kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze kwa kunijibu masuala yangu vizuri na kwa ufasaha Mhe. Naibu Waziri hongera sana naomba nikuulize kama ifuatavyo:-

(a) Ni wananchi wa maeneo gani waliofikiwa na mgao huo kwa asilimia 30.

(b) Kwa nini wananchi wa Pemba hawafaidiki na mpango huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifungo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwakilishi kwa kuuliza maswali yako ya nyongeza.

Kwanza napenda kukwambia kwamba hapo mwanzo nilisema katika vijiji vya MIMCA 31 ni maeneo hayo ndio ambayo yanapata ruzuku hii, halafu Menai ni vijiji 27 vinapata ruzuku hii pia PECCA inapata ruzuku hii.

Sasa kwa upande wa Pemba ni kweli kwamba hawajapata ni kwa sababu Pemba imeanzishwa hivi karibuni, wanaita *Conservation Area* ya Pemba imeanza hivi karibuni na karibuni tutaanza kupata mapato kutokana na hiyo. Lakini kwa upande wa hizi mbili ambazo hazijaanza tunategemea zitakapokamilika utaratibu nazo zitakuwa zinaingiza mapato kama kawaida.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu ya serikali yasiyokuwa na kichwa wala miguu naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa asilimia 30 inawanufaisha watu wengi kama tukiangalia *conservation area* za Bara vijiji vilivokuwepo Tanga, vilivokuweko Bagamoyo vinawafaidisha kwa kujenga maabara na vitu vyengine vingi ambavyo wananchi wenyewe wanaviona.

(a) Serikali itakuwa tayari sasa kututajia vijiji vilivyofaidika na vitu hivyo.

(b) Kwa sababu Chukwani na Buyu iko katika *conservation area* na sasa kumetokea wahalifu wengi wa wavuvi wale wanaokuja kuvua na madau kwa zile nyavu zisizotakiwa za kukokota. Je, serikali ina mpango gani kwenda kuwaona watu wa Buyu na Chukwani kuweza kusikiliza kilio chao ili isije ikatokea maafa makubwa yanayotokea katika sehemu nyengine za Zanzibar hii.

Mhe. Naibu Waziri Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kumjibu Mhe. Mohamed ambaye aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Uvuvi, naamini anajua mengi kwa sababu wao ndio walioanzisha hizi maeneo tengefu, naamini hivyo. Sasa kwa kujibu suala lake ni kwamba tuko tayari kwenda kuona yale ambayo yamefikiwa kutokana na mapato hayo ambayo aliyoyasema, tupo tayari kwenda kabisa na tunaamini tunajua kwamba Tanga kule kuna vijiji vya Pangani, Bagamoyo hao wamefaidika, kuna maabara zimejengwa kwa mapato kama haya. Sasa na sisi tutafuatilia kuona kwamba hizi fedha zinazopatikana basi zinanufaika kama wenzetu Tanga kule wanavyofaidika.

UTARATIBU

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe Mwenyekiti utaratibu, Mhe. Mwenyekiti suali langu namba (b) halikujibiwa watu wa Chukwani na Buyu wako tayari kuwaona Masheha na watu wale kusije kukatokea maafa makubwa kama yaliyotokea katika vijiji vyetu vya Ukongoroni na kwengine.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed alisema yuko tayari alijibu. Alijibu Mheshimiwa kama yuko tayari kwenda kuwaona.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya ufasaha lakini pia nimpongeze tena kwa kuliona eneo la Tumbatu kuwa nalo litakuwa ni miongoni mwa hayo maeneo tengefu ambayo yatatengwa ambayo kayataja hapa maeneo mawili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nipende kumuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa maeneo haya tayari umeshayataja na tayari umeshakuwa katika mpango wa kuyatenga. Je, serikali imechukua hatua gani ya kwenda kuonana na wananchi husika wa hili eneo la Tumbatu kuzungumza nao na kukubaliana nao katika kulitenga hili eneo ili kuepusha kuja kutokea migogoro ya kiuvuvi ambayo huko nyuma tayari kumeshakuwa na historia ya migogoro baina ya vijiji viwili vile tofauti.

Mhe. Naibu Waziri Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kujibu swali la Mhe. Hidaya ni kwamba mpango wa kupita maeneo yote ya kuzungumza na wavuvi ili kutatua matatizo ambayo yanayoweza kujitokeza tumeshaufanya na hivi sasa tunakamilisha *document* tu, zikishakukamilika zile *documents* zinazotakiwa basi tutaanza kufanya kazi kwenye maeneo hayo ambayo tumeyataja hapo juu.

Ni kweli kwamba kumekutokea migogoro na nakumbuka Mkoa wa Kaskazini Tumbatu na Kivunge iliwahi kutokea migogoro watu wakapigana kule na mmoja katika watu waliojaribu kusuluhisha mgogoro huo nilikuwemo mimi tukiongozwa na Mhe. Haji Omar Kheri Waziri wa Tawala za Mikoa wakati ule. Kwa hivyo haya mambo ya migogoro kwa kweli tunayaangalia sana hatutaki migogoro itokee, hatutaki wananchi wetu wagombane kwa sababu ya raslimali yao wenyewe, tunaka waitumie ili iwanufaishe. Kwa hivyo vikao na hata *training,* masomo tunawafanyia ili waweze kujua madhumuni hasa ya kuziweka hizo *conservation area*.

Nam. 113

Kipaumbele Kwa Mazao Mengine Ya Biashara

Mhe. Hidaya Ali Makame – Aliuliza:

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali ningependa kuweka marekebisho madogo ambayo yamejitokeza sana katika swali langu hili, ni kwamba nilikusudia pilipili manga ila hapa mote imeandikwa pili pili hoho, kilichokusudiwa ni pilipili manga Mhe. Mwenyekiti ahsante.

Zanzibar imebarikiwa sana kuwa na mazao ya biashara ambayo yana tija kubwa sana kama vile Karafuu, pilipili hoho, nazi n.k hata hivyo, mkazo zaidi umewekwa katika zao la Karafuu peke yake na mazao mengine kama Pili pili hoho ambazo kilo moja katika soko ni shiilingi 29,000/= mpaka 30,000/= lakini zao hili halipewi kipaumbele kama ilivyo Karafuu.na wakulima wa zao hili hawatazamwi kwenye masoko na badala yake huwa wanapunjwa sana.

(a) Je, Wizara itachukuwa hatua gani kulipa hadhi zao la pili pili hoho ambalo lina bei kubwa ili kuwezesha wakulima wake wajikombowe na umasikini.

(b) Je, Wizara imefanya tathmini gani kwa mazao mengine ya biashara mbali na Karafuu katika kuhakikisha yanaleta tija kwa Wakulima na nchi kwa ujumla.

(c) Je, mazao gani mengine ya biashara ambayo Wizara imeyawekea mkakati kama ule unaowekwa kwa zao la Karafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake Nam. 113 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri samahani kidogo, Waheshimiwa Wajumbe hii ni mara ya pili nasema mazungumzo minong'ono imekuwa mikubwa na natumai kila mtu ana Kanuni. Hebu tuangalie hii Kanuni ya 61, tuangalie sote kwa pamoja kifungu (e) hatozungumza kwa sauti ya juu. Kwa hivyo sauti zimepanda na sisi tunaendesha kazi zetu kwa mujibu wa Kanuni, sitaki yatokee mengine Waheshimiwa. Kwa hivyo tuwe watulivu tusikilizane ili tumpe nafasi Mhe. Naibu Waziri atoe majibu na yule aliyeuliza aweze kusikia lile jawabu lake.

Kwa hivyo mara nyingi hizi sauti zikipanda Mheshimiwa anakuwa hasikii lakini mara nyengine Waheshimiwa nyinyi Wajumbe mtasema hamkujibiwa, kumbe Mhe. Waziri amejibu lakini kutokana na hili zogo, sauti kubwa. Hivyo hatuwezi kusikia. Nawaomba sana mara ya pili nazungumza nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tusikilize na tuwe watulivu tusizungumze kwa sauti za juu, nawaomba Waheshimiwa ahsante. Mhe. Naibu Waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake Nam. 113 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara kwa kupitia shirika la Biashara la Taifa la *ZSTC* limeanza kununua na kuuza bidhaa nyengine za viungo vinavyozalishwa Zanzibar kama pilipili hoho, mdalasini na pilipili manga na mwaka huu wa bajeti wa 2017/2018 Shirika limenunua bidhaa za pilipili hoho, pilipili manga na mdalasini zenye thamani ya TZS. 14,850,000 (kilo 200 za pilipili hoho kwa thamani ya TZS. 5,920,000; pili pili manga kilo 365.5 zenye thamani ya TZS 7,270,000 na mdalasini kilo 81 zenye thamani ya TZS. 1,620,000.

(b) Shirika linafanya uhamasishaji na usajili kwa wakulima wa viungo vilivyotajwa hapo juu ili kuongeza uzalishaji kwa lengo la kupata mazao ya viungo yanayokidhi haja ya Shirika pamoja na soko kwa ujumla.

(c) Mazao ya biashara ambayo Wizara imejiwekea mkakati kama uliowekwa kwenye karafuu ni mazao yote ya viungo kama vile mdalasini, pilipili manga, pilipili hoho, hiliki, tangawizi, vanilla na mazao mengine.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nianze tena kwa kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yakiumakini zaidi lakini ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

a) Mheshimiwa umetaja hapa kwamba wakulima watasajiliwa lakini hao wakulima ambao watasajiliwa ni wakulima wa maeneo ambao tayari labda wameshaanza kusajiliwa na hao

wakulima wenyewe ambao wameshasajiliwa watasajiliwa kinamna gani ili waweze kujiimairisha zaidi na huu ukulima wa viungo hivi.

b) Kwa vile wewe ni mdau mkubwa wa wakulima na wakwenzi, wewe ni Mwakilishi wa wakulima na wakwezi, na hapa tukiangalia hii changamoto hususan inawagusa hao wakulima ambao wewe kila siku unawapigia kelele hapa. Je, utachukua juhudi gani kuhakikisha soko la pilipili manga, pilipili hoho na mdalasini linaimarika zaidi ndani ya nchi yetu ili kuweza kuwawezesha zaidi wakulima wale waachane na yale malalamiko ambayo kila siku wanailalamikia nchi yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Hidaya swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

a) Mhe. kwanza napenda kumpongeza Mhe. Hidaya kwa swali lake zuri na kwamba kutilia mkazo hasa mazao haya ya biashara ya kilimo, lakini nataka kumwambia kwamba Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tayaru inafanya usajili wa wakulima katika maeneo mbali mbali ya mashamba ambayo Wizara ya Kilimo kazi yake kusajili wakulima lakini Wizara ya Biashara kushajihisha mazao haya ya biashara ili wakulima waweze kuyalima kwa sababu yana masoko ya kuuza.

b) Pilipili manga, pilipili hoho na mazao hayo yote ya biashara hata ukaona Wizara yetu ya Biashara imo hata kwenye *budget speech* yetu tumeyazungumza kwa sababu ni mazao ya biashara na yana tija na yana thamani kubwa, lazima yalimwe na masoko yapo ya kuyauza na tayari Wizara ya Biashara kupitia *ZSTC,* ukienda kule tumeanzisha kilimo hai (*organic*), tunaya-*pack* na tunayauza na yana thamani na wananchi wanayapenda hata watalii wamekuwa ni wanunuzi wakubwa wa bidhaa hizi.

UTARATIBU

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri ni maeneo gani ambayo hawa wakulima tayari wameshaanza kufikiwa na kuanza kusajiliwa.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda kwa majawabu mazuri aliyoyaeleza kwa ukakamavu na kwa ufahamu wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, katika jawabu alilosema Mhe. Naibu Waziri alizungumzia kwamba sasa hivi kuna mazao ambayo wakulima wake wamesajiliwa. Pia alizungumzia kilimo cha hai yaani *organic*. Kwa hivyo, kuhusu suala la Mhe. Hidaya Ali Makame kwamba wakulima ambao wamesajiliwa ni hawa ambao wanalima kilimo cha hai, nao wako Gando, Mtambwe kama maeneo mawili hapa Zanzibar pia Kizimbani kuna wakulima wanalima kilimo hai ambacho mazao yao yamesajiliwa na yanauzwa nchi za nje na yana thamani kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa ujuma *ZSTC* haijaanza kununua pilipili hoho na vitu vyengine vya kawaida, kwa sababu huko nyuma *ZSTC* ilifanya kazi hiyo lakini iliwacha kununua kutokana na soko na pia kutokana na kwamba wakulima walikuwa hawana mazao ya kutosha. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba wizara yetu na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tumejiandaa. Katika mkakati wetu wa mwaka huu kuona kwamba wakulima wanashajihishwa walime mazao haya kwa sababu katika bajeti yetu kuna viwanda ambavyo tumekubaliwa kuvianzisha kwa ajili ya kuchakata mazao haya na kuuza nje.

Mhe. Mwenyekiti, shida iliopo ni kwamba wakulima wetu hawajaweza kulima kwa kujitosheleza kuwa na viwanda. Ombi letu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa kupitia Mhe. Hidaya Ali Makame, hasa Kaskazini. Zamani Kaskazini walikuwa wakilima manjano, pilipili manga na tangawizi, lakini vitu hivyo vyote havipo vya kutosha. Mwaka jana tulimwambia Mhe. Hidaya Ali Makame. Kwa hivyo, asubiri na awashajihishe na mwaka huu *Inshallah* tutashirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ili kuona kwamba haya mambo yanapatikana. Suala la soko halipo, kwa sababu soko lipo na Mhe. Naibu Waziri amelieleza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda Mhe. Hassan Khamis Hafidh DIASPORA swali (a) na (b). Kwa kuwa wakulima wetu ni wanyonge sana, hasa katika kuvuna kwao hawajui mazao yao pakwenda kuyauza na tumeona nchi nyingi za nje zikiuza shoki shoki kutoka Thailand mihogo na mambo mengineyo.

(a) Je, serikali kupitia wizara yako mumeshawahi kupeleka shoki shoki, mihogo na mazao mengine kupitia wizara yao nchi za nje kuuzwa kutoka Zanzibar.

(b) Kwa kuwa Zanzibar wakulima wote ni wanyonge. Je, katika Jimbo langu la Chaani umeshawahi wizara yako kuja kuwasaidia wakulima, hasa kwa upande wa ndimu na mambo mengineyo, katika kuweza kufanya viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika swali langu kwamba utafiti uko wazi kwamba mazao yote tuliyoyafanyia utafiti kuwa yana soko, soko lipo. Lakini kuna mambo ambayo yalikuwa yana kasoro, kwa mfano *packaging* ku-*pack* yale mazao, *branding* na mambo mengine. Lakini sasa kutokana na sera ya viwanda ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tutakuwa tuna kitu tumeanzisha *smeader*. Mambo yote haya tutakuwa tunaya-*brand*, tunaya-*pack* vizuri na tutayauza nje. Soko lipo, mambo yote uliyoyataja Mhe. Mjumbe jimboni kwako soko lipo, sasa tunaelekea katika kutekeleza sera ya viwanda ili kuhakikisha tunaya- *branding*, tunaya-*pack* vizuri na tunayauza nchi za nje.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na kunipa nafasi wadau wa kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri anayoyatoa, mkwezi na mkulima. Lakini mimi swali langu liko hapa hapa, kwa kuwa na vanila nayo ni moja katika zao lenye bei kubwa linaloongoza kuliko mazao yote,

na kwamba wakulima wetu wa vanila wameshajihishika sasa kulima vanila, lakini tatizo lao ni mbegu na utaalamu wa kupatikana hiyo vanila.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu liko hapa. Je, kuna utaratibu gani wizara yako ya Biashara na Viwanda kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuwapatia mbegu za kutosha wakulima wa zao la vanila, ili waweze kulima vanila na iweze kuuzika ndani na nje ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kujibu swali lake Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo.

Kwa vile suala hili limehusu sana Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, naomba nichukuwe fursa hii kwanza kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda kwa majibu yake mazuri ambayo anaendelea kuyatoa. Namshukuru sana kwa kuendelea kuwatetea wakulima na wakwezi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba kweli hivi sasa zao la vanila limekuwa ni la bei ya juu kushinda zao lolote lile la viungo na mazao yanayopatikana hapa Zanzibar. Nataka niwathibitishie wananchi kwamba kwa kilo moja ya vanila ambayo imetengenezwa katika kusarifiwa kwenye kiwango chake inauzwa kwa zaidi ya Dola 700 kwa kilo, bei ambayo ni kubwa na inawapasa wafanyakazi sasa hivi kuelekea katika zao hili la vanila ili kujikomboa na kuondoa umaskini katika ukulima.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba mbegu za vanila ni kipande tu cha mvanila wenyewe na mivanila tunayo mashamba ipo mingi sana. Naishukuru sana Kamati ya Wizara yangu imetembelea mashamba ya vanila na tumewaelekeza utaalamu wa kupata mbegu za vanila. Wizara bado inatoa mafunzo kwa wakulima, inatoa mafunzo kwa wananchi na vikundi ambavyo vipo tayari kuzalisha zao la vanila.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa nataka nioneshe takwimu za wazi kwamba Zanzibar hatujawa na uwezo wa kuzalisha hata tani moja ya kusafirisha nje. Wakati soko la China linahita zaidi ya tani 10 kwa mwaka. Kwa hivyo soko lipo na Wizara ya Biashara na Viwanda ipo tayari kutengeneza *branding*, ipo tayari kutengeneza *packaging* na usarifu unafanywa pale katika kiwanda chetu kilichopo pale Kizimbani.

Kwa hivyo, nataka kuwajulisha kwamba wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wapo wenye kuweza kusarifu mazao haya na wapo wenye kutoa elimu hii. Kwa hivyo, sisi Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, wafanyakazi wetu tutashirikiana na Mhe. Mwakilishi, tutakwenda Pemba ambako nako wameshajihika kwa kiasi fulani, kwenda kuwapa ujuzi na utaalamu huu. Katika suala hili tutafuatana na wana kamati wa Wizara yetu bila ya shaka tutaendelea kuwapa elimu na taaluma juu ya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwahamasisha sana wakulima wahamie kwenye zao la vanila, mashamba ya mfano tunayo na tumeshirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda kutoa eneo la kusarifia namna gani mazao yale yanaweza kuwa na soko zuri kule nje. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 120

Kutangaza Utalii Kisiwa Cha Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Pamoja ni jitihada za kukuza utalii Zanzibar na kuweza kuongeza pato la taifa bado haujafanyika, juhudi za makusudi za kuitangaza Pemba kiutalii na kuongeza pato la nchi.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kwa juhudi za makusudi za kuitangaza Pemba kiutalii.

(b) Ni vipaumbele gani vya utalii vilivyopo Pemba ambavyo utalii utaanza na vitu hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 120 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Kamisheni ya Utalii inaendelea na juhudi zake za kuitangaza Zanzibar kiutalii ikiwemo Pemba. Njia tunazozitumia ni ushiriki wa maonesho ya kitaifa na kimataifa yanayohusu utalii, kuchapisha majarida na kuvionesha vivutio vya utalii, kuweka taarifa za vivutio katika tovuti ya Kamisheni ya Utalii, kuandaa *DVD* zinazoonesha vivutio na kuzisambaza wakati wa maonesho ya kimataifa pamoja na kuzipeleka katika ofisi za Mabalozi wa Tanzania. Aidha, serikali inaendelea kuimarisha miundo mbinu na mazingira mazuri ya biashara katika Kisiwa cha Pemba, ili kuweza kuvutia uwekezaji, jambo ambalo litashajihisha watalii kutembelea katika maeneo yaliowekezwa kiutalii.

(b) Mhe. Mwenyekiti, vipaumbele vya utalii vilivyopo Pemba ambavyo utalii utaanza navyo ni kama ifuatavyo.

(i) Kuwepo kwa chumba cha chini ya bahari. Hivi sasa kuna mradi mkubwa wa nyota tano wa "*Luxury tents*", ambao tayari umeshapitishwa na *ZIPA* na ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza karibuni.

(ii) Utalii wa michezo ya bahari ni kipaumbele chengine cha utalii katika kisiwa cha Pemba. Kuwepo kwa kisiwa cha Misali na mkondo wa Pemba (*Pemba Channel)* kunatoa fursa ya michezo ya baharini kisiwani Pemba.

(iii) Utalii wa michezo ni kipaumbele chengine cha utalii kisiwani Pemba. Kwa maumbile yake, Pemba ni kisiwa kizuri kwa michezo hasa ya kuendesha baiskeli na kukimbia (*triathlon and marathon*), michezo ya kitalii ya" *eco challenge*" na mingi yenye mnasaba huo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, amekitaja chumba cha chini ya bahari na michezo

ya baharini, michezo ya kuendesha baiskeli, michezo ya kukimbia ya *marathon* na michezo ya utalii ya *eco challenge*.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni michezo ya kuleta. Mimi namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba kipindi alichokuwepo Marehemu Dkt. Omar Ali Juma aliisajihisha sana mchezo wa ng'ombe na ulikuwa kila mwezi au kila baada ya *weekend* lazima mchezo huu uchezwe kule Pemba. Lakini pia Dkt. Salim Ahmed Salim pia aliushajihisha sana mchezo huu. Lakini mchezo huu sasa hivi umekufa au hauonekani tena kwa mnasaba wake. Sisi tunatizama mchezo wa ng'ombe wa *Spain* lakini hapa wa kwetu sisi hauonekani.

(a) Je, niiulize wizara imejipangaje kuhusu mchezo huu ambao kwa Zanzibar unachezwa maeneo sana ya Mchanga Mdogo au ya Pujini, ili na watalii waweze kuja kuufuatilia mchezo huu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba amejipanga vizuri kwa miundombinu. Mimi namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba usafiri ndio chombo pekee cha kupeleka watu Pemba na kurudi. Nimuulize tu kwamba watalii watakwenda na chombo gani kule Pemba, wakati sisi wenyewe usafiri haututoshi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara ina mpango wa makusudi wa kuhakikisha kwamba ile michezo yote ambayo haionekani. Mhe. Mwenyekiti, nachukua ushauri wake kwamba michezo ile tutahakikisha kuwa wizara tumeirejesha. Vile vile naomba Mhe. Mwenyekiti, nimjibu Mhe. Mwakilishi mwenzangu kwamba kwa upande wa mchezo wa ng'ombe yeye mwenyewe ni shahidi hata matamasha yetu ya Zanzibar ambayo yamefanyika mwaka huu huu, mchezo wa ng'ombe umeonekana ukichezwa siku hadi siku.

(b) Mhe. Mwenyekiti, suala la usafiri ni kweli kwamba ni tatizo kwa sasa hivi, suala la usafiri kwa Pemba. Lakini tutashirikiana na Mhe. Waziri Dkt. Sira Ubwa ili kuona kwamba usafiri umerejea kwa watu wa Pemba, lakini pia na watalii wetu pale watakapokuja katika kisiwa cha Unguja na kwenda katika kisiwa cha Pemba. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, swali langu lina vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Mwenyekiti, tumeona matamasha au maonesho mbali mbali ya biashara ya utalii yakifanyika nje ya nchi kwa ajili ya kutangaza nchi zao. Lakini kumekosekana kwa wawakilishi mara kwa mara kutoka Kamisheni ya Utalii ambao ndio wenye jukumu la kwenda kuitangaza Zanzibar nje ya nchi na kuleta au kutoa vivutio na sifa ya Zanzibar, ili watu wa kule waliokwenda kupeleka ile biashara waweze kukubali na kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Je, ni gharama gani au ni kiasi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia wizara yako imetenga kwa ajili ya suala zima la kutafuta masoko ya utalii nje ya nchi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mpaka sasa hivi katika visiwa vyetu vya Zanzibar hakuna hakuzidi vyumba 3,000 vya mahoteli ya watalii na sisi tunatangaza utalii nje ya nchi.

Je, tumejipanga vipi ili kuona kwamba wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika suala la utalii kuwapa *specification* ili kuweza kuongeza wingi wa vyumba mara baada ya kuitikia katika matangazo yetu kule, wale wageni watakaokuja kukaa hapa wawe na nafasi ya kutosheleza kuliko sasa hivi ambapo vyumba vyetu viko chini ya elfu tatu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, gharama ambayo imetengewa Kamisheni ya Utalii kwa ajili ya kuitangaza Zanzibar kiutalii, namuomba sana Mhe. Mwakilishi kwamba asubiri bajeti yetu keshokutwa, ataona kile ambacho Kamisheni imetengewa kwa ajili ya kuendelea kuutangaza utalii wetu wa Zanzibar kwa nchi ambazo zipo au tunatangaza utalii huu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali katika kujipanga kwa suala la kuongeza vyumba vya kukaa watalii kiasi ambacho inaonekana kwamba kama alivyosema kuwa vyumba vilivyopo havikidhi haja. Katika swali langu mama (b) nilijibu kwamba tuna mradi ambao utakuwa ni *luxury tents* ambao lengo na madhumuni ni kuongeza vyumba kwa ajili ya malazi ya wageni ambao watakuja kutembelea au watalii watakaokuja kutembelea Zanzibar. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Makame Suleiman.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naitwa Suleiman Makame. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kwa sababu na Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo amekosa atapata nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba wanatangaza utalii na kunatengwa pesa maalum kwa ajili ya kutangaza utalii. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika kuutangaza utalii katika jimbo langu Mkumbuu kuna kaburi ya Mwanamwari na nyumba ilioko chini ya bahari pamoja na kisima. *(Makofi)*

Je, imetembelewa mara ngapi na watalii hao.

Lakini pia wizara yako ina mpango gani wa kuweka alama ile nyumba ilioko chini ya bahari na kile kisima ili kuonekana kwamba eneo lile lipo na linaendelea kuwepo *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusu yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kutembea kwa wageni katika kijiji kile niseme tu yeye mwenyewe atakuwa ni shahidi na ni Mwakilishi wa jimbo lile, wageni wanakuwa wanakwenda marakwamara kwasababu wanakwenda kule kuangalia historia ya eneo lile, kwa hiyo ni kweli kwamba wageni wanakwenda kutembelea na kupata historia ya sehemu ile ambayo ipo, lakini vile vile kwa vile sifa alizosema zipo kwamba kuna kisima, sasa hivi tuna hatua za makusudi kwamba sehemu ile tuiboreshe na mwaka huu wa fedha tutaanza kuboresha kwa eneo lile kwanza kwa kuweka ukuta lakini na hili alilolisema pia tutalifanyia kazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Nam. 27

Ukarabati wa Nyumba ya Maendeleo Iliyopo Kengeja

Mhe. Foum Mussa Foum – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, Nyumba ya Maendeleo iliyopo Kengeja imekuwa mbovu sana, miundombinu yake yote hivi sasa haifanyikazi vizuri na hata hairidhishi hivi sasa kwa kuishi watu.

(a) Je, Mhe. Waziri hili unalifahamu?
(b) Je, wizara ina mpango gani wa dharura ili kuhani nyumba hiyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa Nyumba ya Maendeleo iliyopo Kengeja ni mbovu sana na miundombinu yake yote hivi sasa haifanyi kazi vizuri na hata hivyo hairidhishi kwa kuishi watu.

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inalifahamu suala hili na tayari Shirika la Nyumba Zanzibar, kwa kushirikiana na Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia (KIST), limefanya uchunguzi wa awali wa nyumba hiyo ambayo ripoti ya awali inaeleza kuwa msingi wa nyumba hiyo bado upo madhubuti, ila jengo lenyewe *(superstructure)* lipo katika hali mbaya. Ripoti hiyo imeeleza kuwa inashauriwa ufanyike uchunguzi wa kina ili kujua ni jinsi gani jengo limefeli na njia gani zitumike ili kuitengeneza pamoja na gharama za matengenezo yake.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa ili kuweza kutengeneza nyumba hiyo kunahitajika kufanyika uchunguzi wa kina utakaosaidia kutoa maamuzi sahihi juu ya hatua za kuchukua katika kuitengeneza nyumba hiyo. Kwa sasa tunasita kuingia katika

gharama kubwa za matengenezo, kwani kwa makisio uwezekaji tu wa paa unagharibu zaidi ya shilingi milioni 200. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Foum Mussa Foum: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize suala moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba nyumba ya maendeleo iliyokuwepo Kengeja hivi sasa hairidhishi kuishi watu na kwa kuwa majibu yake aliiyojibu amesema kwa sasa wanasita kuingia katika gharama kubwa za matengenezo ya nyumba hii.

Je, Mhe. Waziri ni lini mutaingia katika matengenezo hayo ili kuihami ile nyumba na kuwahami wananchi wanaoishi pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Foum Mussa Foum swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzoni kwamba baada ya kufanyika uchunguzi wa kina wakujua kwa nini imefeli nyumba, ndipo tutakapoanza hayo matengenezo. Lakini pia tupo katika mazungumzo na wale wanaoishi mle ndani, namna gani tufanye kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yanastahiki kuchunguzwa tukikamilisha hayo basi ujenzi utaendelea. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusu yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika nyumba ambazo nazifahamu nyumba ya Kengeja naifahamu, ni nyumba ambayo tuseme ukweli haistahiki kuishi binadamu, kwa wale wanaokaa Pemba na wale walizoziona ni kwamba hazistahiki kuishi mwanadamu, sikatai. Nitauliza swali sikatai kutengenezwa lakini nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwa niaba ya serikali, ni lini wale watu wataondoshwa mle kwenye ile nyumba ili kuepuka magonjwa na maafa, na ni kiasi gani cha maafa kimetengwa kwa watu wale baada ya maafa. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Abdalla Ali Kombo swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema tupo katika mazungumzo nao kwa sababu ikumbukwe kwamba wengi kama sio wote waliokuwa wanaishi pale zile nyumba walipewa kama fidia. Sasa unamtoa mtu kwake kuwe kuwa na mazungumzo, kwanza kufahamu baada ya kufahamu ndipo inapokuwa rahisi kutekelezeka yale mengine, ndipo yanapokuwa rahisi kutekeleze yale mengine, sasa hatujafikiria huko, kwamba tumezitenga kiasi gani kwa ajili ya maafa kwamba yatatokezea kesho, bali tunachofanya ni mzungumzo wafahamu kwamba hii nyumba imetokana na nini uharibifu huu na kuendelea kukaa hapa kunahatarisha ni kwenu na nini tufanye tukishamaliza hayo basi nadhani njia muafaka itapatikana. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana pamoja na majibu mazuri sana Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri kutokana na jibu lako la msingi serikali imeonekana haiku tayari nyumba zile za maendeleo wakati nyumba zile zimekuwa mbovu sana na kwa sababu suala la Mhe. Mussa Foum linashabihiana sana na nyumba za Kilimani, na Nyumba za Kilimani sasa zote zimejaa maji katika mastoo yake, ni nini hatua ya dharura serikali imejipanga.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuna tofauti nyumba zinatafautiana kuna nyumba utamkuta mtu anakaa ni ya kwakwe, kuna nyumba nyengine anakaa ni ya serikali. Kwa hivyo, tofauti hata *treatment* yake, lakini niseme serikali kwa ujumla kwa sababu ilikuwa ina dhima ya kuhakikisha wananchi wake wanakaa katika makazi bora tutajitahidi kuwaangalia nini kinahitajika kifanyike kwa kila nyumba husika. Ahsante sana.Mhe. Waziri *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa Kanuni zetu muda wa maswali umekwisha, lakini natumia kanuni hiyo hiyo kwa kuongeza dakika 15 ili tumalizie haya maswali yaliyobaki. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Nasimama kwa kutumia Kanuni ya 63, lakini halikadhalika naikazia kanuni yangu hiyo kwa kutumia nambari 42(1) ambayo inasema baada ya muda wa maswali kwisha, mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja kwa Baraza liahirishe shughuli zake zilizoorodheshwa katika Orodha wa Shughuli za Baraza na lijadili jambo la dharura na muhimu kwa umma kwa ruhusa ya Spika.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Gavu ana tabia ya kugeuka nyuma

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sijakuruhusu bado.

Mhe. Simai Mohammed Said: Haya, ahsante basi na Mhe. Gavu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nimekufahamu, lakini niliposimama nikasema kwa mujibu wa kanuni zetu muda wa maswali na majibu umekwisha ni saa 4:30, lakini kwa Kanuni hiyo hiyo kiti kinauwezo wa kuongeza muda ili tumalize yale maswali yaliyobaki. Kwa hivyo, ndio maana nikatoa taarifa ile ili Waheshimiwa Wajumbe wajuwe tuendelee na tumalizie yale maswali yaliyobaki, baada ya maswali utaleta hoja yako. Nawashukuru.

Nam. 45

Uajiri wa Wataalamu wa Afya Hasa Madaktari na Wafamasia

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali yetu iliongeza kiwango cha Bajeti ya Wizara ya Afya kutoka Tshs. 44.2 billioni kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Tshs. 58.7 billioni kwa mwaka 2017/2018 pamoja na kupatiwa ruhusa ya kuajiri wafanyakazi ambao watapunguza upungufu wa wafanyakazi kwenye maeneo mbali mbali Unguja na Pemba hasa Madaktari na wafamasia.

(a) Je, hadi sasa ni wafanyakazi wangapi wapya waliokwishaajiriwa hadi kufikia Disemba, 2017.

(b) Je, kutokana na ongezeko hili la bajeti na ajira kwa wafanyakazi, Wizara ina mpango gani wa kupeleka wafanyakazi wa ngazi za Mganga Msaidizi kwenye vituo vya Msuka, Kiuyu Kipangani na Mkia Ng'ombe ambavyo havina wafanyakazi pamoja na kwamba zipo nyumba za kuishi za wafanyakazi hao.

(c) Je, kwa nafasi za ajira ambazo wizara imeshaajiri hadi sasa imepeleka wafanyakazi wangapi Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 45 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Wizara ya Afya napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru sana na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya Uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kutoa kipaumbele kikubwa kwa Wizara ya Afya, kwa dhamira ya kuimarisha huduma bora za afya katika hospitali na vituo kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo sasa naomba kujibu swali (a) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuanzia Juni hadi Disemba 2017, wizara imeajiri wafanyakazi 252 ili kufanyakazi katika hospitali na vituo vya afya Unguja na Pemba. Miongoni mwa hao wamo madaktari 4, wauguzi 132, wafamasia 2, fundi sanifu wa maabara 18, fundi sanifu madawa 9, fundi sanifu vifaa tiba 2, Afisa Tabibu 32, Afisa Tabibu Meno 10, Afisa Ustawi Jamii 12, Afisa Mazingira 16, Afisa Ushauri Nasaha 4, Wakemia 2, Mtaalamu wa *"Microbiology*" 1, Mtaalamu wa "*Moliculary Biology*" 1, Mtaalamu wa Chakula "*Food Science*" 1, Afisa Habari Mawasiliano 4, Mtaalamu wa Viungo Bandia 1 na Afisa Uendeshaji 1.

Mhe. Mwenyekiti, waajiriwa hao wamepangiwa kazi kama ifuatavyo:-

Wafanyakazi 180 wamepelekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Na hili lilikuwa ni ombi maalum lenu Waheshimiwa Wawakilishi mlilokuwa mkiomba muda mrefu kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja iongezwe wafanyakazi. Wafanayakazi 52 wamepelekwa Pemba na wafanyakazi 20 wamepangwa katika vituo mbali mbali vya Afya Unguja. Aidha, uhaba wa wafanyakazi katika baadhi ya hospitali na Vituo vya Afya, tunaendelea kukabiliana nao kwa kuwapeleka wafanyakazi kwa kadri tutakavyoajiri.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali (b) naomba kufanya masahihisho kidogo kwa kulieleza Baraza lako tukufu kwamba hawa waganga wasaidizi walioliziwa, (*Medical Assistants*) kwa sasa tunawatambua kwa jina la Afisa Tabibu yaani (*Clinical Officers*). Wataalamu hawa ni miongozi mwa wafanyakazi walioajiriwa na tayari wameshapangiwa kazi katika vituo mbali mbali kikiwemo Kituo cha Afya cha Msuka, Kituo cha Afya cha Kiuyu Kipangani na kituo cha Afya cha Mkia wa Ng'ombe.

(c) Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2017 hadi Mei 2018 jumla ya wafanyakazi 123 wa kada mbali mbali nilizotangulia kuzitaja wameajiriwa na kupelekwa kisiwani Pemba. Wizara ya Afya inawaomba wananchi waendelee kuiamini serikali yao na kupata huduma za afya zilizo bora katika hospitali na vituo vilivyo karibu na maeneo yao, kwani lengo la serikali ni kufikisha huduma bora popote walipo wananchi. Tunawaomba wawape mashirikiano ya kutosha wataalamu hawa ili dhamira ya serikali iweze kupatikana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza, lakini na mie kidogo kwanza nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na upembuzi na ufafanuzi wa kina alioutoa katika majibu yake, inaonekana wamejipanga kwenye hilo jibu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo pamoja na kwamba ulisema kwamba ilikuwa ni ombi maalum la kupeleka wafanyakazi au kuongeza wafanyakazi kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja na kwa sababu sio Pemba mpaka juzi mwezi wa Mei.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Seif Abeid naomba uliza swali la nyongeza.

Mhe. Omar Seif Abeid Nauliza ndio nakuja huko, Mhe. Mwenyekiti, naomba ili anielewe. Umeshatupelekea wafanyakazi, lakini pia wizara hii ilishawahi kujibu kwamba kule Pemba hakuna Mfamasia na hapa Wafamasia mumeajiri.

Je, nilitaka nijuwe ni Wafamasia wangapi katika walioajiriwa ambao wamepelekwa Pemba ili kutatua tatizo la upungufu wa Wafamasia kule kisiwani. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi makini wa Jimbo la Konde, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nilisema tumeajiri wafamasia 2 na wafamasia hawa wote tumewapeleka Pemba ili kuziba pengo na uhaba wa wafamasia katika kisiwa chetu. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kuniona maana nishanyanyuka zaidi ya mara nne mpaka tano lakini nakusukuru kwamba sasa hivi macho yako kidogo umeniona.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niipongeze serikali kwa kupitia Wizara ya Afya kwa kuwaajiri wafanyakazi hawa ambao wataondoa matatizo makubwa ya wananchi lakini tu pale ambapo wananchi hawa watahitaji mahitajio maalum kwa kupitia Wizara ya Afya, basi wataweza kupata kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa mgao huu uliogawa kwa Wizara ya Afya umezingatia sana zile Hospitali kubwa na miongoni mwa hospitali hizo ikiwemo Mnazi Mmoja na katika suala lako jibu mama umesema kwamba Mhe. Omar Seif Abeid kwamba anailalamikia Hospitali ya Mkia wa N'gombe pamoja na Msuka kwamba hawa umewafanyia kazi pamoja na wafamasia hakuna. Je, tatizo hili ni lini sasa litaondoka kwa sababu umesema kwamba wamepelekwa lakini Mkia wa N'gombe pamoja na Msuka hawakupangiwa. Je, ni lini watapangiwa ili kuweza kuondoa lile tatizo ambalo lipo maana bado hili tatizo bado lipo hawajapelekwa. Mhe. Mwenyekiti na kushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti inaelekea Mhe. Mwakilishi alikuwa hasikilizi majibu

niliyokuwa nayajibu. Katika jawabu langu la msingi nimesema miongoni mwa vituo ambavyo vimepelekwa wafanyakazi ni kituo cha Mkia N'gombe, kituo cha Msuka. Kwa hivyo hayo maeneo ambayo umeniuliza sasa hivi yote ni maeneo ambayo tayari tumeshapeleka wafanyakazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nami niulize swali langu kwa haraka haraka. Kwa kuwa Zanzibar sahivi tumeshikwa na maradhi ya homa siku kwa jina sahihi linaitwa homa ya muungano na serikali iliweka kituo cha Wizara ya Afya kituo cha Ziwani kuwa ni sehemu ambayo iliyokuwa inapata tiba pamoja na Mnazi Mmoja, na kwa kuwa hivi sasa hadi jana usiku kituo hichi cha Ziwani hakifanyi kazi wagonjwa wote wanarundikana Mnazi Mmoja na kwa kuwa huko Mnazi Mmoja madaktari ni kidogo, wagonjwa ni wengi hatua gani unachukua ya dharura kuona kwamba wale watu kule hawapati usumbufu mkubwa, wagonjwa wanaendelea kuingia saa hadi saa. Hatua gani ya dharura itaweza kuongeza madaktari kuweza kuwatibu wagonjwa hawa Mnazi Mmoja pamoja na kufungua sehemu ya Ziwani. Ahsante, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza hatuna taarifa kwamba kituo cha Ziwani hakifanyi kazi, sisi tunajua kinafanyakazi na kina haki ya kufanyakazi kuwatibu wananchi wa Zanzibar kimesajiliwa. Lakini vituo vyengine vyote vya serikali viliopo Unguja pamoja na hospitali zake zote zinatoa huduma hii kwa wagonjwa ambao wanapata tatizo hili bila ya matatizo yoyote. Kwa hiyo kama wananchi wana tatizo la kwamba kituo kile kimefungwa kile ni kituo kimoja lakini vipo vituo vingi ambavyo vinatibu na vinatibu wananchi wote bila ya ubaguzi wowote, hivyo tunawaomba wananchi waende katika vituo vya afya vilivyo karibu nao ili wapate huduma hii ipasavyo.

Nam. 41

Matumizi Mabaya ya Mitandao Nchini

Mhe. Said Omar Said – Aliuliza**:**

Maendeleo ya haraka ya mawasiliano yameleta faida kubwa kwa watumiaji na wananchi kwa huduma kama kutuma na kupokea fedha na kufanya malipo ya huduma na bidhaa na kutumia mtandao wa "*internet*" kupitia simu ya mkononi, hata hivyo wapo wachache wanaotumia vibaya kama vile kufanya uhalifu.

Je, ni wahalifu wangapi waliotiwa hatiani kwa wizi wa kutumia mtandao Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi Said Omar Said wa Jimbo la Wingwi masuala yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi alivyobaini kuhusu maendeleo ya haraka ya Mawasiliano na ndio uhalisia wa mambo kwani yameleta faida kubwa kwa watumiaji na wananchi kwa huduma kama kutuma na kupokea fedha na kufanya malipo ya huduma na bidhaa na kutumia mtandao wa *Internet* kupitia simu ya mkononi.

Mhe. Mwenyekiti, panapo mafanikio hapakosi changamoto. Kutokana na kubadilika mfumo wa utumiaji na usafirishaji wa fedha kutoka njia za asili na kutumia njia za kielektroniki, zikiwemo *mobile money, mobile banking, electronic transactions* ambapo kumepelekea wahalifu nao kutumia vibaya mitandao hiyo na kufanya uhalifu wa kimtandao iitwayo *cyber crime.*

Mhe. Mwenyekiti, suala la wizi limeanza na kuendelea na ndipo watu walipotanabahi kwamba kuna uhalifu huu unafanyika, uhalifu uligundulika baada ya watu wengi kuwa wahanga wa vitendo hivyo na kuanza kulalamika na hadithi zikaenea kwenye mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, pia Serikali katika kuhakikisha kwamba inadhibiti uhalifu wa mitandaoni imekuwa na mashirikiano ya karibu na Kampuni zote za mawasiliano kama vile *TTCL, ZANTEL, VODACOM, AIRTEL, TIGO* na *HALOTEL*. Aidha Serikali iko karibu sana na taasisi zote za usalama kama vile Polisi, TAKUKURU, *ZAECA* pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) ili kutoa ushirikiano mkubwa juu ya makosa yanayotokana na mitandao ya simu na *internet*, pale inapotumika isivyo halali kwa njia ya kufanya uhalifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuliona tatizo hilo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikaamua kutunga Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2018 (*The Cybercrimes Act, 2015).* Sheria hiyo ililetwa Baraza la Wawakilishi na kuridhiwa na Baraza. Lakini kwa kuwa Mahakama zetu za Zanzibar bado hazijaanza kutumia Sheria hiyo katika kuendesha mashauri ya kimtandao yanayopelekwa badala yake huwa wanayaendesha kwa kutumia Sheria ya makosa ya jinai. Hivyo mashauri yote yanayoripotiwa Mahakamani hufanyiwa kazi kama ni makosa ya uhalifu wa kawaida na hurikodiwa kama makosa ya jinai ya kawaida baada ya kurikodiwa kama makosa ya kimtandao. Kutokana na hayo, imekuwa vigumu kupata takwimu za wahalifu waliotiwa hatiani kwa wizi wa kutumia mtandao hapa Zanzibar.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri mwenyewe swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze sana kwa kutoa taaluma kuhusu matumizi mabaya ya mtandao, lakini karibuni tu hivi hapa Unguja alikamatwa mwizi wa kutumia mtandao na ilikuwa amrambe mtu ambaye sitotaka kumtaja sasa hivi hapa shilingi milioni tisa lakini alifanikiwa kupata milioni moja akatiwa mkononi. Je, Mhe. Waziri hili analielewa na kama analielewa mhalifu huyu alichukuliwa hatua gani za kisheria.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, mwisho sikusikia swali lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwakilishi naomba urejee Mhe. Waziri hajasikia.

Mhe. Said Omar Said: Ninasema kwamba hivi karibuni hapa Unguja alikamatwa mwizi wa kutumia mtandao na ilikuwa apewe shilingi milioni tisa hapo alipokwenda kutapeli, na akahusisha viongozi wa juu ili akubalike. Lakini kwa bahati alifanikiwa kupata shilingi milioni moja tu akatiwa mkononi. Je, hili Mhe. Waziri unalijua na kama unalijua. Je, mhalifu huyu alichukuliwa hatua gani.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Suala hili mimi binafsi sijawahi kulisikia lakini kama kuna mwizi kakamatwa kwa ajili ya wizi wa mtandao alikuwa anapaswa kupelekwa Mahakamani kama walivyo wezi wengine. Lakini kama kuna viongozi ambao nao wanashiriki kwenye hili kuweza kuwakomboa wanaofanya hivyo nafikiri hatutendi haki, kwa sababu wengi wa viongozi hao hata hapa Baraza la Wawakilishi, wengi tukiwa wanawake tumeibiwa mimi mwenyewe nikiwemo na tulichuliwa hatua tukapelekwa mpaka Polisi tukafika tulipofika halafu hatukuona matokeo yake. Kwa hivyo mimi nafikiria sasa hivi wanaohusika walichukulie kwa uzito unaostahiki ili suala hili likome.(*Makofi*).

TAARIFA

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nikutake radhi kwanza kwa sababu pale nilikuingilia kwa muda wako, lakini kwa kweli niliona kama muda wa maswali na majibu umekwisha, Mjumbe yeyote anaweza kutoa Hoja kwa Baraza liahirishe shughuli zake zilizooneshwa katika orodha ya shughuli za Baraza na lijadili jambo la dharura na umuhimu kwa umma kwa ruhusa ya Spika.

Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuchukua muda mrefu lakini nataka nitoe taarifa muhimu halafu serikali inaweza kuangalia kwa upande wake inaweza kufanyia kazi. Kwa hivyo naomba niendelee.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waheshimiwa Mawaziri nimekuwa napata hofu karibuni lakini kwa muda mrefu juu ya mdudu ambaye ameingia katika nchi yetu lakini hasa wananchi na wazee wetu mbali mbali wamekuwa wanatumia nafasi yao ambayo serikali yetu pamoja na utaratibu tulioweka wa kisheria na kama mumeuona karibuni kumekuwa kuna watoto wengi sana vijana waliokuwa chini ya umri wanaendesha hivi vipasola au *motorbike* vidogo vidogo hivi wenye umri chini ya miaka kumi na nane wengine mpaka miaka kumi, kumi na mbili wengine wanafika pahala wanapita chini ya Baraza la Wawakilishi na wanakwenda katika skuli zetu za jirani.

Sasa kwa mujibu wa sheria ya *Road Traffic Act* ya mwaka 2003 ukiangalia *section* namba 81 naomba niisome.

Kifungu Nam. 81(1) kinasema:

> *"A person shall not drive on a road motor vehicle of any class or description unless he or she is the holder of valid driving license authorizing him or her to drive a motor vehicle of the class of the description."*

Lakini ukienda *classes of motor vehicles* 82(1) zile ambazo zinawaruhusu ni A ambazo ni za maringi mawili ni *motorcycle,* lakini halikadhalika ukiangalia kifungu namba 83 cha sheria hiyo hiyo kinasema:

"Subject the provision of this part with respect to the competence and fitness to drive a driving license, shall not be issue to any person unless he is at least eighteen years of age for class A, B1 and C1".

Mhe. Mwenyekiti, watoto hawa ukiwaangalia kwa sura wanavyopita njiani tena siyo mmoja tunaangalia pengine kwa mamia wanaokaa mjini, wanaokaa maeneo ya nje ya miji, yaani tena wanatumia hivi vipasola vyenye *CC* kubwa kabisa, inawezekana hata wazee wao wanajua. Sasa mimi sina lengo kubwa sana la kuchukua muda wako mkubwa, lakini kwa faida ya jamii na hasa ukiangalia sasa hivi kwamba vyombo vya moto barabarani vimeongezeka na kwa usalama wa vijana wetu ziko familia nyingi zimeshaathirika tayari. Kuna familia moja watoto wawili wameshaumia na kuvunjika miguu wenye umri wa miaka kumi na tatu.

Sasa mimi sina lengo la kupata majibu hapa au tujadili haya maelezo niliyoyatoa hapa, nnachoomba serikali walipokee na walifanyie kazi kwa haraka sana ili hao watoto wanaopita njiani katika nyakati tofauti basi utaratibu wa kisheria utumike na kama inawezekana basi hata wazee ambao wanawanunulia watoto hawa hizi pasola na kuwapa basi utaratibu wa kisheria utumike na ili sisi kama jamii tuwe tunaonekana kama tunafata sheria kwa mujibu wa utaratibu tuliojiwekea. Haipendezi kabisa kuwakuta watoto hawa wanatumia hivi vyombo wakati sheria zipo na haziruhusi.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushuru sana na niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza, inawezekana isiwe hoja ya dharura kihistoria ikaonekana ina uzito lakini athari ambayo tunayochukua katika jamii yetu kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria tunazojipangia ni mbaya sana. Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana ahsante sana kwa kunisikiliza na nashukuru Wajumbe wa Baraza hili kwa kunipa nafasi hii kunisikiliza ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai kwa hoja yako hiyo na natumai serikali imeichukua na imeipokea na kwa mujibu wa sheria ambazo umezisoma na sheria hizo ndio za nchi yetu basi nadhani serikali walichukue hilo wafuatilie au labda kama kuna jawabu inaweza ikatolewa sasa hivi, lakini naona tuichukue serikali tulifanyie kazi hilo suala nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wajumbe kuna matangazo mawili kutoka kwa mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, wanaombwa baada tu ya maswali hapa na majibu saa tano hii wakutane kwa kikao cha dharura na Mwenyekiti pia wa Kamati ya Maendeleo Wanawake, Habari na Utalii Mhe. Ali Suleiman Ali naye pia ametaka Wajumbe wakutane katika ukumbi wa *VIP*.Waheshimiwa Wenyekiti mlioomba ruhusa hii naomba niwakumbushe kuwa majadiliano pia yanaendelea, kwa hivyo mkimaliza hiyo taarifa mtakayopeana kwa Kamati yenu basi naomba muhudhurie ili tuendelee na kazi zetu. Nawashukuru sana.

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea, sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwanzo katika hotuba hii Mhe. Hamza Hassan Juma atafuatiwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Mwanaidi Kassim ajiandae.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi naungana na wenzangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuja hapa tukiwa wazima wenye afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kuchangia hotuba hii kwa kumshukuru sana Mhe. Makamu wetu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuweza kutuletea hotuba yake ambayo iliyojaa nyama. Naamini Mhe. Mwenyekiti, mimi Balozi rafiki yangu sana na nataka nimtanie kidogo. Naamini hii hotuba kaandikiwa na mtu sahihi kabisa, kwa hivyo nataka nimwambie kwamba atutolee salamu sana na kwa kweli hotuba inajieleza na kimsingi ameielezea serikali ni namna gani ina mikakati gani na nini ambacho wanachokifanya na natumia pongezi hizi pia kukipongeza na kiti chako vile vile kwa jumla pamoja na serikali nzima.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze moja kwa moja Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika kitabu chake ukurasa wa 2, katika 5.0 inaelezea hali ya uchumi. Mimi kwa kweli nataka niipongeze sana Idara ya Uratibu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu kwa ukiangalia kitabu hiki kazi kubwa sana wameifanya wao na moja katika kazi waliyoifanya kuchambua hali ya uchumi wa nchi kuelezea uhalisia, lakini vile vile kueleza mpaka mafanikio ya baadhi ya ziara za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa kweli ni kazi kubwa waliyoifanya na kwa kweli naendelea kuwapongeza sana.

Sasa katika hali ya uchumi Mhe. Makamu wa Pili ameeleza hali nyingi, hali ya uchumi wa nchi yetu unavyoendelea, jinsi unavyokua, kwa hiyo asilimia ambayo aliyoitaja hapo karibu 6.8 kwa nchi zetu hizi za Kusini mwa jangwa la Sahara kwa kweli ni maendeleo makubwa sana. Kwa hivyo tunawaomba tu watendaji wetu wajitahidi kuhakikisha kwamba mkakati huo kwa kuhakikisha maendeleo ya Zanzibar yanafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia katika ukurasa unaofata ukurasa wa 3 ameelezea katika 9.0 ni namna gani kwamba hii mipango ambayo iliyosababisha uchumi wetu kuendelea kukua ni zaidi kuweza kuthamini na kupongeza jitihada za wawakezaji wazalendo wa hapa nchini. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii lugha aloitaja hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lugha hii kwa kweli inatakiwa serikali nzima waichukulie lugha hii kwa ajili ya kuifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia wawekezaji wazalendo kwa kweli wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hapa Zanzibar. Kwanza ukiangalia zile fursa za kupata mikopo kwa kweli zinakuwa ni ngumu sana na tulijaribu kupiga kelele sana kupitia *BOT* kuweza kupatiwa ile mikopo ya *BOT*, mikopo ya *SME* ambayo wenzetu kule Bara mpaka karibu bilioni 4 wamefika pahala wenzetu wanapewa, lakini kwa upande wa Zanzibar hakuna yeyote ambaye aliyefanikiwa lakini *steal* wawekezaji hawa wazalendo wameweza kuwekeza Zanzibar katika miradi mikubwa na kwa kweli lazima tuhakikishe kwamba serikali yetu kupitia taasisi zake zote wanawapa *support* kwa nguvu zote. Lakini Mhe. Mwenyekiti kwa kweli sisi kama Wajumbe, sisi moja katika kazi yetu kuwasemea wananchi wanyonge ambao hawamo ndani ya serikali na hata wale ambao waliokuwepo ndani ya serikali miongoni mwao hawa ni *private sectors.*

Mhe. Mwenyekiti, Mimi naomba sana, kuna baadhi ya wawekezaji wazalendo wanasumbuka sana katika kupata vibali kwa baadhi ya shughuli zao hasa za mambo ya ujenzi na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu hapa wameshaomba ndani ya serikali hii kupata vibali wanafika pahala mpaka miaka mitatu, miaka mitano, miaka sita. Sasa je hapa, hii lugha ya Makamu wa Pili wa Rais kweli hawa wenzetu wengine wanaisimamia vizuri. Sasa mimi naomba wenzetu watendaji ndani ya serikali na kwa bahati nzuri leo *pool* ya Mawaziri ipo ya kutosha pamoja kwamba imepungua lakini kwa kweli hii lugha tunataka iende kwa watu wote. Kwamba ule urasimu hasa kwa wawekezaji wazalendo basi uondoke na kila wanapokwenda waweze kusikilizwa waweze kufuatiliwa shida zao. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa hii kauli ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kweli wafanyabiashara pamoja na wawekezaji wazalendo watafarijika sana baada ya kusikia kauli hii. Lakini vile vile kauli hii ina uwanja mpana. Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya wawekezaji au wafanyabiashara wameikopesha serikali sasa hivi inafika mwaka wa pili wengine mwaka wa tatu, katika bajeti iliyopita niliwahi kulizungumza na nikatoa mfano hai nikataja hapa na nimejaribu kufuatilia kwa karibu, serikali walitoa lugha nzuri kupitia Mhe. Waziri wa Fedha, wakasema wanafanya ufuatiliaji wanataka kuhakiki madeni kwa sababu madeni mengine yalikuwa ni changamoto madeni yale yamehakikiwa Mheshimiwa, tena mimi ile *figure* ambayo nimeitaja kumbe ilikuwa ni ndogo baada ya kuhakikiwa yale madeni mimi nilisema yalikuwa ni milioni thamanini, lakini baada ya kuhakikiwa haya madeni anadai karibu zaidi ya milioni mia moja kama sikosei na kumi na mbili mpaka na kumi na tano.

Lakini mwananchi yule mpaka leo hajalipwa. Sasa je, leo wazalendo gani ambao tunawasaidia Serikali. Naomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili naomba uje ulitolee kauli kwamba hawa wawekezaji wazalendo kwa kweli ifike pahala Serikali iwasaidie kama kwenye mikopo wanapata tabu kukosa. Je, leo wao wameikopesha Serikali lakini vile vile ukija ukiangalia *ZRB* wanakuwa mstari wa mbele kila siku kuwapelekea seke seke. Sasa mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu sitaki kuzuia kifungu chochote cha bajeti, kwa kweli nategemea lugha nzuri ambazo tutakazojibiwa kwa kusaidia wananchi wetu, suala hili ni jambo muhimu sana naomba sana wawekezaji hao.

Mimi nashukuru kwa wale ma-*contractors* waliokuwa wameikopesha Serikali tunashukuru tunazo taarifa kwamba wamelipwa kwa kiasi fulani, pamoja na kwamba tunaambiwa hawajakamilishiwa lakini bado tunawashukuru Serikali ilisikia kilio chetu cha mwaka jana, lakini hawa wengine naomba na wao waweze kufidiwa kwa sababu kuna bajeti zao tunazipitisha, haiwezekani kwamba tunapitisha bajeti tunasema mapato yamekua lakini vile vile kumbe katika mapato hayo kuna sehemu ya mapato ya watu wengine.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hapa katika kifungu cha 11.0 Mhe. Makamu wa Pili wa Rais umeeleza vizuri mafanikio haya ya ukuwaji wa uchumi katibu zaidi ya asilimia 30 kwa mwaka yamepatikana kutokana na Mhe. Rais kuweza kusimamia vizuri mapato ya nchi. Kwa hivyo hili tunampongeza sana Mhe. Rais kweli amekuwa mkali sana lakini tunataka tuone na hatua zinazochukulwa. Mheshimiwa bado unaweza ukasikia tu tutachukua hatua lakini bado husikii

nani na nani kwa kweli wamechukuliwa hatua, lakini kwa kweli tunashukuru sana kwa namna Serikali inavyosimamia haya mapato.

Lakini chengine Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho nilikuwa nataka kukizungumza katika ukurasa unaofuata wa nne 12.0 “Miradi iliyoelezewa ile ya *TASAF* ambayo ya mashirikiano na Jamhuri ya Muungano, hapa mimi nataka kuzungumzia miradi ya *MIVAP*.

Mhe. Mwenyekiti mimi naiomba sana Serikali yetu kwamba kuna hii miradi ya *MIVAP* ambapo kupitia mashirikiano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanatusaidia sana hasa katika kujenga hizi barabara za vifusi, lakini tatizo barabara hizi za vifusi halafu zinaachwa zinachakaa halafu baadae inakuwa hata kupitika hazipitiki. Mimi naomba sana Mheshimiwa kama mfano kuna barabara ile inayotoka Mwera ikaja maeneo ya huku Fuoni kwa kweli ilikuwa ni kitu cha kusikitisha sana, pale Serikali ilikuwa tuweke mkakati tuikamilishe tu kwa lami. Lakini sasa leo kwa kuwa ni barabara muhimu hasa baada ya hapa panapoitwa Kibonge Mzungu na wapi kuwa panajaa maji barabara ile kwa kweli ingeliweza kusaidia sana. Naomba sana hii miradi ya *MIVAP* ili na sisi kuongezea nguvu basi Serikali yetu ingekuwa inatenga fedha maalum kwa ajili ya kusaidia kukamilisha kuweza kuweka lami na kuwapunguia kero wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, najaribu kwenda haraka haraka kwa sababu kuna mambo mengi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mazuri ameyaeleza kuhusu suala la amani, kuhusu hali ya kisiasa. Mimi kwa kweli nakupongezeni sana viongozi wetu jinsi gani mlivyokuwa watulivu, sasa hivi kwa kweli katika kipindi ambacho Zanzibar imetulia kisiasa kwa kweli zaidi katika hichi kipindi kuanzia mwaka 2015 kuendelea mwaka 2020. Tunaomba sana wananchi wetu tuendelee kuunga mkono Serikali yetu kwa ajili ya kuhakikisha amani na utulivu ili maendeleo yaweze kupatikana.

Ukurasa huo huo kifungu cha 14.0 Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameeleza vizuri kuhusu suala la maendeleo ya mafuta na gesi hapa Zanzibar. Kwa kweli tunaishukuru sana Serikali yetu kwa *speed* inayokwenda, utafiti umeanza. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa kulikuwa kuna kitu nilikuwa nakishauri, tayari kuna tafiti za mwanzo ambazo tulizianza kukagua yale maeneo kupitia ile ndege iliyokuja lakini vile vile baadae ikaja na meli na sasa hivi wako vijana wetu wanafanyakazi katika upande wa ardhini kwa ajili ya kufuatilia ile mistari kufuatilia utekelezaji wake.

Lakini kitu ambacho nakiomba kwa kuwa sasa hivi tunaingia katika mfumo au mchakato wa kufanya utafiti wa kutafuta mafuta na gesi, sasa hivi kwa taarifa nilizokuwa nazo kuna ramani ambayo itakayokuwa inatengenezwa kuhusu suala la maeneo ambayo yana *resource* za mafuta hapa Zanzibar, tunategemea kama kazi hiyo haijafanyika inaweza ikafayika kwa kutumia *drones* na sasa hivi ndio chombo kikubwa ambacho kinachotumiwa na ambacho kinaweza kuchukua picha kwa utulivu na kwa haraka sana.

Kwa hivyo naomba katika mchakato huo utakaokuwa umefanyika basi naomba eneo la Fungu Mbaraka musije mukaliacha nje, kwa sababu kama tunavyojua mipaka ya Zanzibar bado itaendelea kubaki ile ile ambayo kabla ya Mapinduzi. Kwa hivyo hili suala ambalo najaribu kulizungumza ili tunapofanya tafiti zetu za mafuta na gesi eneo hili kwa kweli tusije tukaliwacha kwa sababu hiyo ni haki ya wananchi wa Zanzibar.

Lakini vile vile katika eneo hilo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba sana katika hili zoezi lililoanza kufanyika huu mchakato wa huu utafiti, kuna matatizo yameshaanza kwa hao vijana wetu ambao waliokuweko *field,* suala hili sitaki nilizungume *public*, nitaomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Waziri husika wa sekta baadae kwa wakati wako mnitafute niwapeni hali halisi iliyokuwepo. katika jambo ambalo hatutakiwi tulifanyie masihara wala kulifumbia macho hata kidogo suala la shughuli za uchimbaji wa mafuta na gesi hii tunategema ndio itakuwa roho ya nchi. Sasa mtu yeyote atakayetaka kuanza kutuchezea *from the beginning,* mimi nafikiri na sisi tunamalizana naye hapo hapo, muhali hautotusaidia, hata akiwa mtoto wa nani, hii nchi si mtu hii nchi ni ya Wazanzibari wote lazima tuhakikishe kwamba uchumi wetu tunausimamia kwa vizuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwa haraka haraka katika ukurasa unaofuata limezungumzwa suala zima la *TEHAMA,* hapa nilikuwa nataka nije nipate ufafanuzi, katika suala zima la hii *TEHAMA* tumeambiwa tayari Mkongo wa Taifa huu unaoshughulikiwa na Serikali na nashukuru, kwa sababu mwanzo ulikuwa unasimamiwa na *ZANTEL* lakini *ZANTEL* kama tunavyoona mambo ya makampuni wakati mwengine yanayumba mambo ya kupeyana ubia na vitu vyengine, kidogo hali imekuwa sio nzuri tunashukuru sana baada ya Serikali kuchukua wenyewe huu Mkongo wa Taifa. Kwa sababu huu Mkongo tunategemea ni Mkongo ambao utaweza kusaidia kupata mawasiliano lakini vile vile kuongeza kupata mapato ya nchi vile vile.

Sasa kitu ambacho nilikuwa nataka ufafanuzi tumeambiwa umeunganishwa na *E- Health* na tukaambiwa kuna vituo katibu 24 vimeshaunganishwa na Mkongo huu wa Taifa. Sasa wananchi wanataka wajue. Je, baada ya kuunganishwa hivi vituo kutokana na hii *E-Health.* Je, wananchi wanafaidika nini au itasaidia nini inawezekana wengine wakawa wanajua lakini wananchi hapa ndio wanatakiwa wajue zaidi. Sasa hili naomba mje mtusaidie kupata ufafanuzi.

Ukurasa huo huo kifungu cha 19.0 Serikali imeelezea namna gani ya kufanya *feasibility study* ya kutanua uwanja wa ndege wa Pemba, kwa kweli mimi nashukuru sana, hasa baada ya kuambiwa kwamba tunategemea kuna ndege ya *Boeing 737* zinatarajia kutua kwa upande wa Pemba, kwa kweli hili tutashukuru sana kamaalivyosema Mhe. Suleiman Sarahan Makamo wangu kwamba tunagemea uwanja ukitanuliwa na ndege hizi zikaweza kutua basi tunaamini uwanja ule uwakuta unafanya kazi masaa 24.

Sasa kitu ambacho ninakiomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Maulid Diwani alisema hapa leo Zanzibar pamoja na mahoteli yote tuliyokuwa nayo, hapa leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameelezea namna gani nchi ambazo mashirika ya ndege yanatua Zanzibar moja kwa moja sasa hivi. Sasa hapa bado ipo fursa yapo mashirika ambayo yanataka kuleta ndege zaidi ya hizi zinazokuja hivi sasa hivi.

Lakini kuna vichangamoto kidogo hivyo vya Muungano hivi lazima tuvifanyia kazi hasa katika upatikanaji wa *viza*. Leo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nafikiri kama tulivyokuja Afisi kwako na baadhi ya wale wawekezaji wale wako *serious* kwa sababu tumeshafanya kazi na tumeshawaona, wana uwezo wa kuleta ndege nyengine kila wiki *direct* from Kazakhstani na Azerbaijan kila wiki abiria 250. Kwa hivyo ina maana kesho kama wakipewa kibali mkija mtapata *visa on arrival,* ina maana tayari kuna ndege nyengine ambazo zitaweza kuleta watalii elfu moja kwa kila wiki. Sasa hili mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hata

Waziri aliyekuwa wa Utalii analijua hili ame-*fight* nalo sana naomba sana Serikali ifanye hii jitihada.(*Makofi*).

Lakini sio hilo tu hawa vile vile wanataka kujenga hoteli kubwa yenye vyumba 150. Leo hoteli zetu zote kubwa hapa sijui kama kuna hotali inayofika vyumba 120, hawa kwa sababu wale watalii wanawatafuta wao wenyewe, kwa kweli tuwapeni maeneo na naamini Zanzibar maeneo yapo ili waweze kuwekeza kuweza kuongeza ajira. Lakini kitu ninachokushukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais milango yako ipo wazi, wewe unasema wache waje tutawasikiliza kama wakweli tutawapa *facility* wafanye kazi. Naomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais uendelee na uzi huo huo, kwa sababu wengine tunaambiwa aah! ukitaka kwenda kwa fulani bwana kuna vikwazo, kwako wewe mlango uko wazi hakuna vikwazo, tunakushukuruni sana kwa kuona jinsi gani mnavyoshirikiana na hili nafikiri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mkiweza kulisaidia nafikiri idadi ya watalii itaongezeka pengine kuliko hata ile tuliyotarajia katika mwaka uliopita.

Nakuja nukta 21 barabara ya Mahonda Mkokotoni. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakushukuruni sana Serikali katika mwaka ambao mmefanya jambo halijawahi kutokea ni kipindi hichi, leo barabara ya Mahonda Mkokotoni ni barabara kubwa katika barabara zetu lakini tayari mmeshalipa fidia *hundred percent* ni kitu ambacho cha kupigiwa mfano, huko kipindi cha nyuma kuna barabara hapa tulikuwa tumeshajenga wananchi bado wanakuja wanadai barabara tumeshatumia zaidi ya miaka mitano, sita mpaka kumi wananchi wanakuja kudai lakini leo umeshatanguliza.

Sasa kitu ambacho nakiomba kwamba hizi baraara ya Mahond\Mkokotoni hizi barabara ziko karibu nne, hawa wananchi wameshaambiwa itakwenda sijui kuna barabara Fuoni/Jumbi wapi na wapi.,Tunaomba Mheshimiwa zitafutwe fedha na Serikali hawa kwengine walipwe kabisa fidia, tumeona katika mpango wanata kuangaliwa katika bajeti ya mwaka unaokuja. Lakini mwananchi ukishamwambia hapa tunataka kutanua barabara kama una vipando vyako usipande tena, kama una nyumba yako usijenge tena, ina maana yule mwananchi tutakuwa tumeshamzuia.

Sasa hili mimi kitu ambacho nakiomba kwamba Serikali tuhangaike tutafute pesa tulipe fidia katika hayo maeneo mengine ili sasa wale makandarasi wetu wakija waweze kufanya kazi kwa utulivu na kwa sababu kwa taarifa tuliyopewa kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, kwa taarifa tuliyopewa kwamba hawa jamaa hawa ma-*contract* tuliowapata safari hii sio wa mchezo wanaleta meli nzima ya vifaa vyao meli nzima, ina maana hawa wamejiandaa kuja kufanya kazi na hizi barabara tunakusudia kama walivyokusudia wenyewe ndani ya miezi 18 wazimalize zote hapa tunakwenda mwaka 2020 iyena iyena tena tunapitia barabara hizo hizo.

Kwa hivyo mimi nadhani Mheshimiwa hili tukiweza kulipa fidia kwa haraka mimi nafikiri iyena iyena tutapitia barabara ya Mahonda/Mkokotoni/Jumbi na wapi. Kwa hivyo naomba sana Mheshimiwa hii fidia iangaliwe na wale wananchi wengine, kwa sababu wananchi ukishamwambia utalipwa fidia hawezi tena kufanya shughuli yoyote ya maendeleo pale anasubiri fidia ili afanye shughuli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, usinitizame naomba ikibakia dakika tano uniambie kwa sababu kuna kero za Muungano nataka kuweka kiporo kidogo. Mhe. Mwenyekiti, moja katika barabara ambayo haijalipwa fidia mpaka leo ni barabara ya Wete/Chake Chake. Barabara hii tokea mwaka 2009

wananchi hawawezi kulima, mwananchi yake nyumba zao kubomoa hawawezi kwa sababu wakibomoa hawajapata fidia hajui pa kuhamia. Naomba hizi fidia kwa bahati mbaya au bahati nzuri mwaka uliopita tulitenga bajeti hii, watu hawakulipwa fidia, basi naomba katika hii bajeti inayokuja safari hii hawa wananchi wa barabara ya Chake Chake/Wete na wao waweze kulipwa fidia ili kuhakikisha wanafanya shughuli nyengine.

Mhe. Menyekiti, nakwenda haraka haraka kifungu cha 22 ukurasa wa saba suala la maji. Kwa kweli sasa hivi baada ya mabadiliko baada ya kelele zetu Serikali tunakushukuruni mmetusikiliza mmefanya mabadiliko kidogo ya uongozi. Sasa hivi alhamdulillahi si haba tunayapata japo si siku zote lakini tunayapata, ndio maana siku hizi mnatuona tunakuja tunakoga kwa sababu maji angalau yanapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ninachokiomba bado Serikali yetu kuna rai sisi Kamati ya Ardhi na Mawasiliano tulileta ushauri huo, suala la kuhakikisha vile visima vya Ras el Khaimah tunaweka mradi maalum. Leo bado tunakuja na miradi mengine tunaangalia mpango gani lakini hatujaweka mkakati wa kuvifanyia *Installation* vile visima vyote. Naamini Mheshimiwa visima vile vipo katika majimbo yote ya Zanzibar, vikiweza kuunganishwa vile maji itakuwa sio tatizo tena tutakuwa tunazungumzia mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi wake zetu kidogo wataanza kuchana nywele maana vipara unajua tena mwanamme ana vipara, bibi ana kipara hajulikani ndani ya nyumba nani bwana nani bibi. Kwa hivyo tunaamini maji yakiweza kupatikana akina mama wetu hawa watapata utulivu katika maeneo yetu mbali mbali.

Suala la afya Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba ukija *at least* utupe *brief,* sisi tunashukuru Chama cha Mapinduzi baada ya kuona kwamba wananchi wanapiga kelele sana kwenye masuala ya afya walitutuma wananchi na ujumbe ule tukaufikisha kwako na tunashukuru ukaunda kamati ndogo tukenda tukafuatilia kero mbali mbali za Wizara ya Afya, kwa bahati mbaya leo hapa Waziri wa Afya simuoni lakini naamini *at least* angelitupa abc.

Sasa sijui ile ripoti kama mliwapa Wizara ya Afya kwa ajili ya kuifanyia kazi, kwa sababu ukiangalia bado changamoto Wizara ya Afya tunazo na ukiangalia kama sasa hivi kuna maradhi haya yaliyojitokeza yanaitwa maradhi ya Muungano. Sasa sijui yanaitwa ya Muungano sasa sijui yanaitwa maradhi ya Muungano kwa sababu yamekuja kwenye sherehe za Muungano au kwa kuwa yameanza pale Muungano. Lakini sasa maarufu mtu akiumwa anaambiwa maradhi ya Muungano, tunataka taarifa ya Serikali je haya maradhi yanaambukiza au yanakuja vipi kwa sababu utamaduni wetu Mheshimiwa mtu akiumwa ukenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kitanda kimezongewa na watu kumi. Sasa kama yale maradhi yanaambukiza ina maana wale watu kumi wakiondoka na wao wanayapeleka kwenye majumba yao.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine tunaogopa sisi kama viongozi wananchi wakiumwa wanatupigia simu Mheshimiwa tuletee gari, hatukufichi Mheshimiwa la kweli lazima tuseme na hapa tumekamata msahafu tunapeleka vikeri, mtu unaogopa kupeleka gari yako kwa sababu hujui pengine maradhi yale yanaambukiza unapokwenda kumchukua mgonjwa kumpeleka hospitali, maradhi yale na wewe umeyachukua, sasa tuambiwa haya maradhi yanaambukiza au hayaambukizi.

Mimi ndani ya Jimbo langu leo kuna Sheha wangu wa Shaurimoyo amenipigia simu akaniambia tayari kuna wagonjwa karibu mia mbili tayari wameshapatiwa huduma za matibabu, katika hao mmoja jana tumemzika mtoto mdogo ndio hayo hayo maradhi ya muungano, hiyo ni shehia moja tu. Sasa mimi ndani ya jimbo langu kuna shehia sita, sasa tuangalie ina maana ndani ya jimbo langu la Shaurimoyo zaidi ya watu 900 mpaka 1000 inawezekana ikawa wameshapata maradhi hayo, lakini tunashukuru kwamba huduma zinapatikana lakini pamoja na kwamba huduma zinapatikana mnapita na lile bomba lenu mnatutilia dawa tunashukuru *fumigation* inafanyika. Lakini kitu kikubwa tulichokuwa tunataka. Je, haya maradhi ni ya kuambukiza au sio ya kuambukiza ili tujue namna gani ya kuweza kujikinga.

Mhe. Mwenyekiti, chengine kwa haraka haraka nilikuwa nataka nizungumzie suala la chanjo sitaki nilizungumze Mhe. Suleiman Sarahan kazungumza kwamba akinamama wanapatiwa chanjo, sasa na sisi kinababa nafikiri alizungumza ile tezi dume kama nini basi tuweze kupatiwa hiyo chanjo kwa sababu unajua maradhi haya na hasa sisi tunaoambiwa tunafikia umri kuanzia miaka arubaini na kuendelea maradhi yanakuwa yanatunyemelea.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, kitu nilichokuwa nataka kukizungumza suala zima lile la eneo la Mangapwani. Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nashukuru na Kamati yangu vile vile tunashukuru na mpango wa Serikali waliokuja nao, kwamba eneo la Mangapwani ni eneo *very potential* na eneo lile kwa kweli kama nilivyosema pale wananchi wote waliowekeza pala hakuna mgeni wote ni wazalendo, lakini bado sijaiona *formular* ya kuweza kuwa- *compesante* watu wale. Mhe. Mwenyekiti, eneo lile kama hatukuweza kuliwekea mkakati maalum wengine wanaweza wakaja wakapunjwa, wengine wakafidiwa vizuri.

Kwa sababu kwanza kitu nilichokuwa nakiona Serikali eneo lile tayari wanafanya *feasibility study, feasibility Study* ile sijui kama imeshamaliza au haijamaliza, lakini tayari wale tumeshawasimamisha wasiendelee, lakini wengine wanaambiwa waendelee. Lakini vile vile mtu anaambiwa endelea halafu baadae tutakuja kulipa fidia tunaweza tukaja tukabambikiwa pale gharama ambayo hayana msingi. Hii mifano Mhe. Mwenyekiti, tumeshaiona Bara wenzetu kule Mhe. Magufuli aliwahi kwenda pale Uwanja wa Ndege *Terminal* III pale inayojengwa, alikwenda pale akazuia, akawaambia mimi kwa gharama hii sikubali mkandarasi funga vitu vyako nenda zako au tu-*bargain,* mkandarasi akakubali waka-*bargain.* Mhe. Mwenyekiti, ile bajeti iliyokuwepo ilipungua karibu kwa asilimia 25. Sasa leo mtu huyo anayeambiwa endelea tutakuja kulipa fidia, anaweza pale akaingiza gharama yasiyokuwa na msingi, yasiyokuwa na lazima kitu ambacho ninachokiomba kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu pale lazima wale ambao waliokuwepo pale wafungishwe mikataba na katika mikataba ile lazima kuwepo wataalamu, sisi tunayo Bodi ya Wakandarasi. Mheshimiwa Bodi ya Wakandarasi ina uwezo wa kuangalia kile kinachofanywa na gharama halisi itakayopelekwa serikalini ili kuhakikisha kama serikali gharama itakayobebeshwa iwe gharama halisi, tusije tukafanyiwa biashara, tumeona pale kwa kweli kuna uwekezaji mkubwa wengine wanafikia karibu asilimia 80, kuna wengine ndio kwanza asilimia 25, kuna wengine ndio kwanza asimilia 0. Sasa mimi naomba eneo lile lifanyiwe mikakati.,

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa baada ya dakika tano nilizokuengeza zile malizia dakika mbili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mheshimiwa nilikwambia ikifika baada ya dakika tano unambie hukuniambia haya nishasikia, nashasikia. Mhe. Mwenyekiti kuna mengine haya sijawahi kuyasema lakini najua Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais ni Serikali nzima tutakuja kuyazungumza katika wizara nyengine kitu ambacho nnachokitaka kukizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu hatutakiwi tuoneane haya Waswahili wanasema "ukimuonea haya mke ndugu basi watoto hupati". Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala zima la kero za Muungano. Mheshimiwa tulikuwa mwanzo tukaona tutazungumza kero za Muungano tukaambiwa tukizungumza kero lugha si nzuri inaudhi tukasema changamoto za Muungano. Changamoto za Muungano sasa hivi mumeshabadilisha mnasema masuala ya Muungano. Mheshimiwa bado mimi nataka niseme neno kero sasa hivi nabidi lirudi mwanzo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa sipendi kutaja watu kwa sababu unapotaja mtu unabidi uwe na *evidence* lakini hapa mimi nitataja mtu. Mhe. Mwenyekiti, kuna Mbunge anaitwa Keis. Huyu ni kero ya Muungano na Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wewe ni Mjumbe wa Kamati Kuu, mimi naomba nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo ni Mjumbe wa Halmashauri ya Mkoa wa CCM, naomba huyu Keis aitwe kwenye Kikao cha Kamati Kuu ahojiwe, aulizwe maneno yake aseme mbele ya Dkt. Ali Moh'd Shein, kwa sababu leo Keis anapozungumza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Yaani Zanzibar anahisi kama kwake ni kero, mtihani lakini kikubwa hebu tuangalie uraia wake mimi kwanza nishaanza kuwa na wasi wasi wake, mimi nishaanza kuwa na wasi wasi, mtu yeyote ambaye ni raia wa Tanzania hawezi akaizungumzia Zanzibar katika lugha ya kejeli au jeuri kama ile. (*Makofi*).

Mimi nafikiri kama si busara za viongozi wetu kuondoa pasipoti, maana zamani unapokwenda Bara kwa pasipoti, unapokuja Zanzibar kwa pasipoti, laiti kama ingekuwa si busara za viongozi wetu kama ingekuwa kwa pasipoti basi pasipoti ya Keis kuingia Zanzibar ingekua ipigwe X. Mimi ningeliomba asingie Zanzibar kwa sababu hatumjui anakuja na *issue* gani, ni mtu ambaye hana maana wala haisaidi nchi yetu na wala hafai kuitwa Mbunge wa CCM. Hili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba na hii *hansard* yangu naomba uichukuwe wende nayo kwenye Kamati Kuu. Huyu kwa kweli ni tatizo na kama mtataka nitowe ushahidi na mimi nitakuja kwenye hicho kikao nitakuja kueleza huyu anachosababu.(*Makofi*).

Mheshimiwa leo imefika pahala mpaka Waziri Mkuu ameingilia kati suala hili, jinsi unavyozungumzwa Muungano na Zanzibar inavyozungumzwa kwa upande wa ndani wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *source* ni huyu kuna kero ngapi tushazizungumza haya mambo mengine yanatekelezwa, mengine yanazungumzika, lakini sasa yeye sitengeze hiyo kero. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hilo nilisema niliseme lakini kikubwa zaidi bado kuna miradi ya Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, hii barabara ya Wete – Chake Chake niloisema, nimejaribu kufuatilia Bunge wanasema mradi huu tayari fedha zipo. Mheshimiwa pesa zipo toka 2009.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya. Pesa zipo toka 2009 mwanzo wakatwambia mkataba huu umeandikwa kwa lugha ya Kiarabu hauwezi kutafsiriwa, tukawambia upelekeni Chuo cha Kiislamu mkataba ushatafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza mpaka leo kesho, keshokutwa.

Wenzetu Mheshimiwa kule miradi ilikuwa wala haimo katika Ilani ya Uchaguzi, wala ilikuwa haipo katika mipango ya serikali, leo miradi imeshajengwa, sisi leo mradi toka mwaka 2009 tunahangaika nao. Mhe. Mwenyekiti, hili naliomba sana lakini vile vile suala la *Terminal II* tumeambiwa tayari pesa zishakubalika lakini mpaka leo pesa bado hazijapatikana, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, tunaathirika sana na kama nilivyoomba bado kikao kile naendelea kukiomba, mambo ya kila mtu kusema kwenye nyumba yake haifai, naomba sana kikao cha Wabunge na Wawakilishi.

Mhe. Jakaya Kikwete aliwahi kukutukutanisha mpaka hichi Kiswahili kinanitoka, tulikutana Wabunge na Wawakilishi wa CCM tukazungumza na akatwambia kama mna matatizo yetu zungumzeni katika vikao hivi. Sasa tunahitaji kikao hicho wao waseme ya kwao na Waziri Mkuu yupo na sisi tuseme ya kwetu na Makamu wa Pili wa Rais yupo tujue moja. Leo mambo haya ni aibu, leo kila Zanzibar sijui mwanzo tulikuwa tunapeleka magari tunakatwa ushuru, makontena tunakwepa ushuuru, sasa hivi sukari hiyo hapo. leo Zanzibar tunahangaika viwanda, tunaitikia mwito wa Serikali yetu, leo tayari sukari tunaambiwa magendo, yaani mpaka mivao ya kanga 10, leo mivao ya kanga 10 kama unataka ushahidi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais siku moja ma-*boardguard* wako waache, nenda peke yako Dar es Salaam, chukua mivao vyao 10 ya kanga ukipita pale bandarini tayari watakunyanganya watakwambia ulipe, ni aibu. Leo Mhe. Mwenyekiti, wanafaidika ndani ya Muungano ndani ya Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sudan ya Kusini, Rwanda wamekuja juzi wanafaidika, leo sisi ndani ya Muungano huu tunapata tabu kwa nini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti kuna mradi wa Afrika Mashariki ulikuwa unaitwa Rollon Rollo, Serikali ilitakiwa ijenge miundo mbinu ijenge bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Mombasa ili meli mfano kama hii ya Bakharesa mtu anaweza kuwa na gari asubuhi unakwenda kwenda Dar es Salaam unarudi jioni unakwenda zako Tanga unakwenda Mombasa. Sasa hivi miundo mbinu iko meli ya Bakharesa ipo, leo ukipeleka gari Dar es Salaam utafikiri umepeleka unga, lakini gari za Rwanda, za Burundi, watu tunaziona, leo gari ikatoke Sudan ya Kusini ije mpaka Kariakoo Dar es Salaam, leo gari inatoka Zanzibar ni tatizo.(*Makofi*).

Mheshimiwa naomba hicho kikao tukutane salamu hizi tupelekee kwa Mhe. Joseph Magufuli, tunaomba Wawakilishi wa CCM peke yetu, maana tusitiliwe chuwa, Wawakilishi wa CCM tuambizane kweli sisi huku suala la Muungano linatuharibia litatupunguzia *mass.* Leo sisi sekeseke tunayoipata kwenye uchaguzi moja *source* mambo ya Muungano.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii, lakini naomba hayo ambayo niliyoyasema serikali yafanyiwe kazi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Hamza kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kuna taarifa kabla ya kumpisha mchangiaji mwengine, tunatangaziwa kwamba ile shughuli yetu ya uchangiaji wa damu sasa itafanyika hapa Chukwani katika viwanja vyetu vya Baraza la Wawakilishi badala ya kufanyika Makunduchi. Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi tunaomba kuhudhuria kwa wingi katika shughuli hii, itakayoanza saa 3.00 asubuhi kesho kutwa Jumamosi. Vile vile wananchi wote wanaalikwa kuhudhuria kuchangia damu ili kuhami tatizo la ukosefu wa damu katika Benki yetu ya damu hasa wakati wa mwezi wa Mtukufu wa Ramadhani. Ahsanteni.

Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) atafuatiwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajiandae.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (**Dimwa**): Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nikachangia angalau maneno machache lakini mimi nitachangia tofauti sana na wenzangu, mimi nitajikita sana kwenye vifungu kwa sababu maneno mengi wameshayasema.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimuombe Mwenyezi Mungu aniongoze vizuri wakati nikichangia Hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais, aniondoshee jazba na kiburi wakati nikichangia hotuba hii. Lakini jengine Mheshimiwa nimpongeze sana Makamu wa Pili wa Rais wa uwasilishaji wake makini, wenye madaha mengi wakati akiwasilisha hotuba yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kitabu hichi kimesheheni mambo mengi sana lakini nitakuwa mtovu wa fadhila au mwizi wa fadhila kama sijampongeza sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa mchango wake mzuri aliotoa jana lakini nimpongeze sana mdogo wangu Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumza jambo zuri na mengi mazuri ambayo yamehusu Muungano wetu, lakini pia na uchumi wetu wa nchi yetu. Lakini vile vile, nimpongeze mdogo wangu Mhe. Nadir Abdul latif Yussuf naye amezungumza uzuri sana juu ya Muungano wetu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwenye ukurasa 2 kwenye namba ndogo 6.0, naanza hapa kwa sababu imetamkwa uchumi wa Zanzibar jinsi ulivyokua kwa asilimia 6.8. Ni jambo zuri sana kwa serikali yetu kutuonesha jinsi gani uchumi umekua kiwango hiki, lakini nataka kusema tu, jambo hili ni zuri sana walilolieleza lakini hata hivyo malengo ya *vision 2020* bado hatujayafikia kwa ukuwaji endelevu wa uchumi wetu kutoka asilimia 8 mpaka asilimia 10, na hii ina maana gani.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tulianzisha sheria ya *SMIDA* kuweka viwanda vidogo vidogo katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, sera hii naanza kuona kama tunaanza kuchupia gari kwa mbele. Tanzania wenzetu Dkt. Magufuli alikuja na sera ya viwanda na Zanzibar wakati mwengine tukisema tunasema tuna sera ya viwanda, mimi nataka kupingana nayo kwa Zanzibar.

Kwa nini tuwe na sera ya Viwanda Zanzibar kwa sababu moja, huwezi kuwa na taifa la viwanda lenye watu masikini watu wa Zanzibar ni masikini sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kivutio chochote cha viwanda lazima kiwe na soko, soko leo Zanzibar liko wapi. Mheshimiwa mdogo wangu Hamza kasema kuhusu kiwanda cha Sukari. Kamati yangu ilikwenda kutembelea na ikakuta tani nyingi zipo kule. Leo leo Zanzibar haifaidiki hata soko la ndani, lakini sisi seuze soko la Afrika Mashariki, lakini juzi mwezi uliopita nchi 14 za Afrika zimetia saini kwa soko la pamoja, nilikuwa najiuliza au napata ukakasi, hivyo wakati Zanzibar haifaidiki kwenye soko la ndani inaenda kufaidika wapi.

Hivi Zanzibar ikiwa haifaidiki na soko la Afrika la Mashariki, inakwenda kufaidika wapi, bado tuna kazi kubwa ya kufanya na kulinda viwanda vyetu lakini vile vile lazima tujenge uchumi wetu uwe uchumi wa kati, ikiwa watu wetu wanalalamika mmoja mmoja, wengi hawana ajira wanalalamika kipato kidogo, lakini wale wenye ajira wanalalamika kuwa mshahara haukidhi yale mahitaji yao ya kila siku tunajenga uchumi gani. Tulikuwa na Tume ya Mipango ndio inayoratibu uchumi wetu wa Zanzibar.

Sasa ningewaomba sana waangalie jinsi gani ya kuweza kuwasaidia Wazanzibari angalau basi waweze kujenga uchumi wa kati, mtu angalau aweze kwenda sokoni, lakini aweze kwenda *super market* kununua chochote. Mimi nishauri tu Serikali kwenye sekta hii kuongeza mapato. Tuongeze mapato yetu lakini tuangalie Zanzibar ni nchi ya visiwa, tuanze kuweka mfumo mwengine sana wa kupata uchumi wa visiwa unakuwaje. Tulitangaza bandari huru, sheria ipo kwa nini hai-*implement,* tuna tatizo gani haifanyi kazi, ili tuwe na ship-hub katika Zanzibar yetu. Zanzibar uchumi wake mdogo. Nataka niseme tena Mhe. Hamza amezungumza, leo mivao 10 ya kanga unakamatwa. Sasa ndugu zetu hawa wa damu wanafika pahala hawatuwaelewi, kwenye uchumi wetu huu mdogo, uchumi wa visiwa ni uchumi mdogo sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nishauri tu serikali kuangalia watu wake na kuunda uchumi uliokuwa imara na mimi najua serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni serikali sikivu sana, kwa hivyo naamini kipindi kijacho kidogo tutafanikiwa.

Lakini Mheshimiwa nije ukurasa 4 kwenye Miradi ya Pamoja ya Maendeleo ya Muungano. Nimpongeze sana mdogo wangu huyu Mkurugenzi kwa kazi kubwa sana anayoifanya, ni kijana makini wala chaguo la Rais hatuliingilii hapa, *hundred percent*. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika namba 13.0 Hali ya Kisiasa. Sasa mimi leo nataka nianze kusoma ilani ya Chama cha Wananchi (CUF) ninayo hapa. Mheshimiwa sitaisoma yote kwa sababu kubwa na naomba niinukuu katika sekta moja tu ambayo nimesema niweze kuizungumza hapa. Tutakuwa na huduma za viwango vya elimu vya uhakika, hii ilani ya Chama cha (CUF). Sasa naomba tu nitowe pahala kidogo anapoanza yeye. “Serikali ya Umoja ya Kitaifa itakayoongozwa na CUF itachukua hatua ifuatavyo:

Inajenga skuli mpya za kisasa na kuongeza madarasa kadri itakavyohitajika, kuondoa msongamano wa madarasa na mfumo wa mikondo miwili haraka iwezekanavyo, itaweka vigezo vya ukubwa wa darasa, idadi ya walimu na idadi ya vipindi kwa kila mwanafunzi katika viwango vinavyokubalika kimataifa na vinavyopelekea ukuwaji wa haraka wa viwango cha elimu". Lakini jengine wanasema wataanzisha utaratibu wa kufanya tathmini za ukaguzi kwa mara kwa mara ili kuhakikisha ubora wa elimu inayotolewa inakuwa sahihi, lakini ya mwisho, wanasema watafanya jitihada maalum zitakazowavutia wanafunzi kwa hamu kuendelea masomo ili kupunguza idadi ya watu wanaokimbia skuli wanafunzi, kazungumza hali ngumu ya walimu, lakini nataka niirudie tena Mhe. Mwenyekiti, niisome ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika ukurasa 158 (99), "Elimu ni moja ya haki ya msingi kwa kila mwananchi mwenye uwezo muhimu, maendeleo na kiuchumi na kijamii katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2010/2015, sekta ya elimu imepata mafanikio yafuatayo:

Ameanza kuitaja elimu ya maandalizi, idadi ya skuli ya maandalizi zimeongezeka kutoka 238 mwaka 2010 hadi kufikia 279 mwaka 2015, amezitaja vijiji ikiwemo Potoa, Jong'owe, Konde na kwengineko, lakini ameitaja elimu ya msingi vile vile, hiyo elimu ya maandalizi niliyoitaja. Elimu ya msingi ameitaja vile vile na kutoka ongezeko la skuli kutoka 299 hadi kufikia 359, lakini ameitaja skuli za sekondari kupunguza uhaba wa wanafunzi. Hiyo ndio Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa hebu tuzitizame utekelezaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo, inayoongozwa na Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi, hata mimi nimekamata ilani hii kutekeleza kwenye jimbo langu.

Mhe. Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein amezitekeleza Ilani zote mbili kwa pamoja, hakuna sababu ya watu wa CUF, wanachama wa CUF kubaki CUF hakuna sababu, kwa sababu Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi tayari imekidhi vigezo vyote, hakuna sababu. Tuwaombe sana, tuwaombe sana kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi sasa hivi inatekelezeka sana kwa ubora wake. Kwa hivyo tuwaombe si aibu kuja kwetu waje warudi nyumbani sote tulikuwa Chama kimoja. Tuendelee kuiunga nchi yetu mkono, lakini tuendelee kujenga uchumi imara kujenga uchumi wa kati, uchumi wa viwanda lakini kufikia katika hatua ya Dubai ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niondoke hapo, nimesema leo nataka nichangie kwa imara wangu, hiyo hali ya siasa ndio nimeanza kuizungumza, lakini suala la mafuta na gesi mdogo wangu Mhe. Hamza amelieleza lakini mimi nataka niliguse vizuri. Niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo tunaifanya na inshaallah mwaka 2019 tuone matunda makubwa yamepatikana katika nchi yetu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini nina wasi wasi, nawasi wasi ndio akili, hebu serikali atakapokuja Mhe. Waziri anambie kuna mkataba wowote kati ya watafiti au kampuni inatafiti na serikali, atwambie kuna mkataba wowote uliotiwa au tunafanya mambo tu. Ninataka kujua hapo lakini niwapongeze kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa 5 kwenye namba 18.0 "Uimarishaji wa Miundo Mbinu ya TEHAMA". Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na wasi wasi mkubwa sana na siku zote niliwahi kumuuliza mwalimu wangu, walimu Haroun hii kwao wapi, akanielekeza kwao pahala Fulani, hii *government* nina wasi wasi nayo mkubwa sana. Ninataka kujua pamoja na mafanikio ambayo amesema amefikia, mimi nataka kujua ni taasisi ngapi za serikali zimeunganishwa lakini tulipokwenda walisema bado kulipa, kwa hivyo sasa wanalipa ni taasisi ngapi. Kwa sababu nikawa na wasi wasi huo hata humu ndani tumeunga na mkonga wa taifa, lakini hata *interment* hupati, ukizimwa umeme Chuo cha Karume basi Baraza la Wawakilishi halina lolote. Mimi nilikuwa nina wasi wasi huo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze tumefikia hatua gani na wapi wameanza kulipa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 6 kwenye kifungu kidogo cha 19.0 kuimarisha Uwanja wa Ndege Pemba. Niipongeze sana serikali kwa hatua hizi zilizofikia, ili kujenga uchumi mkubwa Pemba lazima tuweze kukifanyia ukarabati wa kutosha na ndege kubwa kuweza kutua Pemba. Pemba bado tunakuhitaji na bado kupo kuzuri kiutalii.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya hapo nilikuwa nataka kuuliza pamoja na kuwa tunatengeneza uwanja, wadau wa pale tunawashirikisha. Tuseme kama *GAPCO* wao ndio wanaotoa mafuta ya ndege pale, tunawashirikisha katika hili, ili kuona mafuta yetu tunauziwa vizuri, kuna *parking* nzuri ya gari zile, lakini vile vile na *fire brigedy* tunaishirikisha vizuri, nilikuwa nina wasi wasi huo, Mhe. Waziri nadhani ameshanisikia na atakapokuja hapa atanambia.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda ukurasa wa 7 kifungu cha 22.0 Huduma ya Maji Safi na Salama. Nichukue furasa hii kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi sana. Pia nimpongeze Mhe. Rais kwa mageuzi aliyoyafanya mazuri ya kubadilisha viongozi. Mkurugenzi Mkuu aliyeletwa hapa ni Mkurugenzi mzuri na jembe kubwa sana. Niliwahi kupingana na Mwenyekiti, wa Kamati hii Mhe. Hamza Hassan Juma, yeye alisema na nikamnukuu na nikachukua *Hansard* yake kuwa hii mamlaka sasa imefika wakati wapewe majeshi waiendeshe. Leo amekiri Mwenyekiti kuwa sasa wapewe raia kwa sababu tayari wanaendesha vizuri na maji anapata Kwamtipura.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema tangu kuundwa ZAWA sijui kama nakosea mwaka 2006 mpaka leo ina miaka mingapi. Kama tuipa ruzuku sasa ianze kujitegemea, tujue inakwenda kwa miaka mingapi. Vile vile nilikuwa nataka kujua *target* ambayo wamejiwekea ni *target* gani na ya kufikia asilimia ngapi. Hivi sasa maji tunapata asilimia ngapi, lakini *target* yetu tuliyojiwekea tunapata asilimia ngapi mpaka kufika mwaka 2020. Hata hivyo nataka kujua *operation cost*, tunapoziendesha, lakini na *income cost* ambayo wanazikusanya nataka kuzijua hapa ili tuanze kuangalia. Je, wanakwenda sambamba na ruzuku tunayowapa. Nataka kuondoka lakini kabla

sijaondoka hapa siamini vizuri sana kama maji Zanzibar hakuna. Maji Zanzibar yapo na ya kutosheleza.

Niende kwenye ukurasa wa 7 huwo huwo kwenye 23.0 Huduma ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, nianze kuipongeza sana serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tukiangalia utekelezaji wa Wizara ya Afya, asilimia zaidi ya 78 tayari wameshatekeleza Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi. Lakini panapomafanikio hapakosi kasoro, juzi tuligawa afya ya msingi kuileta chini ambayo tulisema tunakwenda kwenye D by D *Decentralization* ingawaje mimi siyo muumini wa jambo hilo niseme kweli. Kwa sababu nikiangalia Wilaya zetu zinafika 11 ukigawa na 1.5 ya *population* yetu hainipi kivutio kuwa tunasema sasa hivi tuna *Decentralization,* sijui tulikuwa tunafuata watu tu, mimi sijui.

Mhe. Mwenyekiti, kitu kinachotokea sasa hivi wafanyakazi hawa wa afya ya jamii wanaopelekwa katika afya ya msingi bado hatujawagatua na hapa panaweza pakatokea na tatizo. Tatizo moja linaweza likatokea tunaweza tukapata wafanyakazi hewa. Tuombe Wizara ya Utumishi kuwabainisha wale ambao wanagatuliwa na kuipeleka mishahara yao kule walikogatuliwa, tukiendelea kukaa hapa hatuwezi kuwa na jambo zuri sana na tunaweza tukasababisha *chaos* kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, tuondoke hapo niende kwenye vipaumbele ambavyo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amevieleza ni vingi sana naviona kwa sasa, bado vipo vingi. Lakini hata hivyo vingi vyenyewe 32.0, hata hivyo vipaumbele vingi bado kuna vyengine ameeleza kwa ufupi au sijui vipi, anasema kiambatanisho cha 2, kuimarisha zaidi utalii nchini.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kufahamu, kuimarisha utalii nchini, unaimarisha katika sekta gani, kuna *medical tourism*, lakini kuna utamaduni, au tuendelee kubaki tu na fukwe zetu tu zilizokuwa nzuri. Hapa naomba Mhe. Waziri atakapokuja anambie tunaimarisha katika upande gani. Mhe. Hamza Hassan Juma kasema wapo watu ambao wapo tayari kutuletea watalii wengi.

Lakini ya 4 anasema kuimarisha kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji uvuvi na mifugo, sitaki kuamini vizuri sana. Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein namuonea huruma sana, tangu anaingia madarakani anazungumzia *rice irrigation* tangu hana mvi mpaka kawa na mvi *rice irrigation* haijawa hili jipu. Wakampelekea mbegu mbili sijui kuna nerika, wakamuaminisha, akakubali, wakamuweka kwenye trekta, akavuna, uko wapi, tuambizane ukweli. Sitaki kuamini mambo mengine sitaki kuamini na nasema hili sitaliunga mkono mpaka nipewe majibu ya kutosha.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, uvuvi tuna raslimali kubwa sana ya uvuvi, lakini tuna wawekezaji wengi waweze kufanya viwanda vya uvuvi, lakini uvuvi uweze kuwanufaisha wananchi wetu. Leo tunaweza kusema tunaweka *Fishing Aggregate Devise* ili kuweza kuwavutia samaki. Mwananchi gani anaweza kwenda Bahari Kuu hapa Zanzibar, tumemuwezesha vipi, tumewezesha Shirika letu la Uvuvi tumeliunda. Nina wasi wasi tusije tukarudi kwenye vibanda vya dagaa tena vya Mwembenjugu na Jang'ombe. Wasi wasi wangu lakini Mkurugenzi aliyewekwa pale ni mzuri sijui atakwenda vipi, lakini hatuna vifaa vya kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende kwenye ya 3 niliisahamu Kuimarisha Viwanda Vidogo Vidogo na kuongeza thamani ya bidhaa. Nimeshasema kule hiyo SMIDA yenyewe bajeti iliyopewa labda ya kujenga miundombinu, tutajenga viwanda hivi vipo wapi, soko letu liko wapi, kwanza tufanye utafiti wa kutosha kuliko kutupa pesa hizi za wananchi.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenda kwenye Ofisi ya Uratibu, Mhe. Hamza Hassan Juma, keshaisema sana na mimi nikiisema hii jinsi ya Muungano lakini nikazie padogo tu. Niendelee sana kumshukuru Mbunge wangu Mhe. Turky juzi aliuliza vizuri sana. Pia nimshukuru sana na nimpongeze dada yangu Sada Mkuya Salum na yeye alizungumza jambo zuri sana la Muungano na aliwambia jambo zuri. Vile vile tusisahamu kumpongeza na kumshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub na yeye alifanya kazi kubwa sana (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano ninakukumbusha.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana. Naomba niende kwenye kiambatanisho kwenye ukurasa wa 60, Uendeshaji wa Shughuli ya Tume ya Uchaguzi naona makisio na programu ndogo hizo hazikuwekewa kitu, nilikuwa naomba ufafanuzi. Nataka kuja kwenye kitabu kikubwa Mhe. Waziri dakika tano tu nitazitumia huko, naomba ukikamate kitabu kikubwa kwenye kifungu cha C01 kama umefika kifungu cha PC0101 kifungu kidogo cha AC 010101, Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana ziliwekewa bilioni moja, milioni ishirini na nne laki mbili na kumi na saba, lakini safari hii zimezidi, nilikuwa nataka kuona kwa nini zilizidi nataka kupata ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo kwenye kifungu kikubwa cha PC0102 kifungu kidogo cha AC01020102 Mradi wa Kuimarisha Uwezo na Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa. Mwaka jana zilitengwa milioni mia saba na tisini na nne, laki tisa hamsini, lakini safari hii hazikutengewa kitu. Nikuwa nataka nipate ufafanuzi. Je, hatukabiliani tena maafa au tumeshayaacha au tumepata mfadhili kwenye pesa za maendeleo wametulipa. Jengine niende kwenye ukurasa huu huu kwenye shughuli za SMZ uratibu kifungu kidogo cha AC01020303 Uratibu wa Shughuli, mwaka jana hazikutengewa fedha lakini mara hii kumetengewa bilioni sita milioni mia nane thamanini na tisa na laki nne. Naomba tu kujua kwa nini mwaka jana hatukutengewa pesa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna kifungu kidogo cha AC010101 mwaka jana tulitengewa milioni mia tano arubaini na mbili, safri hii naona kimepanda sana, kimeongezeka. Lakini hapo hapo chini kuna kuimarisha huduma za watu wenye ulemavu, safari hii sikuona kupangiwa. Lakini vile vile kuwawezesha watu wenye ulemavu sikuweza kuona, sijui hatuwezi tena kuwawezesha au vipi, nataka ufafanuzi, kwenye fedha za maendeleo Mhe. Mwenyekiti, siji kwa sababu nakuona una nitizama tizama nataka kwenda kwengine.

Kwenye Tume ya Uchaguzi huku kifungu kidogo AC03020101 Ununuzi wa Vifaa Halisi na Kusimamia Huduma za Rasilimali Watu, tulipanga bilioni moja, milioni mia nne sabini na saba laki saba na hamsini, lakini sijaona makisio mengine. Ningeomba ufafanuzi kidogo na naomba nioneshe nia ya kuondoa fungu katika hili kupeleka kwenye walemavu ikiwa sikupata ufafanuzi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye tungu la CO5 Tume ya Ukimwi, huku nataka kujua tu katika kifungu kikubwa AC050105, uratibu wa muitikio wa Utaifa wa Ukimwi, mwaka jana ilipangiwa milioni kumi na moja laki sita ishirini. Lakini mara hii hazikupangiwa mpaka chini huko, nilikuwa nataka kujua tu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kuna hili suala la kupambana na madawa ya kulevya, niwapongeze kwa kazi wanazoweza kuzifanya sana, nimpongeze Mkurugenzi lakini naangalia na mafungu yake nina niya ya kuyapunguza nikaweka kwenye ulemavu, kwa sababu mengi hayapo vizuri. Kwa hivyo natangaza nia mapema kama sikupata maelezo mazuri kuna mafungu nitayachukua na nitayaelekeza pahali gani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti niendelee kukushukuru sana na nikutakie kazi njema.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kwa mchango wako. Sasa naoma nimwite Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza) na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf ajiandae.

Mhe. Mwanaid Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia hotuba ya makadirio ya mapato ya matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo katika Baraza hili naamini sote ni wazima wa afya. Pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuwakilishia hotuba hii kwa ufasaha zaidi na tumeifahamu vizuri sana. Nimpongeze Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamu wa Pili katika kutuangalia hotuba hii na sisi tukaweza kutoa michango yetu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na mchango wangu mimi nitaanza katika Afisi za Muungano katika Taasisi zetu hizi zinazohusiana na muungano pamoja na changamoto walizoziona Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi. Niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudi zao walizochukua katika kuhakikisha mapato yanayokusanywa kupitia huduma za minara na maboya yanakusanywa kama ilivyokusudiwa kwa taasisi za muungano. Nasema hongereni sana na jitahidini ili tuone matatizo haya katika taasisi zetu hizi za Muungano zinafanikiwa.

Nikiendelea hapa nataka nitoe mfano kipindi cha nyuma tulikuwa tuna kilio chetu cha kukosa mapato kupitia minara na maboya kupitia *TPA,* lakini sasa hivi tatizo hili limeondoka na tunashukuru kupitia Afisi hii ya Makamu wa Pili pamoja na Wizara husika kulimaliza tatizo hili, nasema ahsanteni sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nianze na ukurasa wa 37 programu ndogo ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na Waheshimiwa wenzangu waliozungumzia kuhusu masuala haya ya watu wenye ulemavu.

Kusema kweli nikizingatia Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis na Mhe. Zaina Abdalla Salum na Waheshimiwa wengine mara nyingi wanalipigia kelele suala hili kutokana na ushirikishwaji katika mambo yao na katika Idara hii kupitia kwa Makamu wa Pili. Bado Idara hii inakumbana na changamoto ya ukosefu wa miundo mbinu imara kwa watu hawa wenye ulemavu, kuna ukosefu wa viungo bandia pamoja na ukosefu kuwepo sehemu ya kitengo maalum ya kinachoshughulikia suala hili katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Suala hili limepigiwa kelele sana lakini bado Wizara haijalifanyia kazi, tunaomba basi kwa makusudi kwamba suala hili walishughulikie ili kuona usumbufu kwa wananchi wetu unaondokana.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikiendelea kuhusu masuala ya ulemavu nije katika uhaba wa dawa za watu adimu. Hali inayosababisha watu wenye ulemavu na ngozi kupata tabu. Naiomba serikali pamoja na Afisi ya Makamu wa Pili kulipatia ufumbuzi tatizo hili, kwa sababu kutokuwepo na dawa ni kuzorotesha utendaji wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika suala hili hili la ulemavu kuhusu Wizara ya Elimu, bado katika Idara hii kuhusu wanafunzi wetu waliokuwa walemavu, vitendea kazi katika maskuli bado ni tatizo na ni changamoto. Basi tunaomba mara nyingi Waheshimiwa Wawakilishi wanapiga kelele bado kuna tatizo la vitendea kazi vya wanafunzi wetu wenye ulemavu kukosa kujisomea, ndio mara nyingi tunakuta wanafunzi hawa hata ufaulu wao unakuwa mdogo kutokana na vitendea kazi vya kusomea hawana. Vitendea ambavyo walivyokuwa katika maskuli vipo ni kidogo au kilichokuwepo kimoja kimoja hicho kwa wanafunzi waliokuwepo darasa zima wasomee, ina maana hapa kuna tatizo la kutokuwa na wanafunzi hawa kufaulu vizuri katika mafunzo yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika ukurasa wa 43, Programu ya Kutunga Sheria kupitia Bajeti ya kusimamia taasisi za Serikali. Naomba Ofisi ya Makamu wa Pili kwa kushirikiana na Baraza la Wawakilishi kuyatafutia ufumbuzi wa haraka maeneo yetu ya serikali. Mimi nitakuja katika eneo hili la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita nilichangia kuhusu jengo letu hili la Baraza la Wawakilishi, bado jengo letu hili linavuja, tumeshapiga kelele sana itakuwa sio vizuri, mimi nasimama tena kwa mara ya pili au mara ya tatu nasema jengo hili jamani linavuja, limejengwa kwa pesa nyingi sana za wananchi lakini leo jengo hili ukipita nje unaliona zuri lakini ndani linavuja. Tumeshapiga kelele kama Afisi ya Makamu wa Pili basi walione hili pamoja na majengo mazuri tunayoyataka lakini na jengo letu hili pamoja na uzuri wake bado linavuja, tunaomba tena serikali iliangalie jengo hili au mpaka lianguke ndio tutajua kama linavuja.(*Makofi*)…..

Mhe. Mwenyekiti, vipi kuhusu jengo hili au mpaka lianguke ndio tutajua kama linavuja kwa sababu pakivuja padogo panaendelea *(Makofi)*

Kwa hivyo basi Mhe. Mwenyekiti**,** naiomba Ofisi hii ya Makamu wa pili basi itizame kwa jicho la huruma ambao humu sisi tunakuja kufanya kazi kutunga sheria za nchi, basi tukija katika vikao kwenye Kamati tukianza kwenye kamati viti tunapanga tunarowa na sisi tunakuja humu tunasema tumekuja kutunga sheria basi waliangalie tena, hayo tunayoyazungumza naomba basi serikali ilitizame tena hili jengo, liangaliwe kwa huzuni tusiseme tena bajeti nyengine inayokuja

tusilizungumze tena tulifanyie kazi au tukisha kuzungumza yakesha kuandikwa tukisha kujibiwa ndio kazi yake imemaliza humu (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 44 Tume ya Uchaguzi, vile vile kupitia utekelezaji wa program ya uendeshaji wa shuhuli za serikali na Ofisi ya Makamu wa Pili katika nafasi zilizo wazi zinazohitaji kuajiri wengi kuzingatia vigezo vya elimu pamoja na kuzingatia sehemu hii muhimu nyeti kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, pia naiomba serikali basi katika ajira hii kupitia Tume hii ya Uchaguzi naomba basi katika nafasi hizi za uajiri, wafanye kwa makusudi kuona vigezo vinazingatiwa, kwa sababu kama tulivyosema kwamba sehemu hii ni muhimu na nyeti kwa taifa letu basi naomba vigezo kama mlivyosema vizingatiwe, tusifanye masihara katika eneo hili, eneo hili ni uti wa taifa ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika masuala ya Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Kupitia Tume hii naiomba serikali kwa kushirikiana na wizara husika kuandaa mpango mikakati kuzirasimisha bandari zote bubu kwani kutokufanya hivyo ni kuongeza uingizaji wa madawa ya kulevya visiwani kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi wamelizungumza hili lakini na mimi nikaona si vyema kama sijaligusia, kusema kweli mimi nikuombeni serikali kwa hatua ambazo imechukua katika kusimamia maeneo kama bandarini na uwanja wa ndege tayari kumekaa vizuri lakini bado kuna tatizo la bandari bubu.

Mhe. Mwenyekiti, bandari bubu bado kunapitishwa dawa tukizingatia tunakilio hichi cha watoto wetu kuingia katika masuala haya ya madawa ya kulevya lakini bado kama serikali inatakiwa ijitahidi, bandari bubu bado zinapitisha madawa ya kulevya. Vijana wetu wengi tutawakosa kutokana na tatizo hili, Waheshimiwa wengi wameleta kilio chao, kila bajeti inayokuja tunapiga kelele tunaishukuru serikali kwamba inajitahidi lakini bado tunaiomba serikali izidishe jitihada, bado dawa za kulevya zinapita katika bandari hizi bubu. Kwa hivyo naomba serikali ijitahidi na hizi bandari kupitia katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais, naamini wananisikia nataka utekelezaji ufanyike isiwe inaandikwa katika vitabu vyetu halafu kazi imekwisha, tunaomba ifanyiwe kazi tuone utekelezaji unafanyika. (*Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nije katika ukurasa wa 48, kuhusu Tume ya Ukimwi. Kupitia program ya uratibu wa muitiko wa Taifa na ukimwi naipongeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuona umuhimu wa *ZAPHA PLUS*. Kwa mwaka huu wa fedha 2018 – 2019 kuwaingizia pesa za ruzuku jambo ambalo litawasaidia sana wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hongera sana nawaomba tu *ZAPHA PLUS* waengeze jitihada ruzuku ndio wameingiziwa wafanye kazi kwa uhakika. Mimi sitaki niseme sana kwa vile wenzangu wengi washachangia basi mwisho kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini/Magharibi naunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza) atafuatiwa na Mhe. Mtumwa Yussuf Pea na kama muda utaturuhusu basi Mhe. Mwinyihaji Makame ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti**,** ahsante kwa kunipa nafasi ya kuichangia hutuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema lakini la pili niwashukuru viongozi wote wa ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuleta hotuba nzuri na mimi nimeipitia kwa kina sana na yapo maeneo kama sikupata majibu mazuri maana mengi yameenda vizuri, lakini yapo maeneo maana yake tukitizama mlinganisho wa bajeti iliyopita na maombi ya bajeti hii kidogo tunapata mashaka. Kwa hivyo eneo la mwanzo naomba kuli-de*clare* kama sikupata majibu mazuri nitazuia fungu katika programu mbili za Tume ya Uchaguzi, zote mbili ya uendeshaji na wanashughuli za uchaguzi nitachangia na ninachokitaka nitasema.

Lakini la pili kwenye Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali CO 102 ya kukabiliana na maafa shughuli ndogo, lakini shughuli nyengine ya uratibu wa *SMT* na masuala ya Muungano, lakini shughuli ya mwisho katika eneo hili ni usimamizi wa masuala ya mazingira, naomba kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza kwenye ukurasa wa 3, nipongeze hutuba kwanza hii kwa ujumla wake lakini kuna eneo wametoa pongezi ukurasa wa 3 namba 11, walitoa pongezi *TRA, ZRB* na taasisi nyengine zinazokusanya mapato kwa uwezo wao mkubwa walio uonyesha na kupandisha mapato ya serikali. Lakini *statement* ikaendelea kwa wapo ambao hawaitakii mema serikali kwa maana sio waaminifu na wanapoteza sehemu ya mapato ya serikali. Lakini serikali yenyewe katika hotuba hii ikaendelea kusema tutawachukulia hatua. Wapo walokumbwa na kadhia hii tumewazungumza hata hapa Barazani muda mrefu na kuna utekelezaji kila tukiufatilia na utaratibu wa serikali unavyochukua hatua kunako eneo hili, bado haujaenda vizuri maana wakati mwengine wanahojiwa zaidi hawa wadogo wadogo wale hasa wenye dhamana ya maeneo ya upotevu wa fedha kwa baadhi ya matukio yanavyotokea hawajahusushwa na hata kuhojiwa na kuchukuliwa maelezo kunako eneo hili. Kwa hiyo sisi tunaiomba serikali, dhamira yake njema ya kuwachukulia hatua hawa wote basi na wale ambao wao ndio ma-*incharge* kunako maeneo wahusishwe na matukio haya pale ambapo yanatokea, na wakiwa hawahusishwi basi tunakoelekea sio kwahala kuzuri. *(Makofi)*

Eneo jengine la uimarishaji wa miundo mbinu namba 18 ukurasa wa 5, umezungumziwa mkonga wa taifa. Katika suala hili la uwepo wa mkonga wa taifa upo zamani, lakini tunapopitia utekelezaji wa bajeti na mapato yanayotokana humu sizungumzii taasisi za serikali, nazungumzia zile taasisi ambazo tuna mikataba nazo na wanachangia ambapo ni sehemu ya mapato ya serikali.

Mwaka 2014 – 2015 ukipitia bajeti kuna ziro na taasisi zilikuwepo na tuliingia mikataba nazo, maana kama tunawadai mapato haya yaje 2016 -2017, 2017 – 2018. Nataka kujua kunako eneo hili utekelezaji mzuri wa serikali kwenye wale wadau au wahusika ambao tumeingia mkataba nao, maana yake wanastahiki kutulipa kuchangia pato la serikali. Lakini nende kifungu namba 19 katika hutuba kinaelezea upembuzi yakinifu katika uwanja wa ndege wa Pemba.

Kwanza niishukuru serikali katika hatua hii lakini mwisho katika maelezo ukiyasoma wanasema tunapata, tutakuwa tunapokea ndege aina ya *boeing 737*. Sasa inawezekana *boeing 737* tunayoipokea kama hatukutaja ule ukubwa wa ule uwanja ile dhamira hasa itapotea, maana kuna watu hawawezi kujua tunaweza kujua kama sisi tu tulopata bahati ya kusafirishwa na serikali na wengine ambao wamesafiri. Sasa eneo zima hili likitaja ule mpango mzima wa serikali basi ujue na ile dhamira na ule ukubwa ambao tunautegemea wa uwanja ambao tunaujenga ungetajwa na ingekuwa jambo zuri zaidi, hapa nashauri tu.(*Makofi*)

Lakini niende ukurasa wa 10 kipengele cha 32 cha hutuba, kuna maeneo yalopewa kipaumbele lakini nazungumzia mwaka wa fedha 2018 – 2019 ili nipate kuja katika mwaka huu wa fedha. Hapa niipongeze serikali kuna namba 5 inazungumzia kuimarisha kilimo cha kujenge miundo mbinu ya umwagiliaji maji na uvuvi na mifugo.

Katika eneo la umwagiliaji maji kuimarisha miundo mbinu ya umwagiliaji maji, tulioona jitihada za serikali walitafuta fedha kupitia *EXIM Bank* lakini tukakwama kwenye tenda. Sasa hivi tunarudi tena tumeliona tangazo sisi katika kufuatilia la tenda wametoa wizara ya kilimo, yale yaliyofanyika kipindi kile kwa sababu tumetunga sheria na wasimamizi ni wale wateuliwa wanaokwenda kusimamia wizara, tunaomba kwenye eneo hili kadhia ile ilotufikisha miaka miwili sasa tunasubiri utekelezaji wa programu hii wasije wakaturejesha tena. Sheria tunazo, utaratibu tunao lakini kama fedha za mkopo zimetoka zimetoka katika *EXIM Bank* katika kukabiliana na hili, kwenye *loan agreement* kuna mambo ambayo ni makubaliano yetu baina ya serikali na wao tuyafuate kikamilifu ili tusije tukawachelewesha tena wananchi. Maana kuna Waziri mmoja ndani ya Baraza hili kunako miundo mbinu hii aliahidi kama akipewa na hakufanikisha kupata chakula cha kutosha ndani ya nchi hii yuko tayari kujiuzulu, lakini ndio kahamishwa kapelekwa eneo jengine.(*Makofi)*

Sasa sisi tunataka kuiambia serikali, kunako eneo hili yale mambo ambayo tumeshakubaliana na fedha tayari wenzetu wameshaamua kutupatia hata kama kwa mkopo basi serikali ichukue jitihada katika eneo ambalo wenzetu wa Wizara ya Kilimo kwa ujumla, mimi naamini kuna viongozi wazuri wanaoweza kutufikisha katika utaratibu tunaoutaka. Mimi naomba tu tujitahidi tusirejee katika eneo lile ambalo lilitufikisha mara ile.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nende Baraza la Wawakilishi. Mimi sina tatizo sana ukiacha lile eneo ambalo Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa alilichangia la kuvuja, mimi kule ndio kushamaliza sipiti tena uko napita katika ule utekelezaji, ukisoma yale mambo ambayo wamepangiwa Baraza la Wawakilishi kipindi kilichopita lakini ukija ukisoma utekelezaji wake wamefikia karibu asilimia 98. Mimi naomba kuwapongeza sana, naomba kuwapongeza na kama programu kama hizi za utekelezaji kama ambapo unataka kwenda kulizungumza suala la Tume ya Uchaguzi na maeneo mengine, tungekuwa tunazitilia pesa taasisi na wanafanya kama mambo ambayo tuliyowapangia basi tungekuwa tunaendelea kuwapa hongera sana. Kwa hivyo kwa eneo hili tunaomba kuwapa hongera watendaji wote wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kusimamiwa na Mhe. Spika kwa kutufikisha hapa. (*Makofi)*

Lakini sasa naomba nielekee Tume ya Uchaguzi, ukurasa wa 22 ya hotuba hii katika programu zilizopangwa ukizifuatilia na kitabu hiki cha bajeti, mwenzangu jana alizungumza lakini kuna mambo matatu muhimu, maana yake yamejirejea tena katika maombi ya fedha na mwaka huu.

Sasa ndio maana nikasema tutazuia kunako eneo hili, kuna mambo humu yametaja ununuzi wa magari lakini leo huku huku wametuletea matengenezo ya magari ndio utekelezaji wake.

Lakini kuna mambo mengine yamezungumzwa humu kuwapatia mafunzo ya muda mrefu huku hayakutajwa, lakini kuna shuhuli pia za kuimarisha michoro ya majengo na Ofisi za Tume za Uchaguzi, katika utekelezaji humu hayakutajwa ni mambo mazito sana na uzito wake niliwahi kuchangia mimi humu, lakini leo natoa ufafanuzi tena. Nikianza kwetu Mkoa wa Kaskazini, ukenda Wilaya ya Kaskazini "A" ile Ofisi ya Tume ipo kwenye ghorofa na leo tunazungumza kila siku kwa miundo mbinu bora iwashirikisha na wenzetu watu wenye ulemavu, tumeipigia kelele muda ule na leo bado ofisi iyo ipo pale lakini hatujaona ule mkakati wa serikali wa kuondoa ofisi ile kuiweka katika eneo jengine.

Lakini ukirudi Wilaya ya Kaskazini "B", ofisi sisi sote tunakuwa tunakwenda kwa uharaka Wilaya ya Kaskazini "B" ukiingia wakizidi watu watatu, maana yake afisa mmoja, karani mmoja akizidi mwengine watatu anayepata huduma, hakuna mwengine anayeweza kuingia. Sasa leo tumeombwa pesa mara ile ambazo zinazungumzia masuala ya michoro na majengo lakini watu wanabaki kwenye ofisi hizo na hii ni ofisi kubwa, ina dhamana kubwa, lakini hatujaiona katika kuiboresha ili utekelezaji wake uwe mzuri. Lakini serikali imetoa sasa Wilaya ya Magharibi "A" na Magharibi "B", Ofisi za Tume zipo wapi, maana unatoka Magharibi, watu wanafuata ofisi mjini, haiwezekani kabisa kama watu wana haki za msingi kupata hudumu katika maeneo yao, kwa nini uwatoe huku uwapeleke kule.(*Makofi*)

Sasa leo hili ndio mana nikasema kama hatukupata majibu mazuri ya utekelezaji wa hili mimi hapa nazuia fungu, kabisa hatuwezi kuwashuhulisha watu ambao tumewataja kwenye Ktiba na wanatakiwa kupata haki zao za msingi. Nilianza na watu wenye ulemavu kwa jengo la Wilaya ya Kaskazini "A" tujue haki yao wataipatia wapi katika utaratibu ule au tuwapelekee *lift* tuiunde kwa ajili ya kupata huduma zinazostahiki, vyenginevyo tusiendelee kuwanyanyasa kwenye serikali ambayo mimi naamini haina dhamira hiyo. Kwa hivyo huku tupate majibu mazuri lakini na wananchi wa Wilaya ya Magharibi "A" na Magharibi "B", kwa nini tunawaleta mjini na kwa nini wa mjini hatujawapeleka Magharibi "A" au tukawapeleka Makunduchi, kama kuna Ofisi zote za Tume ili wende wakapate huduma zao bora.(*Makofi*)

Lakini vile vile eneo la Tume mimi nilitaka kujua sehemu kubwa hii ya wafanyakazi upatikanaji wake ukoje, maana ile dhima na yale mambo ambayo baada yanayotokezea unajiuliza hivi hawa wanapatikana kama wanavyopatikana wafanyakazi wengine, maana wengine tunaambiwa hasa huyu leo kaitwa *GSO* huyu kaitwa wapi lakini tunapeleka wafanyakazi wa Tume ikisha tunakamata. Ndio mana nikasema lazima Waziri ukija utupe majibu mazuri tunataka Tume tukaisimamisha ambayo itakuwa na uwezo wa kusimamia haki za msingi na maadili ya Tume kama dhamira ya Tume kuanzishwa kwake.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nende kunako programu ndogo ya ukuras wa 31 (50) ni Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali. Nilisema hapa kuna eneo la mwanzo kukabiliana na maafa. Serikali iliandaa Tume hapa, sijui kamati lakini iliandaa kwa ajili ya wataalamu, kwa ajili ya kuratibu eneo hili ili kupata muongozo mzuri wa mafanikio katika utekelezaji wa mambo ambayo yanatokea na kutukabili. Ripoti yake, maana yake ya utekelezaji tunataka kujua wamefikia wapi na kipi kilitendeka kunako eneo hili tupate majibu mazuri. Lakini shughuli za

SMZ, SMT katika utafiti wa masuala ya Muungano, wenzangu wamezungumza kero na mimi nazizungumza kero.

Mhe. Mwenyekiti, wafanya biashara wetu wapande mbili hizi wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu na tunawaona hasa viongozi wetu wanakaa kwa kushughulikia hizi kero za Muungano, lakini ule utekelezaji baada ya kukaa kwao haupatikani wanaendelea kulalamika tu kila leo kwa serikali zao hizi. (*Makofi*)

Viongozi wanaokaa, ni viongozi wa nchi yetu hii ya Tanzania, hawatoki nje wanatoka ndani lakini wananchi tunaowahudumikia wanatoka ndani ya nchi hii, tunashindwaje maana yake, yale ambayo yashatatuka maana lazima hawa wana vilio vyao wajuuilishwe kwa hili na hili tayari. ikitokea tena rudini lakini kila siku tunazaa jambo jipya, leo yamezungumzwa ya watu wanaozungumza ovyo, mimi hao hata si wazungumzii lakini nazungumzia yale ambayo yanayokwendana na maslahi ya wafanya biashara wetu ambayo ndio sehemu kubwa ya kuchangia uchumi wa nchi. Mimi hapa kama sijapata majibu mazuri alau yale yaliotatuka baada ya kukaa kwa viongozi wetu ni lipi na lipi ili wananchi wakapata faida, fungu hili buti langu litakwenda mara tatu na nitapigisha kura lakini majibu nikipata mazuri sina nia mbaya, nataka kuwa nia nzuri kama serikali ilivyo kuwa na nia ya kuwashughulikia wananchi wake watu tu wapate ile taaluma lakini yale mafanikio ya autekelezaji kunako eneo hili.(*Makofi*)

Usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu kunako eneo hili kuna changamoto kubwa wengi wamesama...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nina dakika tano, itakuwa ishirini imeshatimia, haya nitajitahidi maana wenzangu walipata thelathini lakini hizo hizo kumi na tano zinatosha. Kunako eneo la usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu. Hapa kuna changamoto kubwa kwa ujumla wake tunazungumza haraka haraka hatujakaa tukawatendea haki ipasavyo wenzetu wenye ulemavu. Ninayazungumza haya kwa sababu hata ukipitia zile Sera za Elimu tulizonazo ule upatikanaji wa walimu, upatikanaji wa vifaa lakini upatikanaji wa miundombinu bora haupo. Kuna maeneo ya wenzetu hawa tunawachanganya kwenye madarasa Fulani. Mfano ukienda Muungoni pana darasa pale wanafunzi wale ambao wana mahitaji maalum mpaka wakachukuliwe waingizwe humo darasani, maana si utaratibu mzuri kila siku tunalipigia kelele suala kama hili, wenzetu hawa haki yao ya msingi watapata wapi.(*Makofi*)

Halafu kuna mwanafunzi mimi nimepata hasa taarifa yake na nikamuhoji vizuri anaitwa Bakari, yeye kafika *level* ya *form IV,* ana ulemavu wa macho, lakini yule mwalimu ambaye anamsaidia hata zile lugha za alama ni mwalimu wa *primary.* Maana yule mwalimu wa *secondary* hana wakumfikisha pale tunapopataka, lakini leo walimu wote tunaowaajiri na tunaowapeleka sasa kutoa huduma hizi hatujazingatia hawa. Sasa hawa wenzetu tunawaweka kwenye fungu gani. Sisi kauli zetu tunavyosema ni walemavu watarajiwa basi tufike pahala kunako eneo hili na Mhe. Waziri ukitaka huyu mtu tutakupatia alipo, maana lazima tupate haki zao.

Tanzania sitaki kusema eneo gani, kuna skuli ya watu wenye ulemavu walifeli wote, serikali ikaandaa kamati kidogo ya kwenda kushughulikia suala hili. Hivi tujiulize kunako eneo lile wale

wanafunzi wote walikuwa hawana akili au walimu wanaowasomesha maana yake walikosana nao kunako aina fulani ya ufundishaji au ile miundo mbinu ya vifaa wanavyotakiwa watumie ili *message* zile za mafunzo ziwafikie zilikosekana. Sasa leo hii hatujafikia siye Zanzibar kuja kuwakusanya watu katika eneo hilo lakini tunaelekeza huko.

Sasa mimi naomba sana changamoto hizi lakini ziko changamoto za wenzetu wenye ulemavu wa ngozi, wao huduma hii hapa inakosekana mpaka wasafiri kwenda Tanzania Bara, kwa sababu kuna serikali sikivu mimi naomba kunako eneo hili wajitahidi sana.

Noamba Mhe. Mwenyekiti, uniruhusu nizungumze la mwisho mazingira. Suala la mazingira na nilisema eneo hili nitazuia fungu. Tuna maeneo serikali imeruhusu kuchimba mchanga kwa nia safi, maeneo tumeondoka tumeweka mashimo, tumeweka mahoba lakini kuna ada pia inayochangia katika urejeshaji wa ardhi katika maeneo hayo, lakini huduma inaendelea ya uchimbaji wa mchanga lakini zoezi la kurejesha ile ardhi haipo. Sasa tunataka kujua katika utaratibu wote huo tulioufikia, serikali katika eneo hili ina mkakati gani wa dharura ambao bajeti tunapitisha lakini lazima tufike pahala nchi hii ni nchi ya visiwa. Leo tunakoelekea tunachimba ardhi haturejesha ardhi siku moja tutazama sote.

Sasa tunachohofia ni hicho. Sasa tunataka ule mkakati wa dharura ambao programu hii nilisema mimi ninaizuia katika fungu dogo tunakapokuja kukutana katika mafungu mpaka tupate majibu, kunako uchimbaji wa mchanga kuna ada inatoka katika kufidia urejeshaji wa ardhi lakini misaada mbali mbali tunaipata kunako eneo hili sisi tunafuatilia bajeti. Lakini hatua ya urejeshaji ukoje suala langu lipo hapo na namuomba Waziri kunako eneo hili ajitahidi sana tusije tukakosana na kama kakosea majibu tutakwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, mambo niliyokuwa nayo ni mengi nitachangia kwa maandishi dakika zimeisha nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja hii kwa asilimia hamsini na tano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Miraji. Sasa naomba nimwite Mhe. Mtumwa Peya anafuatiwa na Mhe. Mwinyihaji.

Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi kuweza kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, wenzangu wamechangia mengi lakini mimi nina machache ya kuweza kuchangia hotuba hii.

Kwanza nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili ya Rais kwa hotuba yake aliyotuletea hapa iliyogusa sehemu zote. Lakini la pili niwashukuru sana watendaji wake, waratibu wake wa Afisi ya Makamo wa Rais pamoja na Mkurugenzi wake Khalid kwa mashirikiano mazuri wanayotupa kwa ajili ya kufanya kazi zetu hizi kufanikisha mambo yetu katika majimbo. Mimi nakuja katika mfuko huu hii *TASAF*.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Jamhuri ya Muungano kusaidia wananchi wenye mazingira magumu kwenye maeneo yetu. Kwa kweli suala hili walilolifanya la *TASAF* wameweza kutusaidia hasa sisi Wawakilishi kutupunguzia majukumu katika yale maeneo yetu. Kwa sababu baada ya kuanzia kusaidiwa

watu wenye kaya maskini hata lile suala la utoro maskulini limepungua kwa sababu kuna kipengele kile cha ruzuku ambayo wanapewa wale wananchi wa kaya maskini. Kuna ruzuku ile ambayo siyo ya masharti, lakini kwa kweli ruzuku ile ya masharti. Lakini kwa kweli ruzuku ile ya masharti ni haki yao kupewa kwa sababu juu ya kuweka masharti lakini wanapata maendeleo makubwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ukizingatia kwamba wananchi wanaoishi katika mazingira magumu wanapewa ruzuku kwa ajili ya wanafunzi waende skuli, mwanafunzi asipokwenda skuli ruzuku ile unaikosa, masharti yao hayo lakini kwa kweli sharti lile ni zuri sana kwa sababu sasa hivi imepelekea imepelekea mpaka kupunguza wale watoto wa mitaani, imekuwa wanafunzi wengi wanakwenda skuli mzazi mwenyewe anamuhimiza mtoto wale ili asije akaikosa ile ruzuku ambayo anapewa kwa ajili ya mtoto yule.

Lakini pia imepelekea kina mama wangi kuwaendeleza watoto wao kuwaapeleka *clinic* kwa sababu hapo zamani mtoto akishatimia umri wa mwaka mmoja tu mzazi tayari anakatisha maendeleo ya kumpeleka mtoto wale *clinic*. Kwa hivyo anakosa hata kujua maendeleo ya mtoto wake. Lakini kwenye kaya zile baada ya kuwa kuna ruzuku ile ya *clinic* kina mama wamehamasika sana sasa hivi mtoto mpaka anafika miaka mitano bado anaendelea kupelekwa kliniki. Kwa hivyo niwapongeze sana kwa hiki amcho kimebuniwa kwa ajili ya kaya hizi na tunashirikiana nao vizuri kuweza kuendeleza na hili. Lakini pia wandelee kupatiwa mafunzo baada ya kumalizika huu mradi basi waweze kujiendesha wao wenyewe kwa kujiwezesha na miradi yao maalum wenyewe waliojipangia wananchi wale ambao waliomo kwenye kaya maskini kuondoka na kabisa na huu maskini.

Nije kwenye suala jengine la mfuko wa jimbo niseme kwamba wenzetu wale waratibu kutoka ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais niwapongeze sana, kwanza kutufikishia kwa wakati hizi pesa za mfuko wa jimbo, lakini kama tunavyojua sasa hivi mahitaji yamekuwa makubwa sana na mahitaji yameongezeka. Kwa kweli tunapewa ile pesa ya mfuko wa jimbo ukiangalia na hali ya mazingira tuliyo nayo kwa sasa hivi tunaomba sana kama kuna uwezekano ile pesa iongezwe, kwa sababu ile pesa ni kidogo sana ukizingatia na huu wakati ambao tulionao sasa hivi majukumu mengi, matatizo mengi na yote yanakuja kwa Mwakilishi uliopo jimboni. Kwa hivyo tunaomba sana ikiwezekana huu mfuko wa jimbo nao uongezwe.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninakuja kwenye suala la ujenzi wa barabara. Kuna ujenzi wa barabara hii ya Bububu, Mahonda, Mkokotoni, tumefarijika sana kwamba wananchi tayari wemeshalipwa fidia wote wale kwa ajili ya ujenzi huo. Lakini ninachoomba kwa tumeambiwa tayari kuna mkandarasi naambiwa mzuri lakini bila ya usimamizi madhubuti na msimamizi mzuri unakaofanyika yatatokezea yale ambayo yatatokezea. Barabara inaweza kujengwa isifike mwezi tayari barabara imeshaharibika, hii inatokana kwa sababu gani kawaida yetu tukisha wakabidhi wakandarasi kazi sisi wenyewe tuhajiachia, hatupiti, hatukagui, hatuangalii chochote, kwa nini tushamkabidhi mtu kazi afanye. Kwa hivyo yeye kama kapewa kazi afanye anahitaji kufanya kazi nyengine yeye ataharakiza amalize kazi kazi yake aendelee na akafanye kazi nyengine hatma yake madhara na hasara inazwa kwenye serikali yetu hii. Naomba sana kwenye mawizara yetu, kwenye serikali yetu kuna watu wameajiriwa kwa kazi hizi tu hakuna sababu ya kukaa ofisini inapoanza hii mriadi mikubwa. *(Makofi)*

Lazima watoke waende kuangalia na wakakaguwe nini kinafanyika na ambapo wamemuona mkandarasi kafanya kitu sio sahihi ipo hali ya kumuambia bomoa jenga tena, lakini sisi kawaida yetu kukaa tukasubiri mpaka mradi umemaliza, ndio tunakwenda kuukagua, kwa nini ushakabidhiwa ndio unakwenda kuangalia wewe hatma yake miradi inakuwa mibovu siku mbili ishaharibika, siku mbili barabara hazipitiki, kwa kweli hili ni tatizo lazima tubadilike.(*Makofi*).

Lakini pia hawa wakandarasi waangalie wanapojenga hizi barabara, njia za kupitisha maji, barabara ni muhimu lakini pia maakazi ya wananchi ni muhimu na mfano mmoja ilipojengwa barabara ya Bumbwini, nyumba zilizoko pembezoni ya barabara zilikuwa hazingii maji, lakini baada ya kujengwa barabara nyumba zile zinaingia maji mpaka vyumbani. Hii nini, ukandarasi na ubovu wa ujenzi, lazima kuwe na msingi ya maji ya kuweza kupitisha maji ya kuweza kupitisha maji na kuhakikisha yana sehemu maalum yanakwenda yasingie ndani ya majengo ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja suala la hili la maafa au la mazingira. Kila zinapotokezea mvua basi kuna maafa ambayo yanajitokeza na mazingira yetu yanaharibika, lakini ukiangalia watu mazingira watakwenda, watu wa maafa wote wanakwenda utekelezaji wake kwa kweli haunonekani. Ukiangalia ndani ya jimbo langu mvua zilizopita kuna eneo ambalo wanakaa wananchi kijiji kinaitwa Bumbwini Bwaga. Lile eneo liliharibika sana na ilitokea tunasema maghoba makubwa sana, hayajulikani mwanzo wake hajulikani mwisho wake, watu mazingira walikuja, watu wa maafa wamekuja lakini utekelezaji wake umekuwa zero. Sasa na mvua za mwaka huu zilizonyesha tayari yametokezea maafa haya maeneo mengine kule kule.

Kwa hivyo niombe sana serikali Kitengo kinachohusika twende tukaangalie lakini sio kuangalia tu tukisha angalia na utekelezaji wake tuufanye tushirikiane tuhakikishe mambo hayo tunayaondosha, kwa sababu haya maeneo yapo kwenye vijiji vya watu watoto wanacheza wananchi wanapita pale itakuja kutokea baada ya hasara hii itatokea hasara kubwa zaidi hatma yake tutakuja kushindwa hata kutoa majibu. Naomba sana wizara inayohusika, watu mazingira watu wa maafa tuende tukaangalie wa pamoja tuone tunafanyia kazi vipi suala hili.

Halafu nakuja mwisho suala la saratani. Niishukuru sana serikali kwa kuamua kuanzisha hii chanjo ya Saratani ya Shingo ya Kizazi. Kwa kweli sasa hivi wanawake wengi tunathirika na suala hili la saratani. Niseme tu kwamba wananchi tuhamasike sisi viongozi lakini tuhamasishe na wananchi wetu kwenda kufanya chanjo hii ya saratani na pia nitaka kujua ndani ya Wilaya ya Kaskazini B, hii chanjo ya saratani inatolewa katika vituo gani ili wananchi wetu waweze kujua vituo gani ambavyo vinafanyika waweze kwenda kupata huduma hizi.

Lakini mwisho niseme kwamba nawapongeza tena viongozi wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mashirikiano yao na mwisho kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mtumwa Peya Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipatia wasaa huu mdogo kuweza kuchangia machache kuhusu hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kumpongeza na wezangu kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake hii iliyo *cover* niseme karibu mambo mengi sana yanayohusu Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na nimpongeze yeye pamoja na timu yake Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na wengineo kwa kutunga kitabu kama walivyosema kilichojaa falsafa kubwa sana na mwaka jana nakumbuka nilishauri kwa ukubwa wa wizara hii na uzito wa mambo yake, nilimuomba Mhe. Makamo wa Pili aweke vitengo mbali mbali kumsaidia kazi.

Sasa sijui kama vitengo vipo lakini kutokana na *nature* ya hotuba ilivyogawa kugusa *section* mbali mbali za serikali inaonesha wazi kwamba hivyo vitengo vipo au vinamsaidia kwa lile lengo tunalolitaka Mhe. Makamu wa Pili ili aweze kufanya kazi zake za utatibu kama inavyopaswa. Mheshimiwa baada ya pongezi hizo kwa ujumla ya kazi kubwa kuisimamia serikali yetu ikiwa yeye ndiye mtendaji mkuu nambari moja wa serikali yetu. Mheshimiwa naomba moja kwa moja sasa niende kwenye hotuba yake ukurasa wa kumi na mbili (iv) pale alipozunguza kwamba ofisi imeendelea kushughulikia malalamiko, kero na migogoro ya wananchi inayohusu masuala ya ardhi, nyumba, fidia na kesi za maeneo ya wawekezaji.

Mheshimiwa nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili kwa suala hili kweli wananchi wetu wana malalamiko mengi sana na ushahidi tosha hapa kwamba malamiko thelathini na tano yamepokelewa na kuwasilishwa lakini wameweza kuyapatia ufumbuzi malamiko ishirini na mbili, huo ni mwanzo mzuri. Sasa na mimi nataka kushauri Mheshimiwa ofisi yako kwa uzito wake na hayo ukilinganisha na *nature* ya haya mambo yanayokuja matatizo, ningeomba sana na nakushauri kwamba ungeweka utaratibu wa *open day,* yaani zitamkwe hasa siku watu ambapo wanaweza kwenda kuonana na maofisa au Waziri mwenyewe wewe najua una kazi nyingi mheshimiwa tunakuachia ufanye kazi zako lakini timu yako iweze kupokea wananchi kuwasikiliza mashauri yao na kuwapatia ufumbuzi. Ni kweli usiopingika kwamba kuna matatizo mengi madogo madogo ambayo kwa bahati mbaya mengine urasimu tu tulionao, kwa hiyo ndio serikali iwe na *procedure* zake iwe na utaratibu wake.

Lakini kwa ujumla mtu anotaka *efficient* tunaita ni urasimu ambayo inachukua muda mrefu na mengine miaka na miaka mpaka yanapatiwa ufumbuzi. Kwa hiyo mimi ningeshauri sana mheshimiwa hili ungelifanyia utararibu Ofisi yako. Kuna Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wameanza utaratibu huu na wao walikutana kwenye viwanja basi yule muda hautoshi, kwa wale watu walivyojitokeza kueleza matatizo yaliopo kwenye Mikoa yao, ule muda hautoshi. Sasa mimi ningekuomba sana Mheshimiwa hili ulivyokuwa unashughulika na uratibu wa serikali yetu, hili ni jambo jema nakuomba ulifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiit, naomba sasa niende mbio mbio kwenye sekta nyengine. Hapo hapo katika suala zima la uratibu nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Mohammed Aboud kwa mantiki moja ya kujaribu kujibu *issues* mbali mbali zinapozungumzwa au kutajwa serikali yetu au wengine kupotosha ukweli wa mambo. Mheshimiwa kwenye chama tunamuachia Katibu wetu, mwenezi wetu anajibu. Lakini kwenye serikali lazima tuwe na

msemaji wetu ambao kwa kweli watu wanaopotosha mambo, wanatukashifu kwa uwongo na ukweli lazima wajibiwe wasiachiwe waka *prevail,* kwa sababu ukinyamaza kimya, wengi wanao kwa nini wananyamaza hawajibu yana ukweli yale. Sasa haidhuru mengine tunaona ya kipuuzi yasijibiwe lakini mheshimiwa lazima yajibiwe na nimejaribu ku-quo*te* mfano mmoja na naomba mheshimiwa, hebu kijana zichukuwe hizi mpelekee.

Gazeti la Citizen tarehe 26 April, 2018 katika maadhimisho yetu ya miaka 54 ya Muungano kulikuwa na *Articles* mbali mbali kwenye magazeti. Sasa kuna *Articles* moja kwenye gazeti hilo la *Citizen* la tarehe hiyo niliyoitaja *copy* nitakupa hizi hapa tayari mheshimiwa. Kuna *column* moja hapa imeandikwa *thinking allowed*, kaandika *Professor* Zulfikar Premji anasema. *The union is shining example that must recognized and preserved as such*. Humu akatuponda, akatukanyaga kwamba miaka yote hii hakuna maendeleo yaliyofanywa, hakuna walimu, hakuna madaktari *social welfare* zimekufa zote, na anasema alikuja juzi yeye akaranda Mji Mkongwe inaelekea ni mtu wa Mji Mkongwe hakai hapa kaja mara moja kaondoka. Kwa hiyo, anasema tokea alipoacha Mzee Karume majumba ya Michenzani hakuna tena kilichofanywa watu wako kwenye umaskini, nyumba za makuti, njoo uchukue hizi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mambo kama haya ndio nasema lazima ajibiwe tusinyamaze, hii *Article* mpelekee Mheshimiwa. Naomba ni-*quote* pamoja tu kwa Kiingereza samahani sana na Mhe. Mwenyekiti, mpelekee. Anasema, *sub-sequence leaders including* Mzee Karume *son*, Amani Karume 8 Novemba, 2000 utawala wake mpaka 03 Novemba, 2010 signals ya mtu wa ku-*ignore the poor Zanzibar Population in source or economic development terms*. Yaani kwenye maendeleo ya kijamii na kiuchumi hatukufanya chochote tokea Mzee Karume kufariki, anavyoipotosha jamii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa haya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais si yakunyamaziwa huyu katoa mpaka nambari yake ya *e-mail*. Mimi nilikuwa nishaanza ku-*draft* majawabu lakini nikasema aah! mbali ya mimi kama mtu lakini serikali tumjibu na tumualike hasa, aje aone maendeleo ya Zanzibar yaliyopatikana. Mbali ya vitabu vinavyotolewa na Ikulu ambapo Ofisi ya Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wanatoa na wanajitahidi kuvisambaza, lakini wengine hawapati wanatumia magazeti haya ambayo kwa kweli hawatupendi kutuchafua. Kwa hivyo ningeomba sana Mheshimiwa ofisi yako kiwekwe kitengo maalum Mhe. Waziri anajitahidi lakini si muda wote anayaona. Sasa ukisoma magazeti unayakuta mengi kama haya lazima na sisi tujibu mapigo tusinyamaze.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza vizuri sana yanayozungumzwa Bungeni, huo ni mfano mmoja. Yanayozungumzwa Bungeni lazima na sisi tujibu na tueleze ufasaha mambo yalivyo. Wengine wanayajua lakini wanafanya kwa makusudi kupotosha ule ukweli wa mambo. Sasa hili nilikuwa naiomba ofisi yako Mheshimiwa, magazeti yetu ya chama Uhuru, *Daily News* hayana matatizo na Habari Leo lile. Lakini kuna magazeti mengine wao kazi yao ni kuponda tu basi ule ukweli wote wanaufunika hawasemi ukweli. Sasa tusinyamaze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ningeomba sana hili na sisi ni kama *propaganda* na sisi tutembee kifua mbele, sisi tunajua yaliyofanyika lakini tuwaelimishe jamii waone na wao kimefanywa nini. Kwa hiyo, kama Mratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nahisi hili ni jukumu la ofisi yako mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa haraka haraka niende kwenye Tume ya UKIMWI. Nipongeze kwa juhudi ambazo serikali yetu inafanya kwa kushirikiana na wafadhili mbali mbali katika suala zima la kupiga vita suala la UKIMWI. Nimeona humu kwenye kitabu Mhe. Makamu wa Pili anasema zimetengwa kwenye *recurrent* kama milioni 238 kuratibu muitiko wa taifa wa UKIMWI. Sasa nilikuwa najiuliza huu muitiko umekusudiwa nini hasa, hebu atueleze zile *activities* zake huu muitiko na vipi maana yake zinatofautiana na upande wa Wizara ya Afya zile *activities* zao, wanaoana vipi, isiwe kila mmoja anakwenda njia yake lakini lengo letu kupiga vita UKIMWI. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru pia kuna pesa za utawala na uendeshaji zipatazo kama milioni 665. Hapo nilikuwa nataka ufafanuzi tu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la mazingira. Suala la mazingira nipongeze sana juhudi ambayo serikali yetu inafanya kwenye suala zima la kudhibiti mazingira yetu. Mazingira ndio kila kitu lakini husema hasa ardhi maradhi yote haya vyanzo vyake ni mazingira mabaya, mazingira machafu ndio hayo maradhi tunayoambiwa yanatokea huko kwenye eneo la Muungano. Lakini mimi naomba nijikite kwenye programu ndogo usimamizi wa mazingira ambao lengo kuu limeandikwa kufikia usimamizi endelevu wa mazingira, SC010206. Hapa kwa mwaka wa fedha uliopita idadi ya maeneo yaliyoharibiwa kimazingira yaliyofuatiliwa na kutambuliwa ni 60, na kwa mwaka ujao wa fedha 2018-2019 ambao Mhe. Waziri anaomba pesa zake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ni 84. Sasa nimeangalia hizi kazi hapa viashiria vya matokeo idadi ya tathmini, idadi ya ziara, idadi ya *operation*.

Mhe. Mwenyekiti, nikajaribu sasa kuangalia tena kwenye kazi ambazo ofisi hii itafanya kwa mwaka ujao wa fedha. Kazi hizo ziko kwenye ukurasa wa 88 kitabu cha bajeti, zipo *paragraph* ya 65 kuna *items* kama 7 hivi kutayarisha kanuni 6, kufanya mikutano 32, kuongeza uelewa wa jamii na kadhalika. Sasa nilikuwa najiuliza Mheshimiwa hiyo ni moja kutoa elimu, lakini cha kusema ambacho kiko wazi kwamba kweli watu wetu wengi sana suala la mazingira wamelifahamu, kwa sababu wameona umuhimu wa ardhi wanataka kulima, wanataka kujenga, kuepuka mafuriko. Swali tujiulize tunafanya juhudi gani ku-*recline* zile ardhi zilizoharibika kimazingira, tuta- *rehabilitate* vipi ardhi hizo, rutba tutairejesha vipi.

Haya ndio masuala ya msingi Mheshimiwa nahisi tufanye. Kule Pemba kulikuwa na miradi ya kuweka tuta pale kuzuia maji ya chumvi yasije kwenye mabonde ya mpunga. Masuala kama hayo, vipi tutaweza kurudisha ardhi iliyoharibika, hapo ndio kitita cha pesa Mhe. Makamu wa Pili zitumike huko. *Advocacy* naona hapa imeshafanywa kubwa sana na inaendelea kufanywa, nimejaribu kujumlisha hapa pesa zilizopo kwa miradi ya maendeleo pamoja na kwenye *recurrent* na maendeleo si chini ya 1,336 pesa nyingi tu zimetengwa kwa kazi hizo. Sasa mimi nahisi Mheshimiwa kazi kubwa ije kwenye kuhuwisha yale maeneo yaliyoharibiwa, watu wajikite huko, sio kwenye semina, mikutano, ziara, tathmini, laa! Laa. Hiyo ni sehemu tena iwe ndogo kabisa lakini pesa nyingi iende huko.

Mhe. Mwenyekiti, cha kufurahisha zaidi kwamba mradi huu kuna pesa zote, pesa za maendeleo na pesa za kazi za kawaida, *recurrent* pamoja na *development* ambayo kama nilivyosema ukijumlisha hizo pesa ni nyingi tu zaidi ya 1,336,700 ambapo programu ndogo uratibu wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi yamepangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 1,690 ambapo shilingi 353 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 1,336 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nazidi kushauri kwamba pesa hizo zitumike zaidi kwenye kazi ya ku-*recline*, kazi ya kurutubisha ardhi kupanda miti. Mfano kuna miradi wa *Agro-forestry* watu wanalima na kupanda miti ya kurutubisha ardhi, vitu kama hivyo ndio inapaswa tuvisikie hapa. Lakini ukisema semina, vipindi vya redio, *operation* za kusimamia maliasili, kufanya ziara na pesa zote haya, kidogo Mheshimiwa tunahisi lazima tubadilishe *gear*, tubadilishe *gear* tuone kwamba na *practices* zimeshafanyika kwa mafanikio makubwa kabisa. Kuna ardhi ambazo zimefanyiwa mambo haya tayari zinatumika kwa kilimo na watu wanavuna ndizi wewe mwenyewe utashangaa.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana kwenye *sub-program AC010207* Uratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, tumeambiwa kwamba idadi ya Kanuni ya juu ya Sheria mpya ya Mazingira ya 2015 zitakazoandaliwa ni nne. Kanuni nne hizo tuliahidiwa kwamba zitatengenezwa. Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, tujuilishwe na tupatiwe nakla ikiyumkinika hizo Kanuni nne ambazo zimeshatayarishwa ili tuzijue na sisi zitusaidie kwenye majimbo yetu kuzifanyia kazi. Lakini kwa mwaka ujao wa fedha akasema watatayarisha wanatarajia kufanya kanuni nyengine zipatazo tatu. Ni jambo jema, jambo zuri na naamini litatusaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hotuba yangu kwa kumuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na timu yake na hasa nikisema timu yake, kwa sababu yeye ndio *general* wetu, timu yake iwe inakwenda *field,* yeye ndiye mwenye uratibu wa serikali kuona mambo yako vipi, pameharibika wapi, tutengeneze nini, tena iwe *prompt action* yaani kwa haraka. Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani Mhe. Makamu wa Pili barabara zote za mjini mbovu zinahitaji viraka, huu ndio sura ya mji. Leo pita Darajani Mhe. Waziri wa Nchi yeye ana gari kubwa lile kidogo hayaoni, pita Darajani sasa hivi upige *round main street* utizame. Kwa hivyo, tunasema aah! barabara hazizibiki wakati wa mvua, lakini kuna aina ya jasi alau ukiziba pale lakini leo, maama yake kuna mahandaki kati kati ya mji.

Pili watu imekuwa jambo la kawaida Mjini sasa wanapita *no entry*, mtu Mlandege njia ya Kwahajitumbo nishawahi kuliulizia hilo, hawana habari kabisa, wewe unakuja na gari na yeye anakuja na gari sasa *okay* sijui mwenye sheria nani. Yaani kuna *complete lawless.* Sasa Mheshimiwa ofisi yako ndio yenye uratibu wa serikali yetu, tukizungumza utawala bora haidhuru yuko mwenye utawala bora lakini mambo yetu yasimamiwe, yaongozwe ili yaende vizuri na jukumu hili ndiko kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ndio Ofisi ya Waziri Mkuu hii, sisi hatuna Waziri Mkuu tuna Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Sasa haya naomba sana maofisa, lazima ile *law and enforcement* iwepo, itakuwa serikali watu wanajenga ovyo tu haiwezekani, lazima taratibu na sheria zifuatwe na kufuata kwakwe lazima kanuni sisi wenyewe tuwe wakali, na kuwa wakali lazima usimamizi uwepo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeona nimalizie hili kuiomba sana ofisi yetu hii watu wanajitahidi na wewe mwenyewe unajitahidi Mhe. Makamu wa Pili lakini kazi hii ni kubwa, wizara hii kubwa usimamizi wa serikali mkubwa. Tunakuona juzi ulikuwa Bwawani pale tuna *hall* letu lile, umemwambia yule bwana Manji pale tunataka lijengwe hili ndani ya miezi mitatu, nasikia mpaka leo hajafanya kitu.

Umekwenda mwengine una *intervene*, hivyo ndio inavyotaka mwenyewe uende, lakini wewe mwenyewe utakwenda sehemu ngapi lazima timu yako ikusaidie mugawane kazi. Lakini

mwenyewe uripoti kwako na tunachoomba kwamba hatua zichukuliwe kurekebishe mambo, mambo madogo madogo kidogo yana *challenge good image* ya serikali yetu na haya hayawezi kukubalika ni wachache sana wengi wanafanya vizuri, wengi wanaiweka picha nzuri lakini kuna wachache hawataki kufuata usiwaachie, utawala bora ni kusimamia sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha kikao hiki ningependa tuwatambue wachangiaji wetu wa jioni ambao wakiwemo mawaziri wawili lakini na mjumbe mmoja Mhe. Hussein Ibrahim Makungu atakuwa mchangiaji wetu wa mwanzo na baadae kabla ya kufanya majumuisho Mhe. Waziri tutampa nafasi Mhe. Said Soud Said pamoja na Mhe. Amina Salum Ali, Waziri wa Biashara na Viwanda hao ndio watakuwa wachangiaji wetu wa jioni kabla ya majumuisho ya Mhe. Waziri husika.

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nakushukuruni kwa utulivu wenu lakini pia kwa michango yenu mbali mbali. Sasa naomba niakhirishe kikao hiki mpaka saa 11:00 jioni nawashukuru sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kufika jioni hii katika Baraza lako tukufu katika hali ya uzima na afya njema.

Mhe. Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa ya kuchangia hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais katika Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, naona kama hatukusikii vizuri.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe kwanza kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini pia nimpe pongezi sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri aliyoifanya na juhudi zake kubwa katika wizara hii kubwa na pia Naibu Waziri nimpongeze kwa kazi yake aliyoifanya. *(Makofi)*

Pia niwapongeze sana wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, nimpongeze sana mwenyekiti na wajumbe wake wote kwa kazi yao nzuri wanayoifanya.

Mhe. Naibu Spika, nianze katika ukurasa wa 4 wa kitabu hiki cha bajeti kifungu namba 13, Hali ya Kisiasa Zanzibar. Kwanza nataka kuipongeza sana serikali kwa juhudi zake kubwa ilizoweza kufanya, mbali ya changamoto mbali mbali za maendeleo na kazi za kijamii pamoja na kazi za

jumla za nchi yetu, lakini niipongeze serikali kwa kazi yao kubwa waliyoifanya kwa kuondosha changamoto nyingi sana.

Matatizo mengi ya maji safi na salama, barabara na afya wamejitahidi sana na nimpongeze sana Rais wetu wa Zanzibar kwa juhudi yake kubwa sana kwa kuangalia siku baada ya siku changamoto hizi zinaondoka na serikali yetu kwa ujumla bila ya kujali itikadi za kisiasa na mambo mengine. Kwa hivyo, niipongeze serikali yetu na waongeze juhudi na msimamo hasa kwa hali ya kisiasa Zanzibar iondoke na watu wote wakubali Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi kubwa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 31. Katka kitabu hiki cha bajeti kwenye *bullet* ya 50 nije kwenye shughuli za SMZ na SMT, Utafiti wa Masuala ya Muungano.

Kwanza mimi nataka nipongeze sana viongozi wetu wote wa pande zote mbili kwa juhudi zao kubwa, hata ukiangalia kitabu hiki cha bajeti katika ukurasa wa nyuma huku utakuta imewekwa picha ya Waziri wa Muungano na Mazingira, Ndugu Januari Makamba; kuna Waziri Mkuu, kuna Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna Makamu wa Pili wa Rais wetu na pia kuna waziri wetu wa wizara hii. Napongeza sana kwa picha hii na nishukuru kuwa wanakaa vikao kwa pamoja kutatua zile changamoto za Muungano, kwa sababu kama nilivyosema mwanzo kwamba nchi yetu inafanya kazi kubwa na juhudi zake kubwa sana tunaziona.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kitu kimoja kwamba muungano wetu muhimu sana kwa pande zetu mbili Zanzibar na upande wa Tanzania Bara, ukitizama muungano huu Mhe. Naibu Spika, umeanzia mbali sana kwa kihistoria. Huu Muungano ni wa kupigiwa mfano katika nchi yetu katika taifa letu lote, ukitizama dunia nzima huu muungano ni wa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia tangu Baraza lililopita, Baraza hili lipo hapa leo kihistoria. Kwa kweli kama tunavyojua Mhe. Naibu Spika Baraza la Mapinduzi wakati huo kulikuwa na Mzee Abeid Amani Karume, Mzee Thabit Kombo, Ibrahim Makungu, Mhe. Kaujore na hawa wote leo wamo ndani ya Baraza hili. Ukiangalia Mhe. Ali Karume yumo anawakilisha azma za mzee wake, ukitazama pia Marehemu Mzee Thabit Kombo yumo Mhe. Mahmoud Thabit Kombo anawakilisha, ukitizama na mimi pia Ibrahim Makungu nimo nawakilisha, ukitizama familia ya Kaujore pia imo inawakilisha. Mhe. Naibu Spika, yote haya ni mafanikio wazee wetu wamepanga kufikia hapa leo hii, bila ya wao sisi tusingefikia hapa. *(Makofi)*

Lakini, niseme kitu kimoja kimeniuma sana na leo nakizungumza hapa na *message* itafika. Mhe. Naibu Spika, mimi Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naingia kwenye Bunge kupitia Baraza la Wawakilishi, lakini kitu kimoja kinanikera sana kuwa mjumbe mmoja wa Bunge. Juzi alikuwa anasema anaukashifu Muungano huu wa kupitia Zanzibar, huyu Mheshimiwa anaitwa Mhe. Ally Keissy Mohamed. Mara nyingi sana ukitizama historia tangu kwenye Bunge la Katiba, katiba mpya pendekezwa mimi nilikuwa mjumbe wa kamati ya Bunge la Katiba, lakini alikuwa ana kauli zake mbaya nasema mbaya sana dhidi ya Muungano.

Mhe. Naibu Spika, Mbunge huyu hata hajui Muungano huu umeunganishwaje, hajui Mapinduzi yetu yamekujaje nchi hii. Huu Muungano ni wa kidugu, huu Muungano sio wa mafanikio ya

mapato tu ya fedha, lakini Muungano wa kidugu na nitoe mfano mmoja mzuri Mheshimiwa. Mimi binafsi niliyekaa hapa bila ya Muungano huu au bila ya Mapinduzi yetu ya Mwaka 1964 nisingezaliwa, lakini nimezaliwa baada ya Mapinduzi ni matunda ya Mapinduzi ndio mimi hapa. Nimezaliwa mmoja kuchanganyisha damu baina ya Muhindi na Muafrika, mimi kabila moja ni Mzaramu na moja ni Muhindi. Sasa huu Muungano wetu umechanganisha pande mbili ukiacha mbali ya mapato na kazi za kawaida lakini huu ni Muungano wa damu, tufahamu huu Muungano wa kidamu na umekuja kwa sababu ya wazee wetu kazi kubwa walifanya mpaka Muungano umeunganishwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mtu akiinuka akisema suala la Muungano hasa suala hili la kodi kupitia katika mambo yetu ya mapato katika wafanyabiashara wetu anasema kwamba Zanzibar hailipi kodi, wafanyabiashara wa Zanzibar hawalipi kodi mimi nakataa Mhe. Naibu Spika. Zanzibar jografia yake ni kisiwa na kama tunalipa kodi tunalipa sawasawa kwa sababu hapa kuna *TRA* Zanzibar kuna *TRA* Tanzania Bara. Sasa unapochajiwa kodi unachajiwa kodi ya *TRA* na ukisema kama suala hili la kodi halilipi Zanzibar na jografia yake hata kama kodi itakuwa ndogo Mheshimiwa ndio sisi tulivyo. Zanzibar ukitoka mfano mimi nikitoka nikienda kwa Rais wa Zanzibar nikimuomba nina shida yangu atanisaidia, kama nina shida ya kodi gari yangu siwezi kulipa kodi Mhe. Rais atanisaidia, nikienda kwa Makamu wa Pili wa Rais nikimuomba atanisaidia, nikienda kwa Waziri wa Fedha na Mipango atanisaidia.

Sasa inakuwa mimi nimelipa kodi kihalali, lakini leo ukitoka na mzigo ule ukienda nao Dar-es-Salaam utaambiwa ulipe tena *tax* nyengine. Sasa mimi nasema Mheshimiwa hizi fedha zote zinazokusanywa hapa Zanzibar *ZRB* na *TRA* zinabakia Zanzibar haziendi Bara. Kwa kuwa Muungano wetu huu wa kidugu na kidamu imeonekana kwamba hizi fedha zitasaidia kwenye maendeleo na bajeti ya Zanzibar. Sasa leo tunakuja kushindana kwa jambo hili dogo la kutoka hapa kupeleka mzigo Bara.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilisikia kwenye vyombo vya habari kuna mzigo unatoka Zanzibar umekamatwa mafuta, sukari na mchele vinapelekwa Bara sijui bandari gani vimekamatwa. Sasa haya mambo yatakwenda mpaka lini yatakuwa hivi? Wafanyabiashara mali imeshakamatwa vile basi itataifishwa ni hasara itakuwa na hawa wafanyabiashara wa Zanzibar watapeleka bidhaa zao wapi? Soko kubwa liko Tanzania Bara, ukipita kwenda Kenya, Uganda upitie Tanzania Bara hata ukipita *transit* utaambiwa ulipe ushuru. Sasa mimi naomba sana tuangalie huu Muungano wetu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania basi iweko kitu fulani ukishakulipa kodi hapa iwe mzigo unakwenda.

Mara nyingi ukitizama mimi nimetembelea bandarini Tanzania Bara utakuta watu wanalipishwa kodi zile fedha wala haziendi serikalini, mtu anachukua kwa matakwa yake na hasa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa kweli, inaniuma sana mfanyabiashara wa shilingi milioni kumi au mfano anachukua televisheni yake moja au mbili anapeleka Bara analipishwa kodi. Hili jambo tuliangalie sana huu Muungano wetu ni wa kidugu ukiacha mambo ya mapato madogo madogo. Hawa wananchi wetu asilimia 40 wajiajiri wenyewe kwenye biashara ndogo ndogo hizi za kuchukua bidhaa hapa kupeleka Tanzania Bara, ili kupata ajira kila siku hatuwezi kuajiri vijana wote au watu wote serikalini itakuwa shida. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri hili suala wakae chini waangalie vikao vifanyike kwa nia njema kwa nchi yetu hii Muungano huu. Kwa sababu huu Muungano mimi naomba usivunjike na uzidi kuimarika siku hadi siku kwa

sababu una mafanikio makubwa kwa Zanzibar pia kwa jumla Tanzania nzima, lakini tuuboreshe kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitoe mfano mmoja, leo tuko mwaka 2018 kesho tunakwenda 2019, 2020 tutakwenda kwenye kampeni za kisiasa. Mimi jimbo langu mwanzo lilikuwa la Bububu lile pale uchaguzi mdogo, uchaguzi wa pili jimbo la Mtoni juzi, lakini wanakuja wapinzani wanazungumzia hawazungumzii maji hawana, hawazungumzii hawana barabara, hawazungumzii hawana ajira, hawana hospitali, wanazungumzia Muungano tu, kwa nini iwe hivyo? Kila siku tunakwenda kwenye Muungano huu tunautia doa Muungano wetu mzuri kama nini, tunakwenda kuutia doa kwa nini. Naomba sana Mhe. Waziri aliangalie sana hasa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wasaidiwe mizigo yao iende kwa sababu itakuwa *double tax* kila siku unalipa ushuru mara mbili.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa mfano kidogo, kuna wafanyabiashara pia wakichukua mzigo kutoka nje kama sasa hivi meli kubwa zinafikia Dar-es-Salaam hazifiki huku, ikiwa kuna gari mfano Fuso pale ndani yake unaambiwa ulipe kodi ya *wharfage handling* na *storage* unalipa Dar-es-Salaam, ukishakulipa pale kama unakuja huku mzigo pia magari hayo ukija huku unalipa tena *wharfage* na *storage* na *charge* unalipa tena huku. Kwa hivyo, ushalipa mara mbili tayari, ukitoka gari hiyo hiyo mfano uichukue tena uipeleke tena Tanzania Bara utalipishwa tena kodi hiyo hiyo, sasa hebu tumfikirie huyu mfanyabiashara kweli atakuwa na faida katika biashara yake hiyo?

Mzigo umetoka pale katika *transit* amelipa kodi kuna *tax* fulani unalipa, ukija hapa unalipa tena na ukitoka hapa umelipa *tax* ya *TRA* unalipa ushuru wa thamani, ukitoka ukiisafirisha tena ukienda Bara wanai-*vain* tena upya ule mzigo kwa kulipa kodi tena. Sasa utakuta ile kodi utayolipishwa kule inachajiwa kama gari imekuja leo kutoka nje sio kama imetoka miaka mitati au minne iko hapa *valuation* yake inakuwa kubwa. Sasa huyu mfanyabiashara jamani tunataka tumuuwe, tunataka afilisike asifanye hii biashara hawezi ku-*resist* mfanyabiashara, hiki kitu atafilisika tu huyu acha tuangalie sana hizi kodi mtu akishakulipa hapa ushuru na hapa kuna *TRA* hiyo kodi waithamini na kule bidhaa iweze kuingia kwa bei yoyote ambayo huku imekusanywa. Kwa sababu jografia ya Zanzibar ni kisiwa hakuna njia nyengine ya kufanya biashara isipokuwa kwenda Tanzania Bara, hata kama kuna kodi basi iwe ndogo kama zamani, unalipa kodi mtu hulalamiki. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hiyo kodi ukipiga hesabu unalipa karibu mara nne kwa kitu kimoja hicho hicho. Sasa hawa wananchi wetu wanatulaumu mwisho wa siku, watakwenda watauchukia Muungano wetu huu mzuri kwa kupita kusema mambo mbali mbali, kupita kusema mambo ya ajabu. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri aangalie sana suala hili hasa la hawa wafanyabiashara wetu walipa kodi mpaka ndani ya Bunge inafika huyu Mheshimiwa anaependa kuidhalilisha Zanzibar kusema kwamba Zanzibar hailipi kodi. Hiyo nasema sio lugha nzuri sana aliyoitumia na sijafurahi, sijapata kumjibu lakini iko siku nitamjibu ndani ya Bunge afahamu kwanza historia ya Zanzibar hii aifahamu Muungano huu umekujaje na Mapinduzi yetu yamekujaje hata kufikia hapa Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika ukurasa wa saba (7) kwenye huduma ya afya. Naipongeza sana serikali kwa kazi zake, niipongeze, niishukuru sana kwa kazi yake kubwa ya kuimarisha

huduma ya afya, sio kazi ndogo na hasa katika wizara hii ya afya jambo kubwa lenye gharama kubwa ni dawa, zile dawa ni gharama kubwa na wananchi wetu wa Zanzibar wakienda Hospitali ya Mnazi Mmoja wapate dawa bure, wamezoea matibabu bure na dawa ukiangalia kidogo tu zinakuwa pesa nyingi sana. Sasa naomba sana kupitia serikali yetu na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iangalie kuhamasisha watu wote wawe na bima. Watu wakiwa na bima wakienda hata Dar-es-Salaam wanatibiwa bure ile bima ina-*cover*. Sasa watu wetu wengi kwenye majimbo yetu hata kwenye serikali na sehemu mbali mbali watu bima hawana wanategemea kulipa *cash*, wakilipa *cash* matibabu ya afya si rahisi kuyaweza.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana tuangalie suala hili la afya, tukiangalia vituo vyetu vya afya viko karibu 175 vinatoa huduma hizo, sasa kama huna bima ya afya hapa kuwa serikali ihudumie dawa na kila kitu tutashindwa mzigo mkubwa sana utakuwa. Kwa hivyo, mimi naomba wahamasishwe kuanzia wananchi wetu wa majimbo pia wajue, wazee wetu ili waweze kuwa na bima na kuwa na bima sio kwenda kwa *NHIF* ukiangalie kwa *group* utapata mtu karibu hata shilingi 10,000 kwa mwezi inafika au chini ya hapo. Kwa hivyo, naomba sana kupitia serikali itolewe elimu ya hali ya juu kila mtu awe na bima yake ili iweze kumsaidia katika huduma hii ya afya.

Pia nije kwenye huduma ya maji safi na salama. Ukiangalia hapa serikali inajitahidi sana na niipongeze sana kwa suala hili la maji safi na salama. Lakini tukiangalia shida ya maji bado inaendelea kwenye majimbo yetu kila siku ipo. Sasa haya mambo yatakwenda mpaka lini, kila ukitizama maji hayapo. Ras-el-Khaimah walichimba visima karibu 150 visima vinavyofanya kazi kama vitatu au vinne kama vinafanya kazi. Sasa hili tatizo naomba sana serikali iangalie suala la maji ni kilio kikubwa kwa wananchi wetu hawa wapiga kura wetu wanasikitika sana suala la maji bado halijakaa sawa. Kwa hiyo, *ZAWA* naomba watoe takwimu za kutosha kwa nini maji yanakuwa mpaka leo hayapatikani? Huu mwaka wa tatu au wanne.

Mhe. Naibu Spika, lakini niipongeze sana serikali katika Mfuko wa Jimbo wa kupewa wawakilishi, unatusaidia sana mambo mengi hasa utakuta haya mambo ya maji tuwe tunashughulikia kuchimba visima, kuweka *tanks* ya maji. Naipongeza serikali yangu na naishukuru kwa msaada wao inatusaidia kwa Mfuko wetu wa Maendeleo ya Majimboni mwetu, lakini naomba Mfuko huu kila ikifika wakati upatikane kwa haraka, kwa sababu upate kusaidia mambo mengine, kwa sababu ukichelewa sana inakuwa na huku mambo yanakwama. Sasa naomba kama wenzetu Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukifika muda tu Mfuko wa Jimbo wanapata kwa hivyo, naomba sana na Wawakilishi hali zetu kidogo sio nzuri mambo mengi kwenye majimbo naomba tufikiriwe sana kwa Mfuko wa Jimbo ikifika muda wa kupewa tupate hizi fedha tuweze kuwatumikia wananchi vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa sita kwenye *bullet* ya 20. Nataka niipongeze sana Serikali yetu ya Zanzibar kwa jitihada zake kubwa hasa katika upande wetu huu wa Uwanja wa Ndege wetu wa Abeid Amani Karume. Ukiangalia pia Uwanja wa Karume Pemba pia hili suala la taa niipongeze sana serikali. Baraza lililopita hapa ilikuwa kilio kikubwa hizi taa za uwanja wa ndege, lakini leo Pemba unaweza kutua hata saa moja, saa mbili usiku uwanja unafanya kazi. Hii juhudi sio ndogo karibu shilingi 1.2 bilioni serikali imetumia kwenye uwanja huo kwa kutia taa.

Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Rais kwa juhudi zake kubwa na wizara nzima ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushughulikia hili suala, ilikuwa kero kweli kweli, lakini leo nashukuru wananchi wanafaidika kwenye uwanja ule kutua usiku na mchana. Hili ni jambo jema nakipongeza Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kazi zake nzuri inazofanya.

Mhe. Naibu Spika, niseme kitu kimoja, mbali ya juhudi ya serikali inayofanya kuna ndege mbali mbali zinatua kutoka Zanzibar, zinakuja zinazotoka nje na kuja Zanzibar kama Urusi moja kwa moja, Itali kuna ndege karibu ngapi zinakuja kwa siku moja kwa moja, kuna ndege Shirika la *Qattar Airlines, Kenya Airways, Fly Dubai,* ndege nyingi zinakuja sisi tunashukuru, kuna *Turkish Airlines*.

Mheshimiwa lakini mimi nisikitike kitu kimoja, mimi uwanja huu nautumia sana kila mara nakuwa nasafiri kwenda Dodoma, kwenda hapa na kurudi. Mvua za juzi Mheshimiwa mimi nisikitike uwanja ule unaotumika sasa hivi *Terminal I* unavuja, wageni wanakuja wanapitishwa huku badala ya kutoka *departure* wanapita *arrival***.** Sasa Mheshimiwa hawa wageni wanatoka nje watalii wanakuja kutumia pesa kwenye nchi yetu visiwa hivi leo wanakuja uwanjani wanakuta hali kama kuna mafuriko. Sasa kwa nini *airport* hii ndogo inavuja, angalau iwe *airport* mgeni kafika pale kachoka lakini *airport* iko safi, maji ndani hamna, lakini leo maji yamo ndani unaweza ukaanguka kwenye *tiles* ukaanguka.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mkurugenzi wa *Airport* ndugu yangu Kapteni Said hodari anajitahidi sana mambo mengi, lakini nawaomba hawa watendaji pia akaenao chini awafahamishe, kwa sababu hili suala la watalii kuja kwetu ni pato la taifa letu sote, wageni wakishuka pale ndio sisi tunafaidika kwenye pato la taifa karibu asilimia 70 tunategemea watalii sisi Zanzibar. Sasa wageni wakija pale wakiona hali ya *airport* haiko sawa huku nje kutakuwaje?

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mkurugenzi wa *Airport* aangalie na serikali ichukue hatua ya kuangalia jicho lake kwenye *airport* yetu hasa wageni wanaposhuka na kuondoka.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ukiangalia mgeni yeyote akitoka *airport* atapita njia ya Kiembesamaki anakwenda mjini, lazima apite hapo akiwa Mtaliana, akiwa Mmarekani, akiwa Muingereza kabila yoyote ile. Ukitizama njia hii mheshimiwa ni aibu kubwa siku za mvua. Juzi hapa magari yamekaa hayawezi hata kupita maji yamejaa, sasa kwa nini tusifanye jitihada ya kutosha njia hii tukaiokoa ikawa haikai maji tukatia hata bomba pale likaenda mpaka baharini. Mimi si mtaalamu wa mabomba ya maji lakini unaweza ukanambia sasa hivi nifanye nini nikachimba msingi pale nikachukua maji mpaka baharini ili maji yasikae pale.

Mhe. Naibu Spika, ni aibu kwa sababu wageni wanaokuja ni *Five Star Hotel*. Kuna hoteli vyumba mpaka US$ 2000 kwa usiku moja, kuna vyumba mpaka US$ 1000 hapa vinachajiwa kwa usiku mmoja, leo mgeni anakuja gari yake ikipita pale aibu, kwa maji haiwezi kupita inapita njia ya nyuma huko mashimo mengi, ukiangalia sasa hivi tumetoa hizi Serikali za Mitaa kuwapa hawa ndugu zetu washughulikie hizi barabara lakini hawawezi, hizi fedha ni nyingi naomba Wizara ya Mawasiliano itie mkono wake.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe muda wako umekwisha.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Haya Mhe. Naibu Spika, mimi namalizia kidogo, nimalizie na...

Mhe. Naibu Spika: Nakupa dakika moja tu ya kumalizia.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Haya ahsante. Mhe. Naibu Spika, nimalizie lakini naona muda mdogo mambo mengi, kwa hivyo nitachangia kwa maandishi. Mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja hii kamati yangu naifahamu vizuri, Mhe. Waziri nakaa naye najua lakini nimesema changamoto baadhi ili kujua, lakini naunga mkono kwa asilimia mia moja nashukuru ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Husein Ibrahim Makungu. Waheshimiwa Wajumbe, sasa hivi tutaanza kupata mchango kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri mbali mbali ambao kwa njia moja au nyengine wameguswa katika wizara zao na hotuba hii ambayo tunaijadili sasa hivi.

Hivyo, naomba Mawaziri niwape dakika kumi na tano, kumi na tano muweze kueleza na kwa sababu kunakuja wizara zenu baadae mtaweza kutoa ufafanuzi wa ziada wakati wa bajeti ya wizara zenu. Naanza na Mhe. Said Soud Said Waziri asiekuwa na Wizara Maalum.

Mhe. Said Soud Said: (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuzungumzia hoja ya Hotuba ya Makadirio na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nachukuwa nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na pia nachukuwa nafasi hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kutokana na harakati zake za kusimamia shughuli za Muungano kwani afisi hii ni afisi inayohusiana na mambo ya Muungano na mimi kama Mwenyekiti wa Chama cha Siasa Tanzania Vyama vya siasa ni vya Muungano. Kwa hiyo, mimi nineguswa na afisi hii na nataka niwaambie Wazanzibari na Watanzania wote kwamba Muungano wetu umetokana na Chama cha *ASP* na *TANU* baada ya kuungana na hatimae kuzaliwa Muungano tarehe 26. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nachukuwa nafasi ya kuupongeza Muungano kwamba ndio chombo pekee cha Watanzania wanaojivunia ndani ya Tanzania yao na nje ya Tanzania. Mhe. Naibu Spika, Muungano wetu ni dhahabu kwa vile hakuna mtu ambaye anaweza akaichafua dhahabu hata ukiitia tope basi itasafishwa itarudi pale pale kama dhahabu. Kwa vile yale yanayozuka zuka ya maneno mawili matatu kwenye Bunge au kwenye Baraza ni katika jumla ya kuitengeneza hiyo dhahabu.

Muungano utabaki kama Muungano na Wazanzibari wajivunie sana Muungano na nachukuwa nafasi hii kuwaambia kwamba Wapemba ndio waliofaidika zaidi na Muungano, kwa sababu mara tu baada ya Mapinduzi walifanya kukimbia na hatimae wakaingia Tanzania Bara na

Muungano ukawadhibiti mpaka leo wapo. Kwa hiyo, Muungano ni chombo pekee kinachohitaji kuheshimiwa na kulindwa kwa gharama zozote katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais imekuwa ikifanya mambo mengi makubwa katika kutekeleza majukumu yake yaliyoandaliwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi umefika wakati wa kusema kweli Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa sana kiasi cha kwamba mimi naweza kuthubutu kusema kwamba ifikapo 2020 nchi hii hakuna *CUF* hapa. *CUF* hakuna tena 2020 na nasema hivyo, kwa sababu kama wao waliandaa lazima kutakuwa na maendeleo, maendeleo yanaletwa na Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Mapinduzi na maendeleo yaliyopatikana ni makubwa sana kiasi cha kwamba ni maendeleo yaliyokuwa yanatekelezeka si maendeleo ya kuwadanganya watu kwamba utajenga gati kati ya Nungwi na Mkoani, yale ni maendeleo ya kudanyanya watu. (*Makofi*)

Lakini maendeleo ya Ilani ya Uchaguzi ni maendeleo yanayofanywa kwa uhakika na yanatekelezeka na leo hii Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akiwa pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha CCM, naweza kusema anakwenda na mwendo kasi yaani anakwenda na mwendo kasi katika kuteleza Ilani kama yale mabasi yalioko Dar-es-Salaam ya mwendo kasi basi na yeye anakwenda na mwendo kasi katika kuteleza hii hoja.

Sasa kimsingi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu ndio afisi ambayo inashughulikia zaidi mambo yetu ya Vyama vya Siasa na hata tunapopewa mialiko kupitia vyama vyetu kwenda Tanzania Bara hata juzi tulipokwenda kwa sherehe za Muungano basi tulipewa barua kutokea Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba ndio inayoratibu mambo ya Muungano.

Sasa afisi hii kwa sasa lazima tuseme kwamba imepiga hatua kubwa sana, kwa sababu sote ni mashahidi wa kuona kwamba *TASAF* imechukuwa nafasi kubwa katika kunyanyua hali za maisha ya watu katika visiwa vya Unguja na Pemba. Lazima tukubali kwamba taasisi ya *Sober House* imeweza kuwarudishia vijana wetu uhai katika mazingira mazuri sasa ambayo wanaweza kujituma katika kutafuta rizki za halali.

Lazima tukubali kwamba afisi hii yanapotokea maafa Makamu wa Pili wa Rias pamoja na watendaji wa afisi yake wanakuwa tayari kukabiliana na maafa hayo katika visiwa vyote viwili Unguja na Pemba bila ya kujali muda wao na hivi sasa maandalizi yote yanaandaliwa katika mazingira ya kuondoa maafa katika lile shimo la Mwanakwerekwe na kule Kibonde Mzungu. Ni kwa sababu gani ofisi hii inaratibu matatizo ambayo wananchi wasiweze kukumbana nayo. Lazima tukubali kwamba ofisi hii inaenda vizuri katika mazingira ya kuendeleza masuala ya uchaguzi kupitia Tume ya Uchaguzi.

Sasa hii ni afisi kubwa katika nchi yetu hii ni afisi kubwa ambayo wizara zote tunaangaliwa na afisi hii. Afisi hii inahitaji kupewa kila aina ya msukumo ili iweze kupiga hatua na sisi sote ni mashahidi kumuona kwamba Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar amekuwa halali usiku wala mchana pahala popote panapotokea matatizo yeye anakuwa tayari kufika pale katika mazingira ya kuweza kukabiliana nayo.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme na naendelea kusema kwamba sisi sote Wazanzibari na Watanzania tukubali kwamba tumekombolewa na lazima tuthamini vyama vilivyotukomboa ikiwemo kuwa tumezaa chama kimoja kinachoitwa CCM baada ya kuwa CCM ni Chama cha Mapinduzi lakini pia kina sifa ya kuwa ni Chama cha Ukombozi. Wazanzibari tuheshimu sana Muungano, Wazanzibari tuheshimu sana nchi yetu na Mapinduzi yetu ya Zanzibar hakuna mtu yoyote aliyeweza kupambana na kuondoa idhilali ya Wazanzibari zaidi ya Afro - Shirazi, hakuna mtu yoyote alieondoa idhilali ya Watanganyika zaidi ya *TANU*.

Sasa leo tumekuwa na uhuru wetu tumekuwa na uwezo wetu tusisahau tulipotoka lazima tusimame tulikotokana. Hivi vyama vyengine vyote ambavyo viko huku nyuma vinashangilia maendeleo vibakie kushangilia maendeleo lakini vithamini ukombozi wa Tanzania, wathamini ukombozi wa Zanzibar na wathamini ukombozi wa Tanganyika tusiwe tayari kugombanishwa wala kufitinishwa katika mazingira ya kujenga Umoja wa Taifa moja la Watanzania.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia na naamini Wajumbe walio wengi wataacha ile dhana ya mabuti ili bajeti hii ipite mara moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum), mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda na baadaye atafuata Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati na ajitayarishe Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukuwe nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo sote hapa tunakutana tena baada ya mwaka mmoja katika kikao hichi muhimu cha Bajeti.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nichukuwe nafasi hii pia nimpongeze Mhe. Rais wetu kipenzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kazi nzuri anayoifanya kwa uvumilivu wake na kwa ukakamavu wake na vile vile kwa kuona mbali sana kujenga taifa letu hili la Zanzibar na Tanzania. *(Makofi)*

Pia Mhe. Naibu Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa wetu Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Idd kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi lakini vile vile na nje kama ni msimamizi wetu mkuu wa shughuli za serikali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza wenzetu Waheshimiwa Wawakilishi wote sote naona tuko salama tuna afya njema, tuko tayari kuendelea kuchambua bajeti zetu kwa amani na utulivu na kuweza kuiwezesha serikali iendeleze kufanya majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niseme mwanzo kabisa kwamba naunga mkono Bajeti ya Mhe. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais mia juu ya mia. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nitakuwa na mambo machache kwa ajili ya kukazia tu pale ambapo tunaona kuna haja ya kukazia baadhi ya maeneo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kitabu cha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais imeeleza mambo mengi yakiwemo ya uratibu wa shuguhuli za SMZ mambo ya uratibu ya SMT na SMZ kamati mbali mbali za SMZ na SMT mambo mengi yameelezwa katika kitabu chako na mengi katika mambo haya naweza kusema kwamba yamefanyika kwa ufanisi wa mia juu ya mia. Kutakuwa na kasoro ndogo ndogo lakini ndio kawaida katika utekelezaji wa bajeti lakini sehemu kubwa ya mambo ambayo yalipangwa kwa wizara hii yametekelezwa na yamekwenda vizuri na yametuunganisha sisi vizuri kama watendaji wa wizara mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chake nilitaka nizungumzie ukurasa wa 15 unaozungumzia masuala ya uratibu. Hapa Mhe. Naibu Spika, ningezungumzia kifungu cha 20 ukusara wa 15 na 16 kifungu cha 21. Hii Mhe. Naibu Spika inayohusu kuhusu vikao vya uratibu juu ya mashirikiano baina ya SMT na SMZ. Kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Rais katika kitabu chake Mheshimiwa tumegipa hatua nzuri si tulivyotoka pale mwanzo na sasa hivi kuna hatua kubwa iliyopatikana vikao vimekaa kama ilivyoelezwa humu vya watendaji Makatibu Wakuu na maofisa mbali mbali, vikao vimekaa vya mawaziri naweza kusema kwamba kikao cha mwisho tulichokaa na kimesimamia na mwenyewe Makamu wa Rais wa Tanzania kilifanyika juzi tu mwezi wa Novemba ambacho kiliweza kupunguza baadhi ya changamoto ambazo zilizokuwepo muda mrefu ziliweza kupunguzwa.

Kwa hiyo, niseme kwamba ile nia ya kutaka kukaa inaonekana ya kukaa na kuyamaliza mambo ambayo yalikuwa ni changamoto ipo Mhe. Naibu Spika na mambo mengi yamemalizwa lakini bado Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika mambo ambayo yamekuwa sugu na yamekuwa kama changamoto ambayo haipati suluhu ni mambo yanayohusu masuala ya fedha, uchumi na biashara.

Mhe. Naibu Spika, kikao cha mwezi wa Novemba tulichokaa tulifuata maamuzi kwamba sekta hizi tatu tukae tuweze kupata ufumbuzi wa baadhi ya mambo ambayo yana usumbufu na matarajio yangu pengine mwenzangu anayeshughulikia fedha na uchumi kwa upande wake watakuwa wameshakaa masuala ya kero ambayo ya muda mrefu wa magari yatakuwa yamo katika upande wake nadhani haya nayo yanazungumzwa katika ukumbi huo.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa biashara changamoto katika sekta hii nayo ilipatiwa nafasi ya kuzungumza. Ningeomba niwafahamishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi vikao vilikaa kama tunavyotakiwa tukae na kikao cha mwisho cha Mhe. Makamu wa Rais wa Tanzania Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan tulikaa na tukakubaliana basi tiite kikao chengine ambacho kitazungumzia masuala ya biashara na vikwazo walivyopata wafanyabiashara wa Zanzibar wanaokwenda kufanya biashara zao Bara na mambo mengi yanayohusiana na masuala ya biashara.

Mhe. Naibu Spika, kikao hichi kilikaa hapa Zanzibar kama miezi miwili nyuma na kuna mambo tulikubaliana yakawa vizuri sana na kuna mambo tulikubaliana kwamba tukae vikao maalum kuvitatua hizo changamoto kwa mfano changamoto ya Zanzibar kujiunga kwa baadhi ya vyombo vya kimataifa tulikubaliana tukae pamoja na changamoto nyengine ambazo zitaweza kumalizika. Kwa bahati mbaya wenzetu Serikali ya Muungano wametwambia kwamba wao wana Bajeti sasa hivi lakini tutakaa karibuni kuweza kumaliza hizi changamoto ambazo zilizobakia.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba upande wa vikwazo vya biashara. Wafanyabiashara ambao wanazalisha vitu vyao kwa mfano wale wanaopeleka vitu kama sabuni majani ya chai na vitu vyengine kama maji. Utaratibu ambao tulikubaliana kwamba lazima vyombo kama hivi kampuni kama haya hapa Zanzibar lazima yawe wanasajiliwa, lakini pia yaweza kuweza kupitia katika utaratibu wa vyombo vinavyokagua ubora vinavyokagua afya ya mtumiaji na kadhalika, na tukatoa vile vile nambari ya simu *hot line* wanavyosema wenyewe ambaye yule ambaye atakaekuwa bado bidhaa zake zinapata tabu kupelekwa Bara aweze kujuilisha Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na vile vile Afisi ya Makamu wa Rais hizo namba zipo na tumewatangazia wananchi wote kwamba wakikwama watujulishe.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri mpaka sasa hivi wizara zote tatu hizi wizara yangu, Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Afisi ya Makamu wa Rais Tanzania sijaletea taarifa kwamba kama kuna mtu kapiga simu kulalamika kwamba kwa upande wa bidhaa hizi kuna malalamiko yoyote ama wamepata vikavyo vyovyote. Lakini pamoja na hayo kama bado kuna kampuni au kuna mashirika au kuna vyombo vya Zanzibar vinauza biashara Bara katika maeneo haya kama wanapata vikwazo basi tunawaomba watujulishe tuweze kuzifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, tatizo lililobakia ambalo linatusumbua au halitusumbui lakini naona niseme kwamba limekuwa limeingia katika upande ambao sio mzuri. Mhe. Naibu Spika, tumesikia leo malalamiko ya Waheshimiwa wetu hapa Wajumbe wa Baraza kuhusu suala zima la sukari. Lakini mimi niseme tu kwamba jambo ambalo katika kipindi cha mwaka huu kama mtu ataniuliza jambo gani Mheshimiwa limekuwakatisha tamaa na sikulifurahia ni suala zima la sukari. (*Makofi*)

Suala la sukari Mhe. Naibu Spika, lazima niwe muwazi na wenzangu mnaelewa mimi ni mtu ambaye niko katika Baraza hili kwa muda mrefu nimefanya katika Bunge na nimefanya kazi katika Baraza la Wawakilishi kwa muda mrefu. Lakini Mhe. Naibu Spika, nakiri kusema kwamba hili jambo la sukari limetuweka mahali si pazuri. (*Makofi*)

Sasa kwa nini nasema hivi Mhe. Spika, sisi kwa upande wa SMZ hatukulizungumza suala hili sio kama tulilifurahia hapana hatukulifurahia lakini tuliona kwamba ndugu wakishagombana na wewe ukenda ukaongeza kutia maneno pale inakuwa sasa unaongeza jazba, ndio maana tukanyamaza kwa sababu utaratibu wa kuzungumza mambo yetu kiserikali upo wazi na tunakaa tunazungumza tunakubaliana.

Mhe. Naibu Spika, katika Baraza la Wawakilishi na Bunge vile vile kuna Kanuni sikumbuki Kanuni ya Bunge lakini nakumbuka Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinasema kwamba Mwakilishi au Mbunge hatakiwi kuzungumza lugha za kukera au za kuudhi.

Kwanza naomba nichukuwe nafasi hii kuwapongeza leo Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwa jambo hili la sukari wao hawakutumia lugha za kuudhi, nawapa pongezi wote wawakilishi, lugha waliyotumia leo hapa ni ya kistaarabu ambayo ni yakutunganisha pamoja na kukosoana pale panapotakiwa kukosoana. *(Makofi)*

Lakini ningeomba suala la sukari lisitugombanishe sana, na likatutoa katika muelekeo wetu wa muungano kama nilivyosema pale mwanzo halikuwa jambo zuri, haiwezekani Tanzania nzima

ikatetemeka kwa suala la sukari ya kiwanda kimoja haiwezekani kwa sababu zozote vile haiwezekani.

Mhe. Naibu Spika, suala la sukari mwanzo lilianza kwamba Zanzibar wanapitisha sukari kwenye panya *road*, *route* za panya zilizokwenda Tanga Pemba, lakini tukasema suala la magendo sisi tuna Kikosi chetu Maalum cha Kuzuia Magendo na SMT nao kupitia TRA na *NAVI* na wanao vikosi vya kusimamia. Lakini hili jambo tulizungumze kwa pamoja hio ilikuwa sababu ya kwanza.

Lakini sababu ya pili Mhe. Spika tukaambiwa kwamba Bara wanalinda viwanda vyao vya sukari lakini juzi tukaambiwa tena kwamba kuna wafanyabiashara wa Zanzibar wamepewa ruhusa kuagiza sukari Bara. Sasa nalizungumza hili si kama nazungumza kulirudisha nyuma suala la sukari tena ni mjadala huu na ningeomba ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi tulimalize majadala huu tuumalize kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumekwisha kulimaliza hili suala tumelifanyia kazi na maamuzi yatakayokuwa muafaka kwa sisi wote yatatokea.

Nalizungumza kwa sababu hivi juzi kumetokea mambo mengine, na imekua saivi kama *drama* watu wakitaka kujionyesha kama wasemaji wazuri, wapinzani wazuri wanatumia suala la sukari na kuweza kutifua hali ya hewa ya nchi yetu. Mheshimiwa, jana walikuja watu wa Kiwanda cha Sukari kwangu na waliniambia kwamba Serikali ya Muungano imetoa vibali, kampuni au viwanda vingi vimepewa vibali kuagiza sukari, Kiwanda cha Kilombero, Kiwanda cha Kagera *sugar*, Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa na na kiwanda cha *TTC* cha Kilimanjaro hawa wote wamepewa ruhusa na bodi ya sukari kuagiza sukari.

Sasa mimi waliniuliza sasa vipi suala hili kwa sababu na sisi tunajihesabu kiwanda cha Tanzania kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya Tanzania. Kwa kuwa mimi najua maamuzi ya SMZ tumeshaamua katika suala hili nikawambia basi tuacheni, lakini ukiangalia katika suala zima la *principle* Mhe. Naibu Spika na Waheshimiwa Wajumbe mimi kwa kweli hili jambo kwa kweli nimeacha *precedent* mbaya. Kwa sababu kama unazungumzia Tanzania naona tunajua Sote tunajua si tunajua na wenzetu wa muungano wanajua kwamba Tanzania ni soko moja. (*Makofi*)

Lakini pia Tanzania tumesaini Mkataba wa Forodha, lakini ukenda mbele zaidi Tanzania tuna mfumo wetu mmoja wa fedha *currency* moja, usimamiaji wa fedha za kugeni ni mmoja hata *channel* zetu za fedha zinalingana lingana, kwa sababu ukiwa na taifa kama hili moja huwezi kuwa na sera za fedha zikawa zinatofautiana. Huwezi kuwa sisi tukawa na kodi yetu chini na wao wakawa na kodi yao kubwa haiwezekani hivyo, kutakuwa na khitilafu ndogo ndogo lakini haiwezakani tukawa tunatofautiana.(*Makofi*)

Kwa misingi hio Mhe Naibu Spika, mwaka 1964 – 1965 tunaingia katika mashirikiano haya ya kifedha tulifanya kwa makusudi yaani wazee wetu waifanya kwa makusudi, kwa ajili ya kuiweka Tanzania ni nchi *stable* na nchi itakayoweza kufanya maendeleo hasa mkiwa na sera zenu na mkifanya mambo yenu kwa pamoja ndivyo mnapoweza kushinda na kuweza kusonga mbele kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 1964-1965 Zanzibar haikuwa na hali hii. Sasa inapokuwa maamuzi yanakuja kama haya na hajawahi kutokea mimi sikumbuki maamuzi kama haya kwamba nchi

moja upande mmoja kusema upande mmoja akasema hichi hatutaki sijapata kuona sijawahi kusikia tangu nimeingia katika siasa sijawahi kusikia na hii inaweka *bad precedent* na hii inaweka ufa katika masuala ya muungano na hii inataka viongozi sisi viongozi kuanzia juu mpaka chini tuwe na *vision* moja. (*Makofi*)

Hatuwezi kufanya mambo kama haya ambayo una-*pick* kitu kimoja sukari isingie, sasa lakini Tanzinia ni nchi moja taifa moja. Naomba nitoe mfano kulikua……

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda, naomba umalizie nakupa dakika nne. Aaa! Hamjanisikiliza, misinizomee nisikilizeni vizuri sana nampa dakika nne, nafikiri anawe kumaliza nimeshampa tayari nimemuongezea muda na baada ya huo niliomungezea kwa sababu nilisema dakika 15 lakini nimempa 20 na nyengine namuongezea. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, nakushukuru kwa sababu naomba suala hili tulimalize leo lishe. Kwa hiyo, naomba nitoe mfano nchi moja waligombania manofu ya kuku kuna nchi upande mmoja inakula kuku kuna nchi upande mwengine inakula mapaja wengine kidari wengine mapaja ikaleta matatizo karibu ya vita ya biashara. Pia kuna nchi nyengine walidharau nchi nyengine upande wa pili kwa sababu hawana uwezo wao ndio wenye uwezo wakafungia bidhaa fulani wakasema wasilete huku wakasahau kwamba kuku, nguruwe wanaliwa na watu walioko huku watu wengi ingawa hawana uwezo yakaja matatizo.

Kwa hivyo, tujifunze katika mambo haya Zanzibar mwaka 1965-1967 tulikuwa na fedha na uwezo mkubwa tulikuwa na pauni milioni 25 kwa sauti ya mwenyewe marehemu Mzee Karume tujifunze na hayo, tujenge nchi yetu tu tunaweza kujenga nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba tu hili suala la sukari wenzetu wa Serikali ya Muungano wakalichukulia hatua ipasavyo hao wafanyabiashara ambao wanapata fursa ya kuuza kule sukari, na wao vile vile wafikirie kwa sababu kuna kiwanda chao hapa kwa hivyo wanapozuia kiwanda wakaruhusu wafanyabiashara tayari hapo unakuwa kushabagua. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kimsingi ni kwamba sisi SMZ tushaamua tutakula sukari yetu tutakunywa sukari yetu na tutaitumia sukari yetu kwa mambo yetu yote kwa hivyo sio tatizo tuna uwezo huo tutachukua maamuzi magumu na tushachukua maamuzi magumu kwa hivyo tufanye kazi viwanda hivi vinategemea soko la Bara hatuwezi kusema soko la bara sio muhimu, kwa hivyo wenzetu nao watuone sisi vile vile kwa wakati huu tunahitaji soka la Bara.

Lakini pia na mwisho nisema kwa ndugu zangu wa Zanzibar hasa Waheshimiwa Wawakilishi tujitahidi kuzalisha vitu wenyewe na kutafuta njia nyengine tutokane na utegemezi wa mahali pamoja, lazima tutafute njia nyengine masoko sio Bara peke yake, masoko yako maeneo mengi tufanye hivyo tuweze kufika mahali pazuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka niseme hayo na masuala mengine ambayo yote ambayo yamezungumzwa kuhusu biashara yako vivuri hakuna ugomvi tunakwenda vizuri *ZBS* na *TBS* wanashirikiana *ZFBA* na *TFBA* wanashirikiana kilichobakia cha sukari hichi, lakini kama nilivyosema hii ni *normally* na hatuwezi kuiruhusu lazima serikali ijibu hivi tumalize masuali haya na tusiruhusu kwamba madhali Morogoro zinakwenda bidhaa Zanzibar hazizuiliwi, basi na

bidhaa za Zanzibar vile vile zisizuiliwe kwa visingizio vyovyote vile. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nakushukuru sana Mhe. Balozi Waziri wa Biashara na Viwanda, sasa hivi nitampa nafasi Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, karibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba nianze kwa kumshukuru *Allah Subuhana Wataala* kwa kutufikisha hapa sasa hivi tukiwa katika hali ya uzima lakini tukitekeleza majukumu yetu ya kazi kama inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyoiendesha serikali na kusimamia vyema ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Aidha, naomba kumshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa jinsi anavyotupa miongozo yake mbali mbali katika kuhakikisha kwamba serikali hii inafanya kazi za kufanya mafanikio na kutekeleza ilani lakini vile vile kuhakikisha kwamba zile changamoto zilizojitokeza tunazi-*over come. (Makofi)*

Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri , Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa namna ya kipekee alivyokuwa anaiendesha wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuna mambo mengi yamejitokeza yanayohusiana moja kwa moja na Wizara yangu ,Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati. Na napenda kuchukua nafasi hii basi kuyatolea ufafanuzi mdogo tu kwa sababu bajeti yangu itakuja na watapata Waheshimiwa Wawakilishi fursa kubwa ya kuweza kuijadili na kutoa haya ambayo walikuwa nayo.

Kwanza naomba nichukue nafasi hii sana kuwashukuru wale wote pia waliojitokeza kuchangia kuhusu Wizara yangu. Naomba sasa niingie moja kwa moja katika kujibu kidogo tu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza, nianze na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Hamza Hassan Juma ambao walipenda wajue namna gani tumejipanga tuna mkakati gani katika kuviendeleza visima hivi vya *Ras-el-Khaimah*. Mhe. Naibu Spika, Baraza hili litakuwa shahidi hatua mbali mbali ambazo tumezichukua pamoja na juhudi zao wenyewe ambazo zimo ndani ya Baraza hili katika kuona namna gani tunahakikisha kwamba visima hivi tunaweza kuviunga na vifanye kazi.

Lakini, shukrani za pekee katika hili naomba nizitoke kwa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza lako hili tukufu, kwamba mkakati maalumu tuliopanga ndani ya Baraza hili, kuhakikisha kwamba katika bajeti ya mwaka huu tunayokwenda nayo basi visima hivi tunaanza kuviwekea mpango na kuviwekea fedha ili tuweze kuviendeleza. Na nawashukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa kukubaliana na hilo na Kamati ambayo pia imeongozwa na Makamu wa Pili wa Rais , Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.

Naomba niseme kwamba jumla ya visima 32 tayari vishaungwa katika visima vya *Ras-el-Khaimah* ambavyo vinafanya kazi na viwili viko katika hatua ya mwisho ambavyo vitakuwa 34 na katika bajeti ya mwaka huu jumla ya shilingi bilioni 4 zimepangwa kuendeleza visima hivyo. Kwa hivyo, ni hatua kubwa na kila mwaka tunapokwenda basi bajeti naamini itaendelea kuwa *considered* ili visima hivyo viweze kuendelea.

Vile vile niseme Mhe. Ali Suleiman Ali nae aliuliza hatua gani zinachukuliwa katika wale wanaiharibu vile vianzio vya maji. Naomba niseme kwamba hatua mbali mbali zinachukuliwa kwa kuweza kutoa elimu kwa wananchi wetu kukaa nao, pia kuwatumia masheha na viongozi mbali mbali ndani ya Kamati za Sheha basi kuhakikisha kwamba wananchi wale wanapewa taaluma ili wasiendelee kufanya uharibifu. Lakini pale tunapowapata wale ambao wanafanya ule uharibifu wa moja kwa moja basi hatua za kisheria pia zinachukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna swali ambalo limejitokeza la kusema kwamba Mhe. Hamza aliuliza katika utafiti huu wa mafuta na gesi asilia je, Fungu Mbaraka limekuwa *considered*? Sasa naomba niseme kwamba kwa hatua ya awali kwa sasa hivi tunafanya kazi utafiti umo katika lile *block* kitalu cha Pemba Zanzibar *block* ambayo katika haya maeneo mengine bado utafiti haujaanza. Kwa hivyo, naomba hili nilichukue na tatalizingatia pale wakati ukifika utafiti ukifanywa katika maeneo hayo husika. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka kujua kwamba katika huu mpango wa eneo la Mangapwani kuna mkakati gani ya kuwalipa wananchi fidia. Kwa kweli kuna mkakati mzuri na madhubuti ambao umepangwa na serikali umeuridhia kwa kuhakikisha kila mwananchi atakaeguswa katika eneo lile basi ataweza kulipwa fidia yake bila ya tatizo lolote .

Lakini Mhe. Mohamed Said Mohamed nae pia alitaka kujua utafiti huo uliofanywa kuna mkataba wowote baina ya hao wanaofanya utafiti na serikali? Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mkataba hakuna, isipokuwa kuna makubaliano baina ya serikali mbili Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar na Serikali ya *Ras-el-Khaimah*, katika makubaliano hayo basi tumekubaliana waendeleee kufanya utafiti kwa harama zao na serikali ili iweze kupata vile vitu muhimu ambazo tunaita ni *data* ambazo tutaweza kujua kama kuna mafuta au hakuna.

Mhe. Naibu Spika, *Ras-el-Khaimah* wamechukua jukuma kubwa la kuhakikisha kwamba kazi hii itafanyika kwa usahihi na kwa umakini sana. Vile vile aliulizia swali la kiwango cha maji, maji yapatikana kwa kiwango gani hapa Zanzibar. Naomba niseme kwamba katika mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kwa sasa hivi katika maeneo ya Pemba mjini asilimia 95 ya maji yanapatikana na tumesema ifikapo mwaka 2020 kwa upande wa Pemba asilimia 100 itakuwa imefikiwa. *(Makofi)*

Lakini kwa upande wa Unguja tumesema kwamba kwa mijini asilimia 90 na tunatarajia ifikapo 2020 basi itafikia asilimia 97. Na vijijini pia kwa upande wa Pemba ni asilimia 80 na *target* ni asilimia 85 na asilimia 80 hii ni kwa Unguja na Pemba.

Kwa hivyo, naomba nitoe ufafanuzi huo ili wananchi wapate kusikia, lakini na Wajumbe wa Baraza lako tukufu waweze kujua. Serikali katika dhamira yake ile ile ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama, basi mkakati maalum upo na kazi kubwa inafanyika na naomba pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa mashirikiano yao katika kuhakikisha suali la maji katika kila eneo linafika.

Baada ya hayo naomba nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika kuendelea kuunga mkono hoja kwa asilimia 100 na kukahikisha kwamba bajeti hii inapita na tutazifanyia kazi ipasavyo ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, mchangiaji wetu anaefuata ni Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, baada ya hapo atafuata Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia hutuba ya Makamu wa Pili wa Rais aliyoitoa jana, na nimeona nisimame nichangie hutuba hiyo kwa sababu wizara yetu imaguswa na baadhi ya mambo ambayo ningependa kuyatolea ufafanuzi.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa pia ningependa niwashukuru wachangiaji wote waliochangia kuhusu masuala haya na hasa wale waliogusia sehemu yangu ambayo ninayoisimamia, ili waweze kujua ukweli wa mambo ukoje. Nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar pia kwa kunipa fursa hii ya kuisimamia wizara hii yenye changamoto nyingi, lakini aliniamini kwamba ninaweza kuzisimamia na ninamuahidi kwamba nitazisimamia na zitaondoka.

Mhe. Naibu Spika, nikianza ninachotaka kukizungumza kimegawika katika mafungu ya watu mbali mbali kwa mada mbali mbali, ningependa nianze na fungu la kwanza ambalo linazungumzia suala la ujenzi wa barabara, waliozungumzia ujenzi wa barabara walikuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Hawa wamezungumzia suala la barabara.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa barabara uko katika mafungu matatu, fungu la kwanza ambalo ni kubwa liko chini ya wizara hii ambayo mimi naisimamia. Kwa hivyo, zile barabara kubwa zote za nchi hizo ndio ziko chini wizara yangu. Halafu kuna *group* la pili la barabara ambazo ziko chini Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum. Halafu kuna barabara ndogo ndogo ambazo zinakwenda katika maeneo yanayozalisha ambazo zilitengenezwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, hizo wanaziita *feeder roads,* kwa sababu ni zile ambazo zitaweza kutoa mazao mashambani na kwenda katika barabara kuu ili ziweze kufikishwa katika soko, huo ndio utaratibu wa barabara.

Lakini kwa kuwa wizara yangu ndio inayosimamia barabara, kwa hivyo yale yote yanayohusiana na barabara yanafikishwa kwetu, halafu sisi tunaangalia lipi linatakiwa liwe mwanzo. Kwa mfano, kama tunataka barabara kubwa ndio zilizozungumzwa, basi hizo Mhe. Naibu Spika, ndizo tunazofanyia kazi na mifano ipo mingi tu, kwamba barabara hizi. Kwa mfano wa sasa hivi, tukizungumzia suala la Kibonde Mzungu, barabara hii inayotoka Fuoni kwenda Tunguu. Tukizungumzia barabara nyengine zote ambazo tunazijua kwamba hizi ni kubwa, zinazoelekea katika wilaya na mikoa mbali mbali, zile ziko chini ya wizara yetu na hizo huwa tunazisimamia, tunazifanyia makisio, tunatoa-*contract,* kwa sababu sisi kama sisi kuzihudumia hizi zitachukua muda na zinachukua fedha nyingi na vifaa vingi ambavyo huwa sisi hatunavyo. Kwa hivyo, tunatoa *contract,* kwa wale wanaoshinda wanakwenda wanafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, lakini tukija barabara za vijijini tunaohusika ni mimi tunaohusika na ujenzi wa barabara na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo iko chini ya Mhe. Haji Omar Kheir na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ambao nao wana barabara. Wizara hizi huwa tunakaa kwa pamoja, kwa sababu sisi lazima tutowe usaidizi kwao, sisi lazima tutowe viongozi na wataalamu kutoka kwenye wizara yetu na wao wachangie kulingana na halmashauri zao. Lakini na wao pia wachangie kutokana na wizara zao. Kwa hivyo, barabara hizi zinafanyiwa kazi kwa pamoja katika wizara hizi tatu, na tunatakiwa tuwashirikishe wabunge na wawakilishi wa maeneo husika ambako barabara zile zinapita. Kwa hivyo, kuna kamati maalum ambayo tumeambiwa tuiunde ili iweze kuwa na hao niliowataja tuzishughulikie barabara hizi za vijijini. Naamini kwa umoja wetu tukichangia hili basi barabara hizi zitamaliza. (*Makofi*)

Lakini wakati huo huo na hizo barabara za kilimo ambazo zinatoa mazao, nazo pia ziko katika utaratibu huo huo, kwa hivyo tutachanganya kwa pamoja haya. Katika barabara hizi kuna barabara zilizotolewa ilani, kuna barabara zilizotolewa ahadi, kuna barabara ambazo wizara imezipanga. Katika utaratibu huu tuna imani tukishikana pamoja na kwa makisio ambayo mara nyingi hatukosi kupewa, isipokuwa kila mwaka tunazidishiwa, basi tuna imani tunaweza tukafika asilimia kubwa wakati wa mwaka 2020 pengine kunako asilimia 90 *plus*. Kwa hivyo, itakayotokea kwa bahati mbaya haikutengenea, lakini sio matumaini yangu kwamba hilo nataka litokee, bali itakuwa ni bahati mbaya.
Mhe. Naibu Spika, katika ujenzi wa barabara tumeambiwa tuzingatie ubora wa barabara. Mhe. Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba ujenzi wa barabara ubora wake unazingatiwa, isipokuwa kuna baadhi ya mambo ambayo yanafanya barabara zile zinakuwa na matatizo. Barabara zinazeeka, barabara zikizeeka zinakuwa na matatizo. Lakini barabara ukitaka iwe na umadhubuti basi barabara ile inatakiwa pembeni iwe na misingi, ili maji yasikae, tatizo la barabara zetu hazina misingi, kwa hivyo sehemu nyingi maji yanakaa. Hakuna kitu kibaya kwa barabara kama maji, maji yanaozesha barabara na huwa zinachimbuka. Kwa hivyo, katika maeneo mengi ambayo maji yanatuama utakuta kuna mashimo makubwa pembezoni barabara zimemong'onyoka. Lakini mvua zikinyesha kila wakati mambo haya yanatokea.

Sasa wakati mvua zinanyesha huwezi ukafanya hiyo kazi, inabidi usubiri mvua zikimalizika tuanze kufanya makisio, tuanze kuangalia wapi kumeathirika ili tuanze. Lakini kwa mfano mwaka huu mvua ni nyingi kwa kipindi hiki, kwa hivyo hatuwezi kwenda kutia vifusi saa hizi wakati kesho mvua inanyesha na usiku inanyesha, ina maana tutakuwa tunatwanga maji ndani ya kinu. Lazima tuhakikishe kwa kusikiliza hali ya hewa tukijua kwamba sasa mvua zimepungua kiasi cha kutosha, hapo tutaanza kupita kuzifanyia matengenezo barabara zetu.

Vile vile kuhusu suala la barabara, kuna barabara ambazo sasa hivi zimeshapewa *contract*. Kwa mfano, barabara inayotoka Bububu kwenda Mkokotoni, vile vile tumeambiwa kwamba tujenge maeneo yale misingi wa kutoa maji kupeleka pwani. Mfano, barabara ya Kiembesamaki, *contract* imeshatolewa kinachosubiriwa kila kitu kimeshakamilika, isipokuwa hatuwezi kufanya kazi kwa kipindi hiki wakati mvua zinanyesha. Lakini Kibonde Mzungu, Kiembesamaki misingi ya kupeleka maji pwani hivyo vyote vimeshatolewa *contract* na mara tu mvua zitakapomalizika kazi hizo zitafanywa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika barabara hiyo ambayo inakwenda Mkokotoni kuna madaraja yasiyopungua saba. Mhe. Hidaya Ali Makame alizungumza kuhusu madaraja hayo, barabara ile nayo inajengwa itapanuliwa iwe barabara kubwa na madaraja yale yote yatajengwa ili yaweze kupitisha gari mbili kwa wakati mmoja. Kwa hivyo, ajali zinazotokea pale tunategemea kwamba sasa zitapungua, ibakie tu uzembe wa wale ambao wanapita kwenye barabara, lakini itakuwa barabara sio tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningependa nizungumzie suala jengine linalohusu mkonga wa taifa nalo hilo limetajwa katika *speech* ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Suala hili limezungumzwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed maarufu Dimwa. Mkonga wa taifa umeulizwa kama unafanyakazi upo kweli.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimtowe wasi wasi kwamba mkonga wa taifa wa Zanzibar upo na karibu wizara zote zimeunganishwa na kazi inafanywa. Tuna vituo kama Nungwi kuna kituo cha mkonga, Masingini, Jamhuri *Garden*, Mazizini, Fumba, Matemwe, Paje na Kizimkazi. Hivyo ndivyo vituo vya mkonga wa taifa ambavyo vinaufanya mkonga huu uweze kufanyakazi. Katika vituo hivyo vimezunguka katika visiwa vyote vya Unguja na Pemba pia, kwa sababu Pemba nako kuna vituo ambavyo vimezunguka Pemba ambavyo vinaunganisha mtandao.

Mhe. Naibu Spika, kwenye mtandao huu unafanyakazi mbili kubwa. Kampuni ya *Zantel* inatumia mtandao huo na ndio kampuni kubwa inayotumika Zanzibar. Kwa hivyo, tukiona tunapata simu tujue kwamba mkonga huo ndio unaofanyakazi, ingawa kuna baadhi ya sehemu mawasiliano yanakuwa hafifu na sehemu hizo zinajulikana na tayari zimeanza kufanyiwa kazi, ili kuhakikisha kwamba kila mtu aweze kupata mawasiliano.

Vile vile, mkonga unafanyakazi kwa upande wa mawasiliano ya redio na televisheni *ZBC* wanatumia mkonga huo na nafikiri *ZBC* inafanyakazi nzuri. Kwa hivyo, hizo ndio sehemu mbili kubwa ambazo sasa zimeanza kufanyakazi, lakini na maofisi yote ya serikali yameunganishwa na mkonga huu. Kwa hiyo, hizo ndio kazi ambazo zinafanyika. Ofisi zote ukichukua Pemba na Unguja kuna ofisi 105 ambazo zimeunganishwa, na taasisi yoyote ile ya serikali ikiomba kuunganishwa na mkonga basi hakuna tatizo wanapewa makisio na wanaunganishwa. Kwa hivyo, mkonga unafanyakazi kama ambavyo ulipaswa kufanya.

Mwisho nizungumzie masuala ya uwanja wa ndege wa Pemba. Hili ni suala ambalo serikali imelifanyia kazi kwa ukamilifu wake, michoro imeshatizamwa, maeneo yameshapimwa, tunajua wapi tunatakiwa uwanja ufike na utakuwa ni uwanja mkubwa wa kimataifa. Sasa hivi ndege zinatua kwa dharura wakati wa usiku, lakini haimaanishi kwamba ikitakiwa ituwe usiku haitotua, ndege za dharura zinakwenda. Lakini baadae baada ya haya mabadiliko kule ndege zitatua usiku na mchana na ndege za ukubwa wa *Boeing 37* nazo pia zitatua kutoka maeneo yote ambayo ndege zinazokuja Unguja wakitaka kwenda Pemba wataweza kutua. Kwa hivyo, hilo halina wasi wasi.

Mhe. Naibu Spika, uwanja wa ndege kwa sasa hivi taa zinawashwa kwa majaribio asubuhi na jioni ili kuhakikisha kwamba zinafanyakazi na pale inapotokea dharura taa zinawashwa na ndege inatua hata kama ni saa sita usiku. Kwa hivyo, nawataka niwape afuweni Mhe. Suleiman Sarahani Said na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, kwamba uwanja wa ndege unafanya kazi

vizuri, isipokuwa tu hakuna ile dharura iliyotokea kwa ndege zetu za kawaida zote zinatua mchana ndio maana unatumika mchana. Lakini hayo yakisha basi nafikiri ndege zitaweza kutua mpaka usiku hasa zile zinazotoka nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri hayo ndio masuala yalikuwa yananihusu na nimeweza kuyatolea ufafanuzi, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba ambao watasimama kuzungumza, nafikiri kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe huwa wanaweka vitabu, kwa sababu nimepata vi-*note* vingi kwamba wajumbe hawasikii na hasa wazungumzaji wanapokuwa warefu hizi spika ziko chini kidogo, kwa hivyo inakuwa vigumu sana kusikia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nilikuwa naomba kama itawezekana wajumbe wawe wanafanya kama Mhe. Simai Mohammed Said nafikiri namuona na Mhe. Nadiri Abdul-latif Yussuf. Wajaribu kuweka vitabu ili tuweze kuwasikia vizuri. Nafikiri wale ambao wameniletea vi-*note* wajumbe wengi wanasema kwamba hawasikii vizuri. Mimi nilikuwa sisikii nilikuwa nafikiri tatizo liko kwangu, lakini baada ya kupata note nimejua kwamba sote tuna tatizo moja.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto. Mhe. Waziri karibu. Baada ya hapo atafuata Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kupata wasaa wa kuweza kuchangia na mimi.

Kwanza kwa heshima kabisa napenda nichukuwe nafasi hii ya pekee kumpongeza Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kazi nzuri anayoifanya kwa hekima, busara na upendo na kuendelea kutunza amani katika nchi yetu. *(Makofi)*

Aidha, nimpongeze pia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa ukakamavu na ujasiri anaofanya katika kuhakikisha kwamba masuala mengi ya serikali yanafanyiwa kazi na tunaendelea kuwa katika hali ya utulivu na ushirikiano, pamoja na mengine ambayo yanaendelea kuweza kutusaidia katika nchi yetu ya kuwa na moyo wa ushirikiano juu ya masuala mbali mbali ambayo yanatutokea katika maisha yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda niungane na wajumbe wenzangu wote waliosema maneno mengi ambayo yamezungumzwa hapa, yaliyochangiwa juu ya nchi yetu kuhusiana na masuala ya Muungano, nadhani yamefafanuliwa vya kutosha. Nipende kusema tu tuendelee kushirikiana, tofauti zinaweza kuendelea kuwepo, lakini bado masuala ya kuwepo pamoja ni muhimu na hasa ukiangalia kitabu chenyewe cha Mhe. Makamu wetu wa Pili wa Rais alichokileta hapa. Kuna viongozi wetu wakuu ambao wanasimamia masuala haya kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, ukiwaona kwenye picha hapa kuna Mhe. Samia Suluhu Hassan yuko pale, kuna Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mwenyewe yuko pale, Mhe. Mohammed Aboud

Mohammed yuko pale, kuna Mhe. Kassim Majaliwa yuko pale, kuna Mhe. Yussuf Makamba yuko pale. Lakini bado tuna wabunge wenzetu ambao wanatoka kwenye Baraza letu la Tano, ambao wanashiriki kikamilifu katika suala zima la masuala ya Bunge. Kwa hivyo, mimi naendelea kuamini kabisa masuala madogo ambayo yanaweza kutuhadharisha kuanza kupingana, yanaweza kufanyiwa kazi kama tulivyozowea kwamba tunaambizana ukweli hatufichani na tunaendelea na muungano wetu ambao ni mfano kwa dunia nzima.

Mhe. Naibu Spika, masuala mengi katika sehemu hii yamezungumzwa, mie ambayo yaliyonigusa ni yale ambayo yanafanya mambo ya udhalilishaji kwa watoto wanawake na pia wazee, suala hili limekuwa likishughulikiwa vizuri pia kwa wizara yetu, wizara ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, lakini pia kuna suala zima la dawa za kulevya. Vijana wetu wanaokamatwa ni wale ambao wamekwisha athirika, ambao wao hawajui hata hizi dawa zinatengenezwa wapi. Wanapotiwa kwenye masuala ya misukosuko wakifungwa wanakuwa wanaadhibiwa mara mbili.

Kwanza wanaadhibiwa kwa kujifunza kunywa madawa ya kulevya, mara ya pili ni kwamba anakwenda kupelekwa pahala ambapo anahitaji msaada ni mgonjwa tayari huyu, anapaswa aangaliwe na kuhurumiwa. Lakini mtu mbaya zaidi ni yule anaeagiza haya madawa kutoka nje kwa gharama na yanapita katika njia ambazo ziko wazi zinajulikana, na watu wanafahamika. Kwa hivyo, tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba tusiwaonee haya, kama wanajitajirisha wanajitajirisha wao wenyewe na familia zao, lakini wanaoumia zaidi ni sisi na watoto wetu ambao tunaendelea kukaa nao na hawa ndio viongozi wa kesho ambao tunawahitaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo tusiposhirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunapiga vita kwa pamoja hili suala zima la uuzaji wa madawa ya kulevya katika maeneo mbali mbali tunajiangamiza. Nadhani pia ni suala zima ambalo linaharibu kabisa *DNA* ya Kizanzibari, vinasaba vya Kizanzibari. Wazanzibari kwa asili wamekuwa wakisifika duniani kote kwamba ni watu watulivu, wanaopenda kumcha Mwenyezi Mungu, watu wenye upendo na ushirikiano, lakini inapofika kwenye masuala ya namna hii, tunapoteza yale masuala kwa sababu utashi unapungua. Kwa hivyo, naomba tushirikiane katika kuhakikisha kwamba tunayakemea na kuhakikisha kwamba taifa letu linashikana kwa pamoja, kutoruhusu na kuwaonea aibu wale watu ambao wanaingiza madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, nimesimama hasa kwa makusudi ya kuunga mkono hii hotuba, lakini pia kujibu swali ambalo Mhe. Ali Suleiman Ali wa Jimbo la Kijitoupele, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, ambae ameuliza na kutaka kujua suala hili. Amesema hivi kumekuweko na kuendelea na vitendo vya udhalilishaji hivi karibuni katika jimbo lake. Muhudumu wa ndani aliyemuiba mtoto lakini alikamatwa hata hivyo kuna mtoto yuko *Form One* kapotea na hadi hivi sasa hajaonekana, mtuhumiwa alipatikana lakini alitoweka katika Kituo cha Polisi.

Mhe. Naibu Spika, nataka kusema tu kwamba haya ni masuala ambayo tunahitaji sana ushirikiano wa karibu na hawa watendaji wakuu ambao tunawatumainia wa kutunza amani, mikononi mwa Polisi kupotea kwanza ni kitu ambacho hakipendezi na pia inakuwa ni aibu, ni kitu ambacho tuna kikemea kabisa, kwamba kama kuna suala la namna hii halipendezi. Watu

ambao tunawatumainia watulinde halafu mtu anapotea mikononi mwao, na huyu inasemekana amepotea akiwa na pingu mikononi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba kwanza suala lenyewe lilivyokuwa linasemwa, naomba nilisome ili niweze kujibu vizuri. Kwanza suala la kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji ni changamoto na jukumu la sisi sote kushiriki katika kupiga vita udhalilishaji. Bado wizara yangu na wadau wengine tunaendelea na jitihada ya kupambana na matukio haya, na niwaombe na Waheshimiwa Wawakilishi kuendelea kuunga mkono kwa kutoa taaluma, kuepuka na kupinga udhalilishaji lakini pia kufanya ufuatiliaji katika majimbo yetu. Kwenye majimbo yetu tunawafahamu watu ambao tunaishi nao, wenye tabia mbaya tunawaelewa lakini pia tunakuwa karibu nao zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mtoto aliyeibiwa. Kwanza kabisa wizara ninayoiongoza inapenda kuchukua fursa hii ya kulaani tukio la kuchukuliwa kwa watoto kwa njia ya utekaji, wizi au hadaa. Taarifa tulizokuwa nazo ni kwamba muhudumu huyu ameshakamatwa na jeshi la polisi, mtoto alipatikana na alikabidhiwa kwa wazazi wake kwa kuendelea na uangalizi na matunzo kwa ujumla. Polisi inamshikilia mtuhumiwa na hatua za kisheria zinaendelea kufanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, napenda nitowe wito kwa mara nyengine, nilishawahi kusema hapa mahala na nimesema sana kwenye vyombo vya habari sasa hivi hakuna sababu ya kumuaminni mtu yoyote, kwa mtoto wa kike na kiume hakuna wa kumuamini hata baba yako mzazi, ukikaa nae kwenye sehemu ya siri. Mama yako ambae sio wa karibu na wewe sio wa kumuamini kwa sababu watu wamebadilika hata hatuelewi ni kitu gani kimeingia kaka ndugu yako si wakike na wala si wakiume nikuwa na tahadhari.

Lakini pia kuhusu la mtoto huyu wa *Form I*, kwa mujibu ni kwamba kweli tukio hilo limetokea kutoroshwa baada ya kuombwa na jirani yake ambae ni mtuhumiwa anaejulikana kwa jina la Amour ambae siku husika alimuomba mtoto kumsaidia kuhama nyumba na kuhamia nyumba nyengine na ndipo alipoondoka nae, ni kweli mtuhumiwa huyu alikamatwa lakini alifanikiwa kutoroka kituo cha Polisi akiwa na pingu, kama nilivyosema kwamba ni aibu Polisi wanaendelea kumtafuta yeye na ambae mpaka hivi sasa hajulikani alipo. Naomba jamii na washirika wengine wowote wenye taarifa kuhusu mtuhumiwa na mtoto huyu atoe taarifa kwa vyombo vya sheria. Aidha, mtuhumiwa huyu amekuwa na *recod* ya kufanya matukio kama hayo kwa maeneo kwa maeneo mengine na kukimbia.

Mhe. Naibu Spika, bado niombe jamii kushirikiana na kuomba kila aina ya msaada na ushauri ili kuepusha matukio kama hayo katika nchi yetu yasitokee, kwa sababu kama mtuhumiwa angekuwa alipigwa picha katika matukio ya awali, nadhani mnakumbuka jinsi gani picha zilitusaidia huko nyuma alipotokea kijana aliyefanya uhalifu akataka kupotea, lakini tulipotumia picha kumrusha kila pahala haikuchukua siku 3, nawewe Mhe. Naibu ulishiriki kikamilifu tulipkwenda Makunduchi.

Sasa tunaomba kabisa tunapokuwa na watu ambao ni wageni picha ni muhimu kuwa nazo, maana mshichana anapokuja kwenye nafasi ya kufanyakazi ndani ya nyumba usimkubali kwa kuwa unadhiki ya kwamba ni mwache mtoto awe chini ya mikono. Kwa hiyo, kuwe na mikataba na utaratibu mtuilishe kwa sheha anatoka wapi na kuwajuilisha watu wanaohusika ndio

umuachie mtoto lakini pia kupiga picha itakakapotokezea tatizo la aina yoyote kum-*tress* inakuwa rahisi.

Mhe. Naibu Spika, tungekuwa na picha ya kijana huyu sasahivi tungekwisha mpata nawaomba watendaji wa Jeshi la Polisi kuwa makini katika kutekeleza majukumu yao hususan hili la kutoroka kwa mtuhumiwa ambae alishakuwa chini ya himaya yao, hilo ni lisilo aminika na kwa hili tunasisitiza jitihada madhubuti zichukuliwe mapema iwezekanavyo mtoto apatikane na mtuhumiwa achukuliwe hatua stahiki, ili kukomesha matukio kama haya yanayoharibu ustawi wa taifa letu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jambo hili linasikitisha na nadhani mzazi atakuwa na fadhaa kubwa sana lakini naendelea tena kutoa mifano ya matukio haya ni zaidi ya saba mpaka sasa hivi yaliyotokea katika nchi yetu, mengine tunashindwa hata kuyasema kwasababu tunaendelea kufanya kazi kuhakikisha kwamba tunawapata watuhumiwa kabla ya hawajatoroka. Wengine tukiwatangaza tu wanakuwa njia moja wapo ya kuweza kutukimbia.

Mhe. Naibu Spika, la Mhe. Tatu Mohammed Ussi mchango wake alitaka hatua zaidi zinazopaswa kuchuliwa kwa udhalilishaji, Mhe. Tatu Mohammed Ussi napenda niseme tu nakushukuru kwam mchango wako na napenda kusema wizara yetu inapokea na itaendelea kufanyakazi kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema haya machache naomba niunge mkono hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na pia nimpongeze sana mtendaji mwenzangu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed ambae mara nyingi ana kaimu wizara yangu kwakuwa karibu sana tunapofanya kazi kwa pamoja na kwa kweli anatetea sana masuala ya udhalilishaji kama yeye mwenyewe anaweza kumalizia ni baba mwema wa mfano, kwa sababu baba mwema wa mfano anatetea yeye hajali kwamba ni mwamme jambo la mwanamke na watoto linakuwa kwake. Nawawakieni wote muwe mababa wema Wawakilishi, na muwe walinzi katika familia zenu. Nawatakieni kila la kheir . Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Waziri wa Afya na baada ya hapo atachagia Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba namimi niungane na wenzangu kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, pili kukushukuru wewe na tatu kumshukuru sana Makamu wa Pili wa Rais jembe, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Waziri wa Nchi katika Ofisi yake Mhe. Mohammed Aboud na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kuratibu shughuli zetu na Mhe. Mohammed Aboud ndio mnadhimu hapa, kwa kushughulikia mambo yetu yote ya Baraza anafanyakazi kubwa sana nataka nipongeze sana kwa kazi nzuri anayofanya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pili katika wachangiaji waliochangia hutuba ya Makamo wa Pili wa Rais walikusia mambo 3 makubwa kwa Wizara ya Afya na moja ni suala zima la ugonjwa wa Ini, inaonekana kama umeongezeka sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwa mujibu wa takwimu tulizonazo baada ya serikali kubaini kwamba tatizo hili limejitokeza tukaunda kitengo ndani ya kitengo kinachoghulikia kifua kikuu UKIMWI

pamoja na ukoma hali sasa imedhibiwa vizuri. Katika hotuba yetu tutakayowasilisha tutaoa data za kuonesha ni kiasi gani matatizo haya yamedhibitiwa, na hasa kwa upande Pemba, hali ni nzuri zaidi Unguja asilimia yake si nzuri sana, lakini juhudi zinaendelea kuweza kulitatua jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, la pili ni suala la miundombinu rafiki kwa ajili ya vituo vya afya ukiangalia sasa hivi Mhe. Naibu Spika, vituo vingi vya afya vimewekwa miundombinu ili ndugu zetu ambao wanamatatizo ya ulemavu waweze kupita bila ya matatizo pale ambapo bado kunakasoro serikali ama kupitia Wizara ya Afya au Tawala za Mikoa tutakuwa tayari kurekebisha kasoro hizo ili kuhakikisha kabisa vijana wetu na ndugu zetu wanapata matibabu bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, la tatu ambalo limezungumzwa sana na wajumbe na wananchi wangependa sana kusikia ni suala la maradhi haya yaliyoingia ya homa ya kichun'gunya, lakini niseme kwamba kwa upande wa serikali tumejipanga vizuri sana. Kwanza kushughulikia na ndio maana mpaka leo pamoja na kwamba kuna wagonjwa wasiopungua 1,000 lakini hakuna mtu aliepoteza maisha hata mmoja, hili ni jambo kwanza la neema.

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili serikali tumejipanga vizuri sana kuanzia Jumatatu ijayo tukijaaliwa kutoa taarifa rasmi ama kupitia vyombo vya habari au Baraza la Wawakilishi itategemea mwenye nchi tulomkabidhi ataamua tutumie utaratibu upi wa kuwapasa wananchi habari kamilifu lakini nataka niwatoe wananchi wasi wasi kwamba hakuna mtu yoyote alopoteza maisha.

Lakini la pili matibabu yake ni ya rahisi na ndio maana ndugu zangu Waganga wa kienyeji anamuandikia mtu kombe anakunywa na anapona, kwasabau ugonjwa wenyewe kwa kweli unapoteza nguvu kidogo, unapata *temperature* wakati mwengine ni homa lakini sio ugonjwa kama malaria au kipindupindu ni homa ambayo inatibika na ndio maana pamoja na idadi hii iliyopo basi bahati nzuri hakuna maafa yaliyotoke kwamaana ya vifo ukiacha wasi wasi uliowaingia wananchi, na kwa hili nasema tusubiri mpaka Jumatatu tukijaaliwa serikali itakuwa imetoa taarifa rasmi ili wananchi waweze kuelewa tutaelezea hatua tunazochukua taaluma tunayoitowa na namna gani wananchi waweze kuchukua tahadhari.

Jambo lilitokea kubwa ni kwasababu ni wakati wa mvua na wakati wa mvua bahati mbaya mbu wanazaliana ndio hasa tatizo lililotokea, lakini lilipotokea mara ya kwanza pale mjini lilikuwa rahisi sana ku-*control* siku moja tumefukiza madawa na ukaondoka, lakini huku kuna tatizo kidogo la mvua ndio maana kidogo umechukua muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwatoe wasiwasi wananchi wote na serikali itatoa kauli nzuri tu ya kuona namna gani tunakabiliana na hali hii ambapo kuna mvua na namna gani tunaweza kukabiliana na tatizo hili la awamu.

Mhe. Naibu Spika, namimi naomba niungane na wenzangu kuznugumzia kidogo suala hili la muungano. Nataka nimshukuru sana Mhe. Balozi na Waziri wa Viwanda na Biashara wamekutukumbusha historia.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 1961 tarehe 9 Disemba ilipatikana Serikali ya Tanganyika kupitia kwa kura, tarehe 12 Januari 1964 tulipata Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mapinduzi. Kwanza niseme kuna baadhi ya viongozi wanaziona siku hizi 2 kama ni za kawaida, wanazipuuza puuza wapo sasahivi na hizi ndizo zilizozaa tarehe 26 Apili, Muungano kama havikutokea vitu hivi 2 kusingetokea Muungano wa tarehe 26 Aprili. *(Makofi)*

Kwa hivyo, lazima kwanza tuheshimu siku ya uhuru wa ndugu zetu, lakini watu waheshimu mapinduzi yaliyopatikana mwaka 1964, hatukupata kwa karatasi tu, tulipata kwa damu, haikuwa kazi rahisi tulijaribu kwa karatasi ikashindikana tukasema njia peke yake ilobaki ni kuondoa utawala huu kwa mabavu na tukafanya. Na wale wanaodai kuapishwa apishwa kila siku wajaribu watizame kama wataweza. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo 1967 tukaja na Katiba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila Rais, kila Makamu wa Rais, kila Mbunge anakula kiapo kwa imani yake ya kidini na kukamata Katiba na ndani ya Katiba ile Sura ya 8 inazungumiziwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar uwepo wake, uwepo wa Rais, uwepo wa Baraza la Wawakilishi. Sura ya 7 kuna kifungu cha mgawanyo wa mapato ya Mfuko wa Pamoja wa Muungano, na hapa ndio penye tatizo sote tumekama katiba kula kiapo. Tunahitaji kutembea na katiba, akinyanyuka Mhe. Mbunge au Mhe. Mwakilishi yeyote akienda kinyume na katiba aliokulia kiapo, hafai kubaki ndani ya nyumba hiyo. Mimi namtaja Mhe. Ally Kessy kwa sababu nimekutana nae sana.
Mhe. Naibu Spika, nililieleza hili katika Bunge la Katiba na nataka nilirudie hatukuungana kwa vitu tuliuungana kwa uhai wa watu, wengine walipa kura, wengine tukafanya mapinduzi tukaamua kujenga umoja wa Afrika tukaanzia kwa nchi. Kama ni vitu Zanzibar tumetoa vingi wengine hamfahamu hapa, Waziri Amina amesema kidogo sana.

Mhe. Naibu Spika, Afrika ya Mashariki ilipokuwepo Jumuiya ya Afrika Mashariki Zanzibar tulikuwa na nafasi sawa Tanzania Bara kama tungeingia kwa utaratibu ule tuliokuwa nao na ndani ya Muungano tungekuwa na wabunge 9 leo, tungekuwa na nafasi ya kugombea kwenye uongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tume-*sacrified* tumeacha nafasi. Tena marehemu Mhe. Ngombale Mwiru nimemwambia sie hatutumii akili tungepata nafasi 9 huku na 9 huku 18 tunge-*control East Africa Communities.* Niko katika *bank* tumeikopesha Bara million 15 *dollar* wakati wanashida. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hatukuungana kwa vitu. Mzee Jumbe kaingia hapa katoa majenereta zaidi ya nane kupeleka Bara wakati wanashida ya umeme. Tulikuwa na *Mega* 27 tumezinunua sisi hapa tukaendanazo Kagera kwenye mapambano. Hatukuzungumzia vitu, amekuja na siasa ya kuzungumzia vitu katika watu waliopoteza maisha yao, waliopoteza nguvu zao, hawajui historia ya Muungano wala hawajui madhumuni ya kuwepo kwa Muungano, hawafai kubaki ndani ya vyama vyetu vya siasa watoweni, watatupotezea muda sana. *(Makofi)*

Leo tumefika miaka 52 tumebaki na Muungano wetu. Wako maadui wengi wanafikiri kwamba hauwezi kudumu na sisi miongoni mwetu tunaungana nao katika kufanya hilo tusikubali hata kidogo katika hili. Lakini lazima sisi wenye vyama vya siasa tuwaambie wanachama wetu wajumbe wetu ambao hawakubaliani na katiba ile wanayoilia kiapo watoke.

Mhe. Naibu Spika, ombi langu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akasimamie Mfuko wa Pamoja wa Muungano. Amekula kiapo kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wabunge wamekula kiapo kusimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndani yake mule tumeunda Tume ya Pamoja na Fedha mpaka leo haijafanyakazi ni ya kikatiba. Hili ni moja katika tatizo la Muungano ambalo liko ndani ya katiba na lazima litatuliwe na kama halitatatuliwe basi maneno ya kijingajinga haya yataendelea kuwepo.

Kwa hivyo, nawaomba sana natakiwa nimpongeze sana Mhe. Hamza Hassan, kwamba kuna haja ya wabunge na wawakilishi wa CCM mkakae ili mulizungumze hili, ni la kikatiba na wala sio la hiyari na sheria imeshapitishwa na tume ipo. *Fomula* Zanzibar wameshaikubali, imeshapita na imebakia upande wa pili hawajairidhia mpaka leo, tulimalize hili tatizo Mhe. Naibu Spika, tusione haya. Tukiona haya tutaanza kutafutana bure bila ya sababu. *(Makofi)*

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, hawa wenzetu kina Mhe. Ally Kessy hawaelewi kwamba sisi hatuzungumzii vitu, tunazungumzia uhai wa nchi yetu, uhai wa taifa letu na Umoja wa Afrika hatuwezi kuendelea nao. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya. Waheshimiwa Wajumbe, mchangiaji wetu anayefuata atakuwa ni Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Baadaye atafuata Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Naibu Waziri, karibu.

Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi hii kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sambamba na kutoa maelezo ya ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimeibuliwa kutoka kwa baadhi ya wajumbe, kwa namna ambavyo mapendekezo ya bajeti yameweza kuwasilishwa kwao.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza na hoja moja moja, lakini nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuendana na muda ili sote tuweze kufanikisha jambo hili kwa wakati. Kabla sijaanza naomba tuishukuru sana kamati na Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Omar Seif Abeid, Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu, kwa miongozo yao na ushauri wao ambao wameutoa kwa kupitia ripoti yao ya kamati. Tumeipokea na tutaendelea kuzingatia kadiri ambavyo tutakuwa tukisimamia Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, nitaenda moja kwa moja kuanza na hoja ambayo imetolewa na Mhe. Shehe Hamad Mattar kuhusiana na ujenzi wa nyumba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba. Ni kweli kama alivyosema, mpaka sasa tumetumia jumla ya shilingi milioni 13.5. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 serikali iliidhinisha kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza nyumba ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Pili Pemba. Lakini mpaka hivi sasa tumetumia jumla ya shilingi milioni 13. 5.

Mhe. Naibu Spika, sababu iliyotufanya tutumie pesa hizi mpaka sasa ilikuwa ni taratibu za kijenzi na majenzi na kufanya taratibu zote za serikali ili kufanya ujenzi wetu tujenge kitu ambacho kitakuwa imara, chenye kudumu na endelevu lakini pia kwa gharama ambazo zitakuwa zenye kutizamika. Kwa maana hiyo taratibu za *tender*, lakini pia kumtafuta mshauri kidogo vilichukua muda, lakini mpaka sasa tunasema kwa hatua ilifikia tayari hata ukitizama nyuma ya

kitabu chetu utamuona Katibu Mkuu akisaini na mjenzi amepatikana ambaye atakuwa na Vikosi vyetu vya KMKM, na tunafanya hivi kwa kuendeleza mahusiano mazuri ili kuhakikisha wenzetu nao waweze kuonekana na kuthamini kazi za ujenzi ambazo wamekuwa wakifanya ndani ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu hawa tumeshaingia nao mkataba na tayari hatua iliyokuwepo sasa ni ofisi tunafanya maombi ya *DCU* ili sasa kwenda kuwakabidhi *site* na ujenzi, ili hali hii ipate kwenda kwa haraka.

Tunamuhakikishia tu Mhe. Mjumbe, sambamba na Waheshimiwa wengine kwamba katika kipindi hiki tunaamini sasa tutakwenda *speed* hatutokuwa na jambao ambalo litaweza kutuzuwia, tunachoendelea kusubiri ni hali ya mvua kuweza kupungua ili wenzetu waweze kuhamia saiti kwa haraka.

Lakini hoja ya pili iliyotoka kwa Mhe. Shehe Hamad Mattar ilikuwa ni suala moja la kupungua kwa vyanzo mapato katika ofisi yetu ambayo ilikadiriwa pesa nyingi lakini imeonekana vyanzo hivi vimepungua. Ni kweli na tunakiri hilo lakini katika mwaka wa fedha 2017/18 wizara yetu ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi Milioni 32,521 katika chanzo kimoja kikuu cha mapato ambacho kipo katika Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ambapo katika maeneo ya Mwanakwerekwe tuna jumla ya milango minane, lakini pia kuna vifaa vya sherehe mashamiana pamoja na viti ambavyo kwa wakati mwingine huwa tunavitumia kama ni chanzo cha mapato lakini kama unavyoweza kufahamu Mhe. Naibu Spika, si wakati wote vitu hivi kuwa vinaweza kukodiwa na watu kulipa ili fedha hizi zikaweza kupatikana kwa wakati. Kuna wakati mahitaji ya viti kama hakuna ulazima huwa haviwezi kupatikana, kwa maana hiyo wasipotokea watu kwenda kukodi kile kima ambacho kimekadiriwa na wenzetu wa Wizara ya Fedha tunakuwa tunashindwa kukipata.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika kipindi hiki ambacho tumekisiwa kukusanya shilingi Milioni 32,521 kwa mgawanyo kama ufuatao, tulipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 23,151 elfu, kutokana na ukodishwaji wa vifaa, lakini jumla ya shilingi Milioni 9,360 elfu kwa ajili ya ukodishaji wa milango. Lakini hali halisi iliyokuwepo tumefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 5 ,850 elfu kwa ajili ya ukodishaji wa vifaa sambamba na jumla ya shilingi milioni 7,680 elfu kwa ajili ya ukodishaji wa milango.

Kwa hiyo, tulikuwa tunamuhakikishia tu kwamba huu ndo uhalisia uliokuwepo kama tunapata watu wengi wa kuja kukodi mashamiana na viti basi pia mfuko wetu utaweza kutuna na tunaamini mambo yetu yatakuwa vizuri na kile kima ambacho tutakuwa tumekisiwa na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango tutakuwa tumekipata kwa wakati. Kwa hivyo, tumtoe hofu tu haikuwa kusudio letu lakini hali halisi ya biashara inavyokwenda.

Mhe. Naibu Spika, pia ntakwenda katika Tume ya UKIMWI ambayo nayo bahati nzuri imepata wachangiaji wengi ntawataja kidogo kwa namna ambavyo wameweza kujua hoja zao, wapo Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Mohammed Said Mohammed,

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini na wengine wengi ambao wamechangia.

Kwa hiyo, nitajibu kwa pamoja maana kuna baadhi ya hoja zimekuwa zikisemwa na kila mmoja wao, Mhe. Machano Othman Said alizungumzia suala zima la mchanganuo wa fedha za programu za fedha za Utawala na Uendeshaji katika ofisi kati ya Unguja na Pemba. Kweli maelezo halisi ni kwamba progam ya Utawala na Uendeshaji ya Tume ya UKIMWI imepanga kutumia jumla ya shilingi Milioni 650,49 elfu kati ya hizo shilingi milioni 191, 640 na elfu 4 zimetengwa kwa ajili ya uratibu kwa masuala ya UKIMWI Pemba na jumla ya shilingi Milioni 459,445 elfu zimetengwa kwa ajili ya shughuli za Utawala Unguja. Mhe. Naibu Spika, huo ndio mchanganua halisi kwa namna ambavyo hoja ya Mhe. Mjumbe ilikuwa aliyoizungumza.

Vile vile, Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliuliza ni vipi dawa za kuzuia maambukizi ya VVU iliyozinduliwa hivi karibuni kwa upande wa Tanzania Bara, ni kweli wenzetu siku za karibuni wameweza kuzindua dawa kwa mujibu walivyosema kwamba kuzuia maambukizi ya UKIMWI, hata sisi dawa hiyo tunayo tunaitumia lakini namna ambavyo tunaitumia kwa upande wetu Zanzibar ni tofauti na namna ambavyo wanaitumia kwa wenzetu wa Tanzania Bara. Sisi tume-*base* zaidi kwa watu ambao ni Mume na Mke ambao mmoja ni muathirika wa UKIMWI anapotumia dawa ile watu wale wawili wanakuwa hawawezi kupata maambukizi ya UKIMWI. Lakini pia dawa hizi wamekuwa wakitumia watu ambao inawezekana wanawake wanaojiuza au wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja, sambamba na watu wengine kana kwamba wanapotumia dawa hizi kunakuwa na ugumu wa kuweza kupata maambukizi, lakini kwa sisi Zanzibar msimamo wetu kwamba tutatoa dawa hizi kwa familia ambazo wameingia katika ndoa lakini mmoja iwe mke au mume awe ameathirika ili kuweza kupunguza yale maambukizi ya UKIMWI. Mhe. Naibu Spika, tumelazimika kusema kwa sababu hoja ilikuwa iliyozungumzwa kwa hiyo mtatuvumilia Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed alitoa hoja kuhusiana na fungu la HC05010201 ambalo kwa mwaka wa fedha 2017/18 ilitengewa jumla ya shilingi milioni 11,620 kwa nini mwaka huu wa fedha halikutengwa fedha yoyote. Lakini tunaomba tumuhakikishie tu Mhe. Mwakilishi kwamba pia katika mwaka huu wa fedha tumetenga fungu hilo lakini pia limetajwa moja kwa moja na linahusu utafutaji wa fedha kwa muitiko wa UKIMWI ambapo ni moja ya vipaumbele kwa mwaka wa fedha ujao 2028/19. Fungu hili limetengewa jumla ya shilingi milioni 49,835 elfu katika kifungu cha HC05010205. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Mohammed Said Mohammed yeye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bajeti akienda katika fungu lile ataona ingawa limekuja tofauti na namna ambavyo ilivyokuwa mwaka jana, mwaka jana ilikuwa moja lakini mwaka huu imeingia katika fungu kubwa la jumla. Waliochangia hapa wengi lakini ntajibu zile hoja kwa jumla ingawa wengi walijaribu kutoa pongezi kwa namna ambavyo waliweza kuona utekelezaji katika mwaka uliopita.

Mhe. Naibu Spika, pia niende katika suala zima la Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, hapa napo bahati nzuri wengi kila mmoja kama ambavyo tulisema mwaka jana jambo hili la vita vya dawa za kulevya siyo letu peke yetu, jambo la vita vya dawa za kulevya siyo ya kuiachia serikali peke yake wala si la kuiacha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais peke yake, vita hii ni yetu sote kila mmoja humu ndani tumejaribu kusema na Mhe. Makamu wa Pili kila anapokwenda katika shughuli hizi amekuwa akisisitiza, vita hii ya madawa ya kulevya ni vyema tukapigana sote, kwa hivyo hata michango ya Waheshimwa Wajumbe imeonesha namna gani kila mmoja anavyoguswa na jambo hili la dawa za kulevya.

Lakini, nianze na hoja ya kwanza ya Mhe. Machano iliyohusu suala zima la ujenzi wa kituo tiba cha marekebisho ya tabia kilichokuwepo pale Kidimni, tunakubali lakini katika mwaka wa fedha katika serikali ya awamu ya tano 2010/2015 serikali iliazimia kujenga *Rehabilitation Center,* yaani Kituo cha Kurekebisha Tabia ambacho kwa wakati huo kilitengewa eneo la Tunguu ingawa baadae yakaja kufanyika mabadiliko kutokana na namna ya eneo la Tunguu lilivyo na mahitaji ya eneo lilivyotokezea.

Lakini kwa mwanzo kabisa naomba nitaje ule mchanganuo wa fedha kwa namna ambavyo Mhe. Mjumbe alijaribu kuuliza na tunaweza kumpatia ili aweze kupitisha vifungu twende tukasimamie hili tuweze kupunguza gharama kwa zile *Sober House* sita ili likikamilika hili gharama itabaki kuwa kwetu. Kwa mwaka wa fedha, fedha zote zilizotumika mpaka sasa katika ujenzi ule tumetumia jumla ya shilingi bilioni 2,292,689,69.72 kwa mpaka sasa gharama yote ni hiyo. Lakini kwa sababu ujenzi ule unajengwa kwa awamu na bahati nzuri kituo kile kinajengwa kwa fedha zetu za ndani na serikali imeazimia hatuwezi tukajenga jambo lolote katika mwaka mmoja tutajenga kidogo kidogo kwa namna ambavyo mahitaji na upatikanaji wa fedha utakuwa unapatikana. Kwa hivyo, ndio maana katika hatua ya awali kabisa serikali iliidhinisha shilingi milioni 100 kwa dhamira ya kwenda kutafuta kiwanja cha kuanza kutia uzio katika eneo lile la Kidimni. Kwa wale ambao wamaejaribu kufika wataona mazingira ya hali halisi pale hakuna ardhi ya kawaida kuna jiwe gumu linahitaji gharama kubwa sana ili kuweza kutia.

Mhe. Naibu Spika, katika awamu ya pili ambayo ilikwenda na ujenzi wa lile jengo lenyewe la *Min Building* yaani *Rehabilitation Center*, ambayo imegharimu jumla ya shilingi bilioni 1,413,475,217.72 ambazo kwa hatua ya awali iliweza kukamilika mpaka *ground flow* na kutumia jumla y a shilingi milioni 49,485,704 kwa ajili ya malipo ya mshauri kwa wakati huo.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia katika awamu ya pili wakati tunaendelea na ujenzi, tumeendelea kujenga katika majengo ya visaidizi yaani sasa hivi ukifika pale utakuta *Laundry* pamoja jiko ambapo hapo sasa pia serikali iliweza kutoa jumla ya shilingi million 621,269,009 ambazo hizo zote ukienda katika huduma ya *Laundry* na jiko tayari kwa sasa vimeshakamilika. Sasa tunakuja katika mwaka huu wa fedha kwa sababu jambo hili ni endelevu. Katika mwaka huu wa fedha

tunaomba wenzetu mtuidhinishie hii shilingi milioni 500 ili kwenda kupandisha *flow* nyigine juu na wakati huo huo kuweza kutia *funiture* mle ndani kwa ajili ya kituo kile kianze kufanya kazi.

Kwa kweli, msimamo wa wizara na sisi tumeona kama vile ambavyo mkiona nyinyi kila mwaka serikali inatoa pesa kwa ajili ya ujenzi katika kituo hiki lakini tumeazimia katika mwaka huu wa fedha 2018/19 kuweza kituo hiki sasa kianze kutumika haraka iwezekanavyo. Hiyo ndio dhamira yetu na tunategemea kama upatikanaji wa fedha utakuwa vizuri *Alhamdulillah* katika mwaka huu wa fedha kituo hiki kitaanza kazi mapema iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, pia ipo hoja iliyotoka kwa Mhe. Rashid Makame Shamsi kuhusiana na changamoto ya kutokujua idadi ya vijana wanaoingia katika maeneo ya *Sober House*, hii tunasema kwamba idadi ya vijana wanaoingia kwenye *Sober House* idadi hiyo ipo na zinapatikana, isipokuwa kwa sababu katika *Sober House* zile kuna utaratibu unaowekwa kila anaeingia na kutoka hii kwa sababu suala la madawa ni *addicted* kuna wakati tunahesabu mtu alietoka halafu akaingia kwengine inavyoelekea, lakini idadi kamili ipo na kwa mujibu wa takwimu zetu kila kitu kipo sawa.

Kwa mwaka huu 2017/18 kuna jumla ya vijana 378 walioingia katika nyumba za upatikanaji nafuu ambao jumla ya vijana 328 waliingia katika maeneo ya Unguja ambapo Kaskazini B walikuwa vijana 8, Wilaya ya Mjini walikuwa vijana 131, Magharibi A walikuwa vijana 96 na Wilaya ya Magharibi B walikuwa vijana 95. Sambamba na Pemba walikuwa jumla vijana 50, Mkoani walikuwa vijana 12, Chake chake walikuwa vijana 28 na Wete walikuwa jumla ya vijana 10. Kwa hivyo, tunasema Mhe. Rashid Makame Shamsi takwimu hizi zote zipo wakati tunaandaa kitabu hiki wakati mwingine *space* inakuwa ndogo hatuwezi kuingiza kila kitu lakini unapokuja kwenya *Database* yetu pale katika Tume ya Kuratibu Dawa za Kulevya kila kitu unakikuta kipo kwa utaratibu uliokuwa mzuri.

Mhe. Naibu Spika, pia imetolewa hoja kwa Mhe. Hidaya Ali Makame kuhusiana na serikali kuwachukulia hatua watu wanaoingiza dawa za kulevya ili sambamba na ile iliyolosemwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwamba kamati yao ilipofanikiwa kutembea katika maeneo ya Vyuo vya Mafunzo vyetu ilibahatika kuona watu waliokuwa wanatumia na wauzaji. Serikali sote tunatambua katika kipindi hiki serikali imeweza kukamata watu wengi ambao wanajihusisha na biashara ya dawa za kulevya na wengi wao wapo katika Vyuo vya Mafunzo yetu haya, lakini pia ni vyema Waheshimiwa Wawakilishi tukawa wepesi pia wa kukumbuka pale ambapo tunakuwa tunasimamia.

Mwaka jana hapa tuliambiwa kwamba tujitahidi ili kumtafuta mtu ili kumtafuta kumpata mtu anaeingiza madawa ya kulevya tuanze hawa wanaotumia, lakini hekima na busara ya serikali kwa sababu sisi tuna *Sober House*, sisi tunahudumia *Sober House* tukasema sisi tutaendelea kuwapa *treatment* lakini wakati huo huo wale ambao tunawakamata ambao wanajihusisha na

biashara hii hata kwa kiwango kidogo hatuwezi tukawaacha mtaani. Lakini hata wala wale ambao wanajihusisha na biashara hii kwa kiwango kikubwa na wenyewe pia wako ndani inawezekana hamkubahatika kuwaona wote ndani kutokana na *sensitivity* ya watu wenyewe siyo kila mtu aliyekuwepo katika vyuo vya mafunzo unaweza ukamuona katika mazingira yote.

Kwa maana hiyo jambo hili serikali inashughulika na watu wa aina zote, wauzaji wadogo sambamba na wauzaji wakubwa. tuendelee Waheshimwa Wajumbe kutoamini katika hilo na tushirikiane kwa pamoja sisi na nyinyi katika kupeana taarifa ili jambo hili liweze kwenda sambamba, kwa maana hiyo jambo hili serikali inashughulika na watu hawa wa aina zote wauzaji wa dogo sambamba na wauzaji wakubwa. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe muendelee kutuamini katika hilo na tushirikiane kwa pamoja sisi na nyingi katika kupeana taarifa ili jambo hili liweze kwenda sambamba.

Lakini pia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alisema kwamba tuwatowe hawa watu ambao ni watumiaji. Lakini sisi tunasema kwamba yule mtumiaji inawezekana alikutwa na dawa za kulevya na kile alichokutwa nacho mkononi madhali ni kizibiti basi nayo inatosha kwenda katika vyombo vya sheria na madhali ameshafika kule basi vyombo vya sheria na mkono wa sheria unawajibu wa kufuata taratibu za kisheria ili kuweza kuwachukulia hatua.

Mhe. Naibu Spika, pia ilitoka hoja kwa Mhe. Mohammed Said Mohammed kuhusiana na maendeleo juu ya ongezeko la makadirio ya fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ya Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Tunamjibu kwamba katika makadirio hayo yameongezeka kutokana na huduma zilizotarajiwa kutolewa ikiwemo;

1. Kazi za kawaida za Unguja na Pemba ni shilingi milioni 6,726,098,000.
2. Ni shughuli ya uendeshaji wa huduma ya kituo cha tiba ya maendeleo ya kurekebisha tabia Kidimni.

   Sambamba na ile kule awali nilisema, tumeomba shilingi milioni 500 kwa ajili ya kupandisha *floor* nyengine katika ujenzi ule. Pia tumeomba shilingi milioni 268,702,000 kwa dhamira ya kuingiza *furniture* na baadhi ya visaidizi kwa watu ambao watahitaji kuingia katika kituo kile. Hiyo ndio dhamira yetu na hiyo ndio sababu iliyofanya fungu hili likaweza kuongezeka.

3. Ni kazi za maendeleo za kuendeleza ujenzi wa jengo kuu la kituo cha Kidimni. Hii ndio ile ya shilingi 500 milioni ambayo tumeomba katika mwaka huu wa fedha.

Kwa kweli, hizo ndio sababu kubwa zilizofanya bajeti hii kuweza kuzidi. Kwa hivyo, tunaomba tu Mhe. Mwakilishi atuvumilie na atustahamilie apunguze buti, atupitishie kifungu ili twende tukapunguze kundi kubwa ambalo linaendelea kuitesa serikali na jamii yetu linayotumia dawa za kulevya ambao wapo katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa nitakwenda katika Tume ya Uchaguzi. Hapa napo pia Waheshimiwa Wajumbe wengi bahati nzuri tunapoigusia Tume ya Uchaguzi basi sote humu ndani tunakuwa *beneficiary* kwa uzuri. Kwa hivyo, kila mmoja anaona raha na anatamani tume ile iweze kuwa na

vitu vyote vinavyostahiki. Sambamba na hilo nitaanza na ile hoja ya Mhe. Rashid Makame Shamsi ambapo yeye alianza kuzungumzia suala la majengo ya ofisi, ufinyu wa watendaji, vitendea kazi na maslahi ya wafanyakazi. Lakini haya yote ofisi na serikali imekuwa ikiyashughulikia kwa karibu sana.

Mhe. Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni serikali na Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein aliweza kutoa majengo na maeneo ya wazi kwa Tume ya Uchaguzi, ili kuweza kuwapa maeneo ambayo kwanza wataweza kupanua ofisi zao, lakini pili kuweza kutengeneza ma- *godown.* Lakini sambamba na hii Mhe. Naibu Spika, nitaijibu sambamba na ile hoja ya Mhe. Miraji Khamis Mussa aliyokuwa anasema kwamba kuna baadhi ya Ofisi za Tume ya Uchaguzi sambamba na ile iliyokuwepo katika Wilaya ya Kaskazini B ipo juu ya ghorofa, ambayo inawapa tabu baadhi ya watu wenye mahitaji maalum kuweza kufika.

Tutajitahidi sana tutaweka miundombinu rafiki, lakini pia tuseme tu kwamba serikali imeipatia Tume ya Uchaguzi Fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari, ambapo kwa makisio mpaka kufikia mwaka 2020 tunategemea serikali kuipatia gari kumi mpya Tume ya Uchaguzi. Lakini kwa mwaka huu wa fedha unaomalizika wa 2017/2018 tayari kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya gari mbili mpya ambazo taratibu zake za manunuzi tayari zimeshaanza kazi. Kunako mwanzoni mwa mwezi wa Juni/Julai tayari ofisi itakuwa imeshapata gari mpya kwa ajili ya matumizi ya tume. Mara hii itakuwa na gari mbili na katika bajeti hii pia itakuwa ina gari mbili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo kulikuwa kuna hoja ile ya kuhusiana na wafanyakazi. Kwa bahati nzuri Wizara ya Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma wanalo jukumu hilo wanaendelea nalo litakapokuwa tayari tutapata watendaji bora, makini na ambao wataweza kufanyakazi vizuri katika Tume yetu ya Uchaguzi. Pia bado serikali inazingatia sana na kuyatazama maslahi ya wafanyakazi wote wa serikali, sio tu wa Tume ya Uchaguzi, lakini wote kwa ujumla wake.

Mhe. Naibu Spika, lilizungumzwa pia jambo katika bajeti ya mwaka 2016 pia yamo katika malengo ya mwaka 2017/2018 hayaendani na utekelezaji kama ambavyo yameainishwa, kweli inawezekana Mhe. Mjumbe aliona hivi na sisi tunakiri. Lakini *ZEC* ilipanga malengo sita katika mwaka 2017/2018, kati ya hayo malengo matatu yametekelezwa kwa ukamilifu, lakini lengo a,b na c hayakuweza kutekelezeka kwa wakati huo na hili ukiyasema vizuri malengo haya nina hakika Mhe. Miraji Khamis Mussa atakuwa anakumbuka, lakini pia Mhe. Rashid Makame Shamsi atakuwa anayatizama vizuri.

Mhe. Naibu Spika, ukiyasoma malengo haya yanakwenda sambamba na Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ambayo tumeifanya mwezi wa 12 katika Baraza hili tukufu, ina maana katika wakati ule tulishindwa kutekeleza, maana ya malengo haya moja kwa moja yanakuja sambamba katika sheria ile. Kwa hivyo, busara ikatuongoza tukasema twende kwenye sheria ili tukimaliza utaratibu wa sheria malengo haya yatakuja kutekelezwa katika sheria hii mpya na tayari sheria ile imeshasainiwa kwa hivyo utekelezaji wake utakuja sasa katika sheria mpya kwa pamoja, ndio maana kwa wakati huu hatukuweza kuyatekeleza kwa wakati. *(Makofi)*

Lakini pia hoja zimetoka bajeti ya Tume ya Uchaguzi ndogo hoja ya Mhe. Machano Othman Said lakini pia Mhe. Rashid Makame Shamsi haya yote tumeweza kuyapokea, lakini tunasema Mhe. Machano Othman Said shughuli zote zimeainishwa katika kifungu cha 105 ukurasa wa 51

katika program ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za uchaguzi na fedha zake zitalipwa kutokana na Mfuko Mkuu, ilitoka hoja kwamba pesa hizi zilizotengwa ni kidogo. Lakini tunapokwenda katika suala zima la uchaguzi fedha ya uchaguzi inakuwa haitokani na bajeti mara nyingi fedha ile inakuwa inatoka katika mfuko mkuu wa serikali.

Kwa hivyo, tunamuomba Mheshimiwa atuelewe hilo mungu akitujaalia bajeti hii kwa mwaka huu imeongezeka kidogo katika kipindi hichi na namna ambavyo Wizara imekuwa ikipanga program zake.

Lakini pia ilitolewa hoja na Mhe. Mohammed Said Mohammed kuwa hakuna fedha iliyopangwa katika program ya uendeshaji wa shughuli za uchaguzi. Lakini tunasema fedha za programi hii zinatoka katika mfuko mkuu wa uchaguzi hii itakwenda sambamba na ile hoja ambayo ilitoka kwa Mhe. Machano Othman Said. Kwa hivyo, tunaomba tu Waheshimiwa Wajumbe wapunguze buti watupitishie bajeti hii, ili tuende tukawarahisishie wenzetu wa Tume ya Uchaguzi kuweza kufanya kazi hii vizuri.

Mhe. Miraji Khamis Mussa alizungumzia suala zima la ununuzi wa gari ambalo nalo pia itakuwa nimeshalisema pale, katika kipindi hichi mpaka kufikia 2020 tunategemea kuwapa gari 10, lakini hiyo ilikuwa ni program ya muda mrefu. Lakini nini tutafanya kwa muda mfupi wakati Tume wanakabiliwa na suala zima la upungufu wa magari, Wizara kwa kushirikiana na tume ikasema lazima tuende tukafanye repea ya magari yote ya Tume ya Uchaguzi yaliyokuwepo ndio maana tukaona katika bajeti yetu hii wameona sehemu ambayo kwamba tume imeweza kufanye reperea ya magari yote ili yaweze kutumika. Tayari magari yale yamerudi katika condition yake nzuri yanatumika na yanaweza kusaidi vizuri, zitakapokuja hizo nyengine zitaweza kusaidia na kufanya utekelezaji uliokuwa bora zaidi kwa tume yetu ya uchaguzi.

Vile vile, Mhe. Mtumwa Peya Yussuf walizungumzia suala la utendaji tunawasubiri wenzetu wa Wizara ya Katiba na Sheria watuletee watendaji na tunaamini hawawezi kutuletea watendaji ambao hawana sifa wala vigezo, kwa sababu wizara ile ni wachapa kazi nae Mhe. Waziri pale ni mtu makini na yeye atatuletea watu makini ambao watakuwa na uwezo wa kuhudumu katika shughuliza uchaguzi.
Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende katika suala zima la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa *CDF* tumepokea mawazo kwamba fedha tunazotoa ni kidogo na sisi tunakiri hizi changamoto na *demand* katika majimbo zimekuwa zikiongezeka siku baada ya siku, Waheshimiwa Wawakilishi hawa wana jukumu kubwa la kuhakikisha wanawapa maendeleo watu hao. Lakini sisi tumelipokea hili tunachosema dhamira ya serikali imeanza vizuri na huko ilikoanza serikali ilikuwa imeshawapa Waheshimiwa Wawakilishi jumla ya milioni kumi. Kutokana na maendele na ukusanyaji wa uchumi unavyokwenda kadri ambavyo uchumi wetu unaimarika ndio kadri ambavyo tunaweza kuwaongezea fedha Waheshimiwa Wawakilishi katika mfuko huu wa *CDF*, tumetoka milioni kumi, tumekwenda milioni kumi na tano na sasa tuko katika kiwango cha milioni ishirini.

Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akitujaalia namna ambavyo uchumi wetu utaimarika ndani ya serikali hii, basi muda wowote serikali haitosita kuwaongezea fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Kwa hivyo, tuendelee kuiombea kheri serikali yetu, ili iweze kufanya makusanyo yaliyokuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niende katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu hapa nako pia Waheshimiwa Wajumbe wengi waliweza kuchangia kwa namna yake. Kwanza tukiri bila ya sisi kuna changamoto ambayo ipo katika suala zima la maeneo ya skuli zetu, mazingira sio rafiki sana hasa kwa watu ambao wana mahitaji maalum hasa katika Kitengo cha Elimu Mjumuisho, katika hili tunawashukuru sana wenzetu wajumbe wa kamati maana wao waliweza kufika katika maeneo ya skuli nyingi wakaweza kutoa ushauri wao na wakaweza kutoa nasaha kwa maekelezo yao. Haya yote ushauri wao na maelekezo yao yaliweza kupokelewa moja kwa moja na wenzetu wa Wizara vilivyo kwa maana tuna ushirikiano wa karibu zaidi sisi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais huwa tunawapa maelekezo wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hasa wale wanaosimamia elimu mjumuisho, ili kuwawekea mazingira bora mazuri vijana hao watu waliokuwa na mahitaji maalum hasa katika suala la kupata elimu.

Sambamba na hilo ilizungumzwa changamoto ya majenzi hasa katika majengo ya serikali na binafsi. Kwa hivi sasa serikali tayari imeshapitisha muongozo rasmi hapo awali katika kipindi cha nyuma ukiwa na muongozo mzuri katika maeneo ya majengo, hivi sasa serikali imeshapitisha muongozo rasmi katika kipindi hichi cha juzi na tayari sasa hivi tupo katika kufanyia *translation* muongo ule kuutoa katika Lugha ya Kiingereza kwenda katika Lugha ya Kiswahili. Tunaamini sasa majengo yote ya binafsi na serikali yatakapoanza kujengwa watakuwa na wajibu wa kuweza kupata muongozo.

Tunafahamu kuna changamoto hiyo ipo hapa lakini tuna changamoto hiyo ipo katika Afisi yetu ya Makamu wa Pili. Lakini, Afisi yetu ya Makamu wa Pili katika bajeti hii sisi tumeshamaliza kila kitu tunategemea bajeti hii itakapopita sisi tutaweza kuweka *limit* pale kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum wanapofika katika Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais waweze kupata *lift* kwa ajili ya kufika katika afisi za juu.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, ilitoka pia hoja kutoka kwa Mhe. Mohammed Said Mohammed kuhusiana na kifungu cha kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu, tunasema kifungu hichi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fedha zake zimegawiwa katika huduma tatu tofauti, lakini katika mwaka huu wa fedha kifungu hiki kimeingizwa katika sehemu moja ukitizama uzuri katika Program ya Ujumuishaji wa Watu Wenye Ulemavu kwa Kujenga Uwezo Watu Wenye Ulemavu na Uhamasishaji Masuala ya Watu Wenye Ulemavu, ambavyo ukitiama katika program ya *HC* 01020501 inaonesha vizuri zaidi katika ile hoja ambayo umeitoa. Ina maana lile fungu limetoka kama ambavyo liliwasilisha katika mwaka uliopita katika sehemu tatu mara hii limekuwa katika fungu moja.

Kwa hivyo, tukutoe hofu katika hilo bado tuna dhamira nzuri ya kuwasaidi watu wenye mahitaji maalum na ndio maana tukawa tunazingatia, tumekuwa tukifanya hivyo kila wakati pale ambapo tumekuwa tukihitajika.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niende kwenye Idara ya Mazingira ambayo nayo kwa namna pekee wajumbe wengi pia wameguswa. Nianze na hoja iliyotolewa na Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na mradi unaostahiki. Mhe. Mwenyekiti katika ripoti yao ya kamati walishauri na walielekeza hata katika vikao vya ofisini kwamba ni vyema kila mradi sasa ufanyiwe utafiti mapema, sisi ushauri wote uliotolewa na Kamati tumeupokea tunauchukuwa na tunaamini

tutakavyokwenda katika utekelezaji tutayazingaria haya yote ya kamati ambayo wameweza kuyatoa.

Lakini pia ilitolewa hoja na Mhe. Machano Othman Said kuhusiana na tofauti iliyopo baina ya mradi wa kukuza uwezo wa kitaifa wa kuhimili athari ya mabadiliko ya tabia nchi, na mradi wa kuimarisha uhimili wa mabadiliko na tabia nchi. Naomba kumjibu na kumtoa hofu Mhe. Machano Othman Said kwamba mradi wa kukuza uwezo wa kitaifa…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri, malizia kwa sababu kuna Mhe. Waziri wako itabidi na yeye aje ajumuishe, Mhe. Makamu wa Pili itabidi aje ajumuishe muda umeshatumia mkubwa sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, katika kwa sababu ya muda na mimi nitamuachia Mhe. Waziri lakini kwa heshima ya pekee na namna pekee na kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Mwera na mimi natumia fursa hii ya kuunga mkono hotuba ya bajeti hii ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia moja nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sasa hivi nitampa nafasi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, aidha nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena jioni hii tukiendelea katika shughuli zetu hizi za kikao cha bajeti. Baada ya shukurani hizo naomba uniruhusu nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna ambavyo anaiongoza nchi yetu na juhudi zake anazosimamia kwa namna ambavyo anaiongoza nchi yetu na juhudi zake anazosimamia kwa kuwa na umoja na utulivu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Aidha, shukurani za kipekee nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kumsaidia sana sana Rais wetu lakini pia kwa kuongoza ofisi yetu na kusimamia shughuli katika Baraza letu la Wawakilishi, pia Mhe. Naibu Spika, niushukuru sana uongozi wenu wewe pamoja na Mhe. Spika na Wenyeviti wote kwa namna mnavyotuongoza katika kusimamia Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, sina budi nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya viongozi wakuu ya Baraza la Wawakilishi, pamoja na wajumbe wake wote kwa namna ambavyo wanatupa mashirikiano makubwa sana katika kutekeleza kazi zetu katika ofisi yetu hii.

Vile vile, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa namna ambavyo wanashirikiana na serikali katika kuendeleza mambo mbali mbali ya kuwahudumia wananchi wetu, shukurani za kipekee ziende kwa Waheshimiwa wote ambao wametuchangia katika hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naamini kabisa atakapokuja Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hapa atawatambua mmoja baada ya mmoja ili kuelezea imani yake juu yenu.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru sana sana Mawaziri wenzangu walionitangulia katika kueleza hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wajumbe walizileta mbele ya Baraza hili tukufu na wakachukua hatua waheshimiwa Mawaziri hawa kuzieleza vizuri sana niwashukuru wote kabisa.

Mhe. Naibu Spika, leo tuko katika kuendeleza suala zima la kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe watupitishie bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa sababu Mheshimiwa tumejitahidi sana kufanya wajibu wetu kwa hivyo kwa heshima na taadhima tunawaomba wajumbe wote waipitishe bajeti yetu kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, serikali yetu imefanya kazi kubwa sana na mawaziri hapa walieleza namna mafanikio mbali mbali katika sekta zao sina haja ya kuyarudia, kwa upande wetu nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, ameeleza mengi na mimi nieleze machache yaliyobaki ili kuomba Waheshimiwa tena budi zipungue.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, kamati yetu ilichangia katika hoja hii na wajumbe wengi wakichangia akiwemo Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe, Machano Othman Said, Mhe. Asha Abdalla Juma, Mhe. Suleiman Makame Ali, Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Suleiman Sarahan Said. Wengi walitaka kuelewa sababu zinazopelekea kukubwa na kadhia hii ya maafa hasa mafuriko yanapotokea wakati wa kipindi hichi cha mvua.

Mhe. Naibu Spika, serikali ilichukua jukumu kuunda Mamati Maalum ya Wataalam, ili kutafuta kuelewa chanzo chenyewe cha matatizo haya kujirudia na hatua gani zichukuliwe, ili kuondoa kadhia hii ya mafuriko ambayo yanasababisha maafa nchini kwetu, kamati yetu ile ya wataalam ilifanya kazi nzuri na waliwasilisha serikalini na serikali ilitoa baraka zake na ilitoa maelekezo na namna ya utekelezaji.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kazi imeanza ya utekelezaji na ndio maana mkaona hatua mbali mbali zimechukuliwa na serikali, ikiwemo kutengeneza miundombinu imara ya kupitishia maji ya mvua ikiwemo misingi na madaraja kama ile iliyojengwa Karakana, Kwahani, Jang'ombe, Kwabitiamrani na maeneo mengine. Vile vile, hivi sasa serikali ina mpango kwa kuendelea kuondoa maji katika eneo la Mwanakwerekwe ambalo muda mrefu huwa linasababisha kadhia kubwa sana, kuna mpango mkubwa wa kuondoa maji pale ili maji yale yapelekwe moja kwa moja baharini.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo serikali pia ina mpango wa kujenga barabara katika eneo lile la Mwanakwerekwe itakayokuwa juu, ili hata kama ikitokea maji yakituwama pale isilete tena bughudha kwa wananchi, kwa hivyo serikali inachukua hatua mbali mbali ili kuona matatizo haya yanaondoka. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe tuvute subira wakati serikali yetu tukilishughulikia jambo hili na kuondoa kabisa tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya waheshimiwa walitaka kujua maana ya maafa jambo hili tumeshalieleza mara nyingi sana katika ukumbi huu, tulisema maafa ni athari zinazotokezea baada ya majanga ambayo ama yanasababishwa na mwanadamu ama kwa rehema za Mwenyezi Mungu, kwa hiyo tujitahidini kwa upande wetu kama wanadamu tusisababishe majanga ambayo yanatokezea maafa. Tumuombe Mwenyezi Mungu atuepushie sana sana kutupa majanga katika

nchi yetu, ili tuendelee kubaki salama na kuepukana na maafa mbali mbali ambayo yanajitokeza hasa wakati huu wa mvua.

Kwa ufupi, mengi katika eneo hili ambayo Waheshimiwa Wajumbe walieleza ilikuwa ni ushauri na sisi kwa heshima na taadhima tunaupokea ushauri huo na kuufanyia kazi, isipokuwa yapo malalamiko kidogo yanayoelezea kuhusu misaada inayotokana na baada ya kutokewa na maafa. Waheshimiwa serikali inajitahidi kwa upande wake kutoa misaada mbali mbali kwa walioathirika wa maafa. Lakini tuelewe kwamba utaratibu huu una ngazi mbali mbali kuna ngazi ya shehia, wilaya na pale ambapo serikali kuu inatakiwa kutoa mchango wake. (*Makofi*)

Kwa hivyo, nawaombeni wana waheshimiwa pale ambapo kiwango cha maafa kinafikia cha kitaifa kamati ya maafa ya kitaifa hukaa na kufanya uamuzi, kwa msingi huo pale ambapo kamati ya kitaifa inaona bado haijafikia maafa kwa kiwango hicho basi levu ya shehia na levu ya Wilaya huchukua nafasi yake, naomba sana tushirikiane sote katika kushughulikia matatizo haya yanapotokea.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa nimeona kofi zinapigwa pigwa hivi kiasi ya kuniambia Mheshimiwa usiendelee sana mambo yanakwenda vizuri nawashukuru sana. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa suala la Tume ya Uchaguzi Mhe. Naibu Waziri amelieleza vizuri sana, na ameeleza kwamba fedha hizi ambazo zilitengwa ni kwa ajili ya shughuli za uendeshaji tu, na kukitokea mahitaji mengine ya shughuli yenyewe ya uchaguzi Serikali Kuu huweka fedha hizo kwa Tume ya Uchaguzi kwa hili naamini tumeelewana vizuri.
Kwa upande wa Muungano, nataka niseme kwamba Muungano wetu ni imara tena ni imara sana serikali zetu zote mbili zinamaelewano makubwa zipo imara tunashirikiana vizuri na tuna utaratibu wetu ndani ya serikali wa kutatuwa matatizo yanapojitokeza, ama kuondoa kero zinapojitokeza na hakujatokea kero ambayo inatupa changamoto kubwa sana ambayo haiwezi kupata majibu sahihi. Kwa hiyo, nawaomba tu Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi wote tuwe na subra wakati serikali ikilishughulikia changamoto mbali mbali.*(Makofi)*

Naelewa wapo wakorofi na wasioutakia mema Muungano wetu, wanamuomba Mwenyezi Mungu sana inapotokea kasoro yoyote hutafuta kila namna ya kuzidisha kutokea kuharibikiwa, lakini nataka niseme kwamba dhamira hiyo waliyonayo haitofika mahala maana tumesikia viongozi wetu wakuu wakieleza kwa kina, nia na dhamira ya kuulinda Muungano wetu na hivi karibuni tu Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisema wale wenye dhamira ya kuuvunja Muungano wetu basi, Muungano utawavunja wao mwanzo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tusishituke kabisa na kelele za mlango hazimkoseshi mwenye nyumba usingizi, naamini kabisa mambo yote ambayo yanajitokeza tutakaa, tutayapatia ufumbuzi, ili kuendelea kuimarisha Muungano wetu, na hakuna lolote kubwa ambalo litatushinda katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaishi vizuri katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hayo

madogo madogo yanayojitokeza yatapata ufumbuzi wa muafaka, ili kila upande uendelee kupata fursa na mafanikio ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Kwa kweli, yako mambo mengi Waheshimiwa Wajumbe yameshapata ufumbuzi katika kipindi cha karibuni, ikiwemo suala la fedha zile za minara ya kuongozea meli, vile vile suala la uvuvi wa bahari kuu, mgawanyo wa ajira katika taasisi za Muungano na mengine mengi nia na dhamira ni kwamba kila litakalokuwa ni tatizo tutalishughulikia na lipate ufumbuzi. Vil vile, vikao vingi vya wizara na taasisi mbali mbali tunakutana kwa msingi wa kutatua kera zilizo mbele yetu. Kwa hiyo, sina shaka yoyote Mwenyezi Mungu akitujaalia na haya mengine ambayo yamejitokeza yamezungumzwa kwa uchungu mkubwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, nataka niwahakikishie kwamba yatapata ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu miradi mbali mbali, limezungumziwa hapa suala la mradi wa *Terminal II* ya ujenzi wa *Airport*, nataka niwambie waheshimiwa wajumbe kwamba jambo hili limepata ufumbuzi na ujenzi unaendelea. Vile vile, kuhusu suala la barabara ya Chake – Wete utaratibu mzuri unaendelea nalo karibuni hivi litakuwa limemalizika na litaendelea na utaratibu wake kama ulivyopangwa. Ila ambalo linaleta maslahi kwa nchi yetu tutahakikisha tunalisimamia na limalizike katika njia ya salama kwa mafanikio ya pamoja na kwa maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa mengi yamezungumzwa, limezungumzwa kidogo linalohusiana na nyongeza ya bajeti kwa upande wa Baraza la Wawakilishi, nataka niseme kwamba serikali itachukua kila hatua kadri ya uwezo utakavyoimarika zaidi kwa nguvu zetu za kiuchumi bajeti ya Baraza itaangaliwa kama ambavyo inaangaliwa kila baada ya muda mahitaji yanapojitokeza.

Kwa hiyo, tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe, mjue tu kwamba serikali ina imani kubwa na Baraza hili tukufu na pale penye mahitaji basi serikali itafanya hivyo, kwa upande wa mafunzo kwa sasa tutatumia hichi ambacho tumekipata, kufanya mafunzo kwa wajumbe wetu na pale ambapo tutakapojenga nguvu zaidi basi na serikali itaongeza nguvu zaidi ili kuhakikisha kwamba wajumbe wetu wanapata mafunzo ya kutosha kama inavyotakiwa.

Kulikuwa na malalamiko ya kuvunja kwa baadhi ya sehemu ya jengo letu hili, nataka niwahakikishe Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika kipindi hichi ya bajeti ya mwaka huu tutalishughulikiya vizuri suala hilo, na kila kasoro inayojitokeza tutaanza kulishughulikia ili kupunguza matatizo na jengo letu liendelee kuwa la imara zaidi.

Vile vile, serikali inatambuwa umuhimu wakuhakikisha kwamba wafanyakazi katika Baraza letu tukufu wanapata maslahi mazuri kama ambavyo wanavyopata katika taasisi yengine za serikali sina shaka yote hili nalo litashughulikiwa vizuri, na yote mnaona jitihada za serikali katika

upande huu. Kwa ufupi, Waheshimiwa Wajumbe mengi Mhe. Naibu Waziri alishayaeleza kwa hiyo mimi niendelee tu, kuwaomba tuendelee kuiunga mkono bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tuweze kumaliza mapema leo na mimi Mhe. Naibu Spika naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais. Sasa nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na yeye aje kutoa machache kuhusiana na bajeti yake Mheshimiwa karibu. *(Makofi)*

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, awali ya wote na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uwezo wa kujadili mambo ya msingi kwa ajili ya taifa letu. Pia napenda kuwashukuru waheshimiwa wawakilishi wote ambao wamechangia Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Napenda niwahakikishie kwamba ofisi yangu itazingatia michango yao, ili kufanikisha utekelezaji wa kazi zetu na kufikia malengo tulojiekea ambayo yametokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa 2015/2020. Najua wazi kwa hiyo michango mingi imetolewa au yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, imelenga katika kusaidia kufanikisha shughuli za ofisi yangu, pamoja na kuwashukuru sana wawakilishi, wajumbe waliochangia Hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais napenda niwatambue waliochangia hotuba hiyo kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa);
2. Mhe. Ali Suleiman Ali;
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar;
4. Mhe. Machano Othman Said;
5. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf;
6. Mhe. Asha Abdalla Mussa;
7. Mhe. Rashid Makame Shamis;
8. Mhe. Suleiman Makame Ali;
9. Mhe. Simai Mohammed Said;
10. Mhe. Suleiman Sarahan Said;
11. Mhe. Abdalla Maulid Diwani;
12. Mhe. Wanu Hafidh Ameir;
13. Mhe. Ali Khamis Bakar;
14. Mhe. Hamad Abdalla Rashid;
15. Mhe. Hidaya Ali Makame;
16. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma;
17. Mhe. Hamza Hassan Juma;

18. Mhe. Miraji Khamis Mussa;
19. Mhe. Mohamed Said Mohamed;
20. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa;
21. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf;
22. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini;
23. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu;
24. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum);
25. Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda;
26. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati;
27. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji;
28. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto;
29. Mhe. Waziri wa Afya;
30. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais;
31. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe waliochangia kwa maandishi na kwa heshima kubwa napenda kuwatambua.

1. Mhe. Said Omar Said;
2. Mhe. Tatu Mohamed Said;
3. Mhe. Ussi Yahya Haji;
4. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha;
5. Mhe. Salma Mussa Bilal;
6. Mhe. Mgeni Hassan Juma;
7. Mhe. Bihindi Hamad Khamis;
8. Mhe. Masoud Abrahman Masoud;
9. Mhe. Nassor Salim Ali;
10. Mhe. Zaina Abdalla Salum;
11. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda;
12. Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wako, ambao wamezungumza mambo mengi sana na mengi nawashukuru sana, Naibu Waziri wangu pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais, ambao wametoa majibu mengi ya ufasaha kujibu hoja zote zilizotolewa na wajumbe. *(Makofi)*

Lakini, mimi najibu machache kwanza kuhusu suala zima la mafuta na gesi asilia, nakubaliana na wote waliochangia hoja hii kwamba ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu hivyo naomba ifahamike kwa serikali itakuwa makini katika kuhakikisha suala hili tunakwenda vyema kwa usahihi na kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar kama ilivyokusudiwa kwa

mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Serikali haitomfumbia macho mtu yeyote au taasisi yoyote ambayo itakayotaka kujinufaisha kwa maslahi yao au kwa maslahi yake binafsi kwa kuhujumu uchumi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wajumbe wengi wamezungumzia juu ya suala zima la Muungano, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda kwa ufafanuzi mkubwa sana alioutoa, pamoja na Mhe. Waziri wa Afya na pia Mhe. Mohamed Aboud.

Mhe. Naibu Spika, Muungano wetu ni kielezo cha umoja, udugu, ushirikiano na usalama wetu, sote tukumbuke kwamba Muungano huu uko kwa faida ya pande zote mbili za Muungano na bado uko imara, na utaendelea kuwa imara na utaendelea kuimarika na kusimamia kuimarisha kutekeleza na kuulinda kwa manufaa ya wananchi wake wa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Muungano wetu ni tunu ni tunu duniani na nchi nyingi duniani zinatamani kuwa na Muungano imara na kudumu kama Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zipo nchi zimejaribu kuungana lakini zilishindwa, zilishindwa njiani na zikavunja Muungano wao, sisi tumeweza na sasa ni miaka 54 tangu tuasisi Muungano wetu.

Kama Mhe. Waziri wa Afya alivyosema, Muungano huu haukuja kwa sababu ya kitu umekuja kwa sababu ya utu na udugu. Wakati waasisi wetu Marehemu Julias Kambarage Nyerere na Marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume, walivyozungumzia kuunganisha nchi hizi mbili, baada ya Zanzibar kupata uhuru wake kupitia Mapinduzi Matukufu ya Januari 1964, kauli aliyoitoa Mzee Karume, alisema nakubali Muungano tuunganishe nchi zetu wewe Rais mimi Makamo wako, sasa tujue hapa ilikuwa nia safi ya kizalendo iliyosababisha kupata Muungano huu. *(Makofi)*

Muungano huu ni wa damu baina yetu, ndio maana umeweza kukua hadi leo hii. Lakini jambo lolote duniani lina mafanikio na pia lina changamoto, Muungano wetu umefanikiwa lakini na changamoto vile vile tunazo, na kawaida changamoto ni sehemu ya kuimarisha na kuimarika kwa jambo husika. Ili basi changamoto zinapojitokeza serikali zetu mbili zinaendelea kutatua changamoto hizo kwa kupitia vikao tulivyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa hoja zilizojadiliwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza zinahusiana na Muungano, suala hili litakuwa ni ajenda muhimu zitakazozungumzwa katika Kikao kijacho cha Kamati yetu ya SMT na SMZ. *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, naomba kidogo kwa sababu muda wa kumalizia shughuli yetu kwa jioni ya leo umekaribia na kwa sababu bado tuna shughuli ya kufanya. Kwa hivyo, ningemuomba Waziri katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kutengua muda ili tuweze kuendelea na shughuli yetu. Mhe. Waziri karibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli iliyombele yetu bado kumalizika na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 23 (1) muda wetu unakaribia kumalizika. Kwa hivyo, niliombe Baraza lako tukufu tuweke kando Kanuni ya Muda ya 23(1), ili tuweze kumaliza shughuli ziliyombele yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tayari ameshatoa hoja ya kuongeza muda, wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, naomba sasa uendelee.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, naomba nirejee kusema kwamba napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa hoja zilizojadiliwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza zinazohusiana na Muungano suala hili litakuwa ni ajenda muhimu zitakazozungumzwa katika vikao vya Muungano ambavyo tutajadili hoja na changamoto mbali mbali na kutafuta ufumbuzi kama zilivyopatiwa ufumbuzi changamoto zilizotanguliya. Katika utekelezaji wa suala hili viongozi wa SMT na SMZ wanaohusika na masuala ya muungano watajadili kwa kina na hatimaye kutoa muongozo ambao utasaidia sana kuimarisha Muungano wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tutambue kwamba licha ya changamoto chache zilizojitokeza muungano wetu huu unafaida nyingi sana kwa nchi yetu na wananchi wake kwa jumla yakiwemo masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiulinzi na kiutamaduni. Muungano wetu huu upo pazuri na siyo busara tena kuuchokonoa chokonoa ama kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au kupitia Baraza lako tukufu. Sote tuulinde, tuuthamini na tuupende, mengi ambayo yanajitokeza tutayafanyia kazi wakati ukifika wa vikao vyetu. Lakini haina budi sote hatukatazi kuyasema yale yanayotukwaza, lakini niseme utafika wakati tutayazungumza na sio muda mrefu tutakutana katika kikao chetu cha SMT na SMZ ili kuzungumzia mambo haya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto amezungumzia suala zima kuhusu udhalilishaji, nakubali kuwa wanawake na watoto serikali inaendelea kuchukua juhudi dhidi ya kadhia hii. Afisi yangu tayari imeshafanya vikao mbali mbali ikiwemo viongozi wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto pamoja na viongozi wa dini mbali mbali, Kamati za Shehia, Asasi za Kiraia pamoja na washika wa maendeleo.

Katika vikao hivyo tumejadili kwa kina na hatimaye kukubaliana, kuandaliwa kwa Waraka Maalum wa kupeleka serikali kwa maamuzi mazito ambayo yatatoa suluhisho juu ya kadhia hii ya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Mhe. Rais wetu amekuwa akilizungumzia suala hili kwa kila mkutano wake. Hivi karibuni alikuwa ana mikutano na Mabalozi wa nyumba kumi wan nchi nzima Unguja na Pemba na katika kila mkutano amezungumzia suala zima la udhalilisha na namna ya kulipiga vita.

Natoa wito kwa wananchi washirikiane na vyombo husika kutoa taarifa juu ya matokeo haya ya udhalilishaji na kuachana na tabia ya muhali, tabia ya kukingiana kifua ili suala hili tuweze kupigana nalo hadi tupate ushindi.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe pia wamezungumzia juu ya suala zima la mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Serikali inaendelea na jitihada ya kuziwezesha taasisi husika katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Nachukua nafasi hii kuvitaka vyombo vyote vilivyoundwa kusimamia suala hili kutekeleza wajibu wao kwa umakini na kufata sheria na maadili ya kazi zao. Pia niwaase watendaji kujiepusha na rushwa na uhujumu uchumi pamoja na kutokuwa na muhali kwa mtu au taasisi yeyote itakayokiuka Sheria ya Maadili katika kupiga vita dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, miongoni waliochangia hoja hii alikuwa ni Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ambaye alisema kwamba jimboni kwake kuna kituo kinachoshughulikia dawa za kulevya, lakini jengo la kituo hicho ni kibovu mno. Namuahidi kwamba tukimaliza Kikao cha Baraza nitakwenda kukitembelea na kuona ni kiasi gani tunaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kusimamia suala la UKIMWI serikali itaendelea kutoa taaluma na kusisitiza athari za janga hili katika kuzuia maambukizi mapya ya VVU mapia kutoa huduma kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Aidha, serikali inazitaka taasii kushiriki kikamilifu katika kulimaliza tatizo la UKIMWI nchini mwetu. Kwa sasa UKIMWI bado upo, hatuna budi kujitahidi tufanye kila linaloweza kuepukana na ukimwi. Ugonjwa ambao hauna dawa wala hauna chanjo. Nachukua fursa hii kuwaomba wananchi kuendelea kutunza amani iliyopo na kuviripoti vitendo vyovyote vinavyoashiria uvunjifu wa amani. Pia navitaka vyombo vyote vinavyosimamia amani na usalama wan chi yetu kuendelea kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kuhakikisha amani na usalama wan chi yetu unaendelea kudumu.

Mhe. Naibu Spika, suala la utatuzi wa migogoro, kero na malalamiko ya wananchi, hii ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ibara ya 189 imetutaka kusikiliza kero zao na kuzitafutia jawabu, hivyo nawahakikishia wajumbe wa Baraza hili kuwa Serikali ya CCM ni mtetezi mkuu wa wananchi kuwapatia haki zao bila ya usumbufu kwa kuwa na matumaini ya kuendelea kuongoza hadi 2020. *(Makofi)*

Mhe. Nibu Spika, kuhusu watu wenye mahitaji maalum nalo hili Waheshimiwa Manaibu Waziri na Mawaziri nalo pia wamelikemea, serikali inatambua umuhimu wa mchango wa watu wenye ulemavu katika ujenzi wa taifa letu. Kwa kutambua hilo serikali inaendelea na utaratibu wa uundwaji wa sera ya watu wenye ulemavu ambayo ndiyo itakayotoa dira ya ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika nyanja zote zikiwemo kisiasa, kiuchumi, na kijamii.

Pia tayari muongozo wa miundombinu rafiki umeshazinduliwa, tunaomba taasisi za ujenzi na zinazotoa vibali vya ujenzi kufuata muongozo huu, huku kanuni na muongozo wa hili ulitafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili katika hatua za mwisho wa kukamilika.

Nachukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuwe na subira na suala hili, linapewa umuhimu unaostahiki ili kuwa na jamii mjumuisho katika jamii yetu. Nachukua fursa hii tena kuwaomba wananchi kuendelea kutunza amani iliyopo na kuviripoti vitendo vyote vinavyoashiria uvunjifu wa amani, tunavitaka vyombo vyote vinavyosimamia amani na usalama wa nchi yetu kuendelea kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kuhakikisha amani na usalama wa nchi yetu unaendelea. Nchi bila ya amani haiwezi kupiga hatua, haiwezi kupata maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena nachukua nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Naibu Waziri, Mhe. Mihayo Juma N'hunga, Katibu Mkuu ndugu Shaban Seif Mohammed na Naibu Katibu Mkuu Abdalla Hassan Mitawi, Wakurugenzi wote na wafanyakazi wote wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mashirikiano yao wanayonipa ambayo yananiwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, waipitishe bajeti hii bila ya buti, najua kuna Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wamesema watazuia vifungu, lakini naona baada ya maelezo yaliyotolewa haya na Mawaziri, sioni sababu kwa nini tena waendelee kufanya hivyo. *(Makofi).*

Mwisho Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa hoja hapa. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

$$$

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki nashauri wakati Serikali inapotafuta wakandarasi wa ujenzi wa barabara ambao watajenga barabara zilizo imara kwani tumeona barabara zetu zinazojengwa hazichukui muda zinaharibika, kutokana na hali hii Serikali baada ya kujenga barabara nyengine inabidi zitumike kwa kufanya ukarabati wa barabara hizo ambazo zimejengwa hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti hii naomba Serikali naomba kuiangalia na kuipa kipambele barabara ya Mkoani/Chake ambayo imeharibika kwa mvua za masika zinazoendelea kunyesha ili kuwaondoshea shida ya usafiri, hasa ukizingatia barbara hii ndio inayotumika kwa usafiri wa kwenda Melini wakati wa kuasafiri.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 8 masuala mtambukka Mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kipindi cha Julai, hadi Machi, 2018 jumla ya kesi za watoto 1298 zimeripotika katika mahakama za Vuga, Kaskazini, na Kusini Pemba. Kati ya hizo 45 zimepatiwa hukumu na 8 zimefutwa na 76 zinaendelea ni jambo jema, kuona kwamba hakuna kesi hizo zinaendelea kutolewa hukumu nashauri kesi zilizobakia ziendelee kutolewa uamuzi unaostahiki kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, uk.11 Programi ya Uratibu wa Shughuli kifungu 34(i) za Makamo wa pili wa Rais. Katika ziara aliyoifanya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nchi za kiarabu kufuatilia ziara hiyo, Zanzibar ilifanikiwa kupata msaada wa kusomesha madaktari bingwa 15 kwa gharama nafuu. Mhe. Mwenyekiti, tayari madaktari 8 wapo nchini kutoka Cuba wakiendelea na masomo yao.

Aidha Zanzibar imepatiwa madaktari bingwa kutoka Cuba kwenye fani za mionzi, figo, sikio, pa na koo ni jambo la kupongeza sana hivyo nashauri Wizara zile nafasi 7 zilizobakia wapelekwe vijana wengine, ili tusipoteze nafasi hiyo na hasa tukizingatia kuna upungufu wa madaktari hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Kwanza nianze kwa kuipongeza ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake na utendaji wake katika ofisi yake, pia na Waziri wake na Naibu Waziri wake kwa mashirikiano yao na utendaji kwa ujumla.

Pia niwapongeze Wajumbe wa kamati wa Baraza la Wawakilishi kwa utendaji wao na ufuatiliaji wao wa kuazi zao za kamati na kushirikiana na Wizara kwa kusaidiana na Wizara katika kutekeleza kazi za baraza.

Niende kwenye suala la maafa na fungu la fedha lililotengwa kwa ajili ya maaafa, kwa kweli fungu siodogo linavoonekana, lakini kutokana na suala la maafa fungu hili halitoshi, hususan ukizingatia zaidi linagusa kazi za maendeleo. Na wakati ukiangalia katika vipaumbele ambavyo vimeorodheshwa na program ndogo huoni suala la kazi za kimaendeleo, je, fedha hizi hatuoni kwamba hatuzitendei haki wakati ukiangalia maafa yanapotokea misaada yake mara nyingi yanatokana na wahisani. Pia suala la kukabiliana na maafa linaonekana kutokupewa kipaumbele zaidi kuptika Serikalini nakuonekana zaidi wanategemea wahsani zaidi.

Pia suala la madawa ya kulevya bado ni changamoto kubwa kwa mikoa yote ya Unguja na Pemba, lakini pia Serikali bado ni kikwazo kikubwa kwa vijana wetu wa kike na kiume kutokana na kuwa suala hili ufumbuzi wake bado ni kitendawili katika nchi yetu, hivyo kuonekana kama Serikali bado ina mzigo mzito juu ya ufuatiliaji wa suala la uingiaji wa mawada ya kulevya.

Kwa hivyo naiomba sana Serikali iliangalie kwa jicho la uchukivu na kuchukua hatua ambazo waingizaji hawa wa madawa ya kulevya kuwa wanazibitiwa kwa hali yoyote na kutolewa tathmini ya kila mwezi kwa wanaokamatwa kwa uingizaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache ahsante sana.

Mhe. Ussi Yahaya Haji: Kwqanza naomba pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa hotuba yake ambayo imetupa matumaini kwa namna ya utekelezaji wa ilani ya CCM 2012- 2020 pamoja na baadhi ya ahadi za viongoi.

Pili Mhe. Makamo katika hotuba hii sikuona sehemu yoyote ile ambayo tutafanya mabadiliko ya katiba yetu ambayo, vikao vilivyopita tuliambiwa kabla ya kumalizika mwaka 2018, Serikali itafanya mabadiliko makubwa ya katiba namuomba Mhe Waziri aniambie lini Wizara hii italeta mabadiliko ya katiba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono mia juu ya mia hotuba yake. Ahsante sana.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipongeze Serikali kwa kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuwajali na kuwathamini watu wenye ulemavu, Vile vile kwa kuweka idara ya watu wenye ulemavu kuwa ni moja ya Idara zilizomo katika Ofisi hiyo. Pia leo hii tumeweza kuona pia watu hawa wanaoweza kushiriki na kushirikishwa katika nyanja mbali mbali za Serikali na za kibinafsi, hasa zikiwemo za Afya, elimu na za kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto za watu wenye ulemavu ni nyingi sana lakini nyingine zimeshatajwa na wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kukosekana kwa madaktari bingwa na kuweza kuwatumikia au kuwahudumia ili kuipunguza hali zao za ulemavu, kwani kuna ulemavu mwingine huzidishwa na ukosefu wa huduma bora za afya.

Mhe.Mwenyekiti, ukosefu wa elimu sitahiki kwani walimu wetu huwa wengi wao hawatoi elimu kwa muundo mbinu ambayo wanayo pewa katika mafunzo yao ya kujengewa uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, kuwa maskuli ya Elimu Mjumuisho kuwa mbali na maeneo wanayoishi, niombe Serikali kulichukulia hatua maswali haya kwani tunawea kupata watu wenye ulemavu wenye mazingira mazuri na kupunguzia Serikali mzigo mzito.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, naanza mchango wangu ukurasa 37 Mhe. Makamo programu ndogo ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu, Mhe. Makamo bado idara hii inakabiliwa na changamoto kwa watu hawa, kuosefu wa viungo bandia pamoja na kukosekana kuwepo sehemu au kitengo maalumi kinacho shughulikia suala hili, katika hospitali ya Mnazi Mmoja hivyo tunaomba Serikali pamoja na Wizara husika kuanzisha kutengo hicho muhimu ili kuwaondolea usumbufu wanaoupata wanapofuatilia huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, uhaba wa dawa za watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino) hali inayosababisha watu hawa kupata tabu sana, hata hivyo tunaiomba Serikali pamoja na Ofisi ya Makamo wa Pili kulifuatilia na kulitafutia ufumbuzi tatizo hili.

Mhe. Mweyekiti, ukurasa wa 44 Tume ya Uchaguzi, vile vile kuptia utekelezaji wa Program ya uendeshaji wa shughuli za uchaguzi naiomba Serikali na ofisi ya makamo wa Pili wa Rais katika nafasi zilizowai na zinahitajika kuajiri wengine, kuzingatia vigezo vya elimu pamoja wataalam kwa sehemu hii ni muhimu na nyeti kwa raifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 43 Program ya kutunga sheria, kupitia bajeti na kusimamia taasisi za Serikali, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba ofisi yako kwa kushirikiana na Baraza la Wawakilishi kufuatilia ufumbuzi wa haraka maeneo yote yanayovuja katika jengo hili, kubakia kama lilivyo ni kuzorotoshe utendaji kazi wa muhimili huu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 46 Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti dawa za Kulevya, Mhe. Makamo kupitia program ya uratibu wa mwitiko wa taifa wa ukimwi naipngeza Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Ofisi ya Makamo wa Pili kuona umuhimu wa ZAF PLUS kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019. Kuwaingizia fedha za ruzuku jambo ambalo litasidia sana wananchi weu.

Mwisho. Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa Kusini naunga mkono hotuba hii. Ahsanteni.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Mwenyekiti, nampongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake uliojaa hekima, elimu na ushujaa, maana ushujaa ni kuvumilia mpaka akawanyamazisha wapinzani kutoa meneno ya kejeli kwa Serikali iliyopo madarakani na kuwafanya kwa hiyari yao kushiriki katika miradi mbali mbali ya maendeleo.

Mimi mwenyewe wakati ninapeleka mipiria ya maji nilioni wachimbaji wa mitaro wengi ni wapinzani, nashukuru kama atatokea mtu yoyote ambe ataonesha vitendo vya kuvuruga amani apewe adhabu kali.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za maji safi na salama kwa kuwa Serikali imefanya juhudi kubwa kusambaza maji safi na salama mijini na vijijini, sina budi kupongeza ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa moyo safi wa kuwatakia wananchi maisha bora, nashukuru fedhazilizotengwa ziongezwe ili suala hili la maji kutotosheleza limazikike kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa pili tuweke watu maalum katika kila Shehia yaani waajiriwe ili wapewe jukumu la kufuatilia kupotea kwa maji kwa kuachwa mifereji wazi katika nyumba bila kutumiwa, pia kuacha maji yakapotea bure ka mifereji iliyoko mitaani na pindi ukigundulikana mkosaji huyo achukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, suala la madawa ya kulevya hili ni gonjwa la kuambukiza kama magonjwa mengine, moja kati ya sababu za kuenea kwa madawa ya kulevya yanasababishwa na wahamiaji wanatoka mijini na kuhamisa vijijini na kuwarithisha vijana walioko vijijini, kama tunavyojua siku zote kila jambo higwa iwapo jambo hilo limefanywa na vijana wa mjini hata lugha inayotumiwa na vijana wa mjini ni rahisi kutumika vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu wale vijana wanaotuhumiwa na kuhusika na madawa ya kulevya anapohama mjini akahamia vijijini au mashamba lazima wafuatiliwe na kupewa taaluma tosha wazazi wa vijijini kulijua hili na kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu mfupi naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni.

$$$

Mhe. Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa majumuisho yako mazuri kabisa na mimi natarajia hivyo hivyo kama ulivyosema kwamba vifungu vitapitishwa bila ya wasi wasi wowote. Sasa niwaulize, Mheshimiwa tayari ameshatoa hoja, niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kupitisha vifungu vya Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Machano Othman Said, nimekuona umesimama lakini nataka kukwambia tu kwamba Kamati ya Matumizi inashughulikia matumizi tu.

Machano Othman Said: Sawa Mhe. Mwenyekiti, tunawazo tu leo kwa kuwa ni siku ya furaha kwa sababu leo ni siku ya furaha *backbanche*rs tumekubaliana kwa sababu Makamo wa Pili ni mwenzetu, Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, ni mwenzetu na Naibu Waziri, Mhe. Mihayo Juma N'hunga ni mwenzetu leo kusiwe na buti katika kupitisha bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Machano Othman Said, nimekuelewa vizuri sana na naamini kwamba Wajumbe wengi ndivyo wanavyotaka, lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu inabidi tupitishe vizuri. Kwa hiyo, tayari Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ameelewa na nafikiri ana *appreciate* hayo lakini itabidi tuendelee kupitisha vifungu. Naomba sana Waheshimiwa tusikilizane, naomba sana wakati ambapo tunapitisha vifungu hoja yenu ya kupitisha itaonekana wakati tunapitisha vifungu. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, tunatatizo la *echo* kidogo kwa hivyo akisema aseme kwenye *microphone* ili tumsikie ahsante

Mhe. Naibu Spika: mazungumzo yamezidi ndio mana hatusikilizani vizuri.

FUNGU C (01) - OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

Kifungu C0104 - Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa 59,474,000/-

Kifungu C01111 - Mamlaka ya Usimamizi Mazingira Zanzibar (*ZEMA)* 81,000,000/-

Jumla Kuu ya Mapato Fungu C01 **140,474,000/-**

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu PC0101 - Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais 1,291,205,000/-

Kifungu PC0102 - Uratibu wa Shuhuli za Serikali 27,619,484,000/-

Kifungu PC0104 - Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais 3,757,711,000/-

Jumla Kuu ya Fungu C01 **32,668,400,000**/-

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C02 - BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu PC0201 - Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali 7,682,159,000/-

Kifungu PC0202 - Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi 12, 672,641,000/-

Jumla Kuu Fungu C02 **20,354,800,000**/-

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C03 - TUME YA UCHAGUZI

Kifungu PC0302 - Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uwendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi Zanzibar - 1,774,100,000/-

Jumla Kuu C03 **1,774,100,000**/-

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C04 - TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Kifungu PC0401 -	Udhibiti wa Dawa za Kulevya	925,274,000/-
Kifungu PC0402 -	Uendeshaji na Uratibu wa Tume za Dawa za Kulevya	516,126,000/-
Jumla Kuu Kifungu C04		**1,441,400,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C 05 - TUME YA UKIMWI

Kifungu PC0501	-	Kuratibu Mwiitiko wa Taifa wa UKIMWI	252,451,000/-
Fungu PC0502	-	Utawala na Uendeshaji	651,049,000/-
Jumla Kuu ya Kifungu C05			**903,500,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais bila ya mabadiliko. Sasa, naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

MUONGOZO

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Muongozo wa Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nakusikia endelea.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, naomba muongozo wako wakati walipokuwa wakitajwa wachangiaji Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma sikumsikia kutajwa, ili kuweka *hansard* sawa na yeye kwa mujibu wa kanuni alichangia moja kwa moja, lakini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hakumtaja, yaani hakujisikia. Naomba muongozo wako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, sawa. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais namtambua Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma na kwa makosa yote tunaomba radhi. Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri nakushukuru sana na hata mimi Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma alinileta ki-note. Lakini nashukuru sana tayari ameshaingia kwenye hansard na mchango wake umethaminiwa.

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabisa nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais, nampongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wake, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa wizara kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kwa kweli imeonesha mfano mzuri hasa kwa zile wizara nyengine zitakazokuja baadaye. Kwa hiyo, niwapongeze sana pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu mbali mbali na pia kuwa na umoja kushirikiana kupitisha bajeti hii.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumaliza hapa nilikuwa na tangazo hapa ambalo linatoka kwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya tangazo silioni. Lakini najua maudhui ya tangazo hilo, Mwenyekiti wa *Club ya Simba Sport Club* ametangaza kwamba baada ya kikao hichi anataka ile Kamati ya *Simba Sport Club* ibakie hapa kwa ajili ya kupanga mikakati ya kusherehekea ushindi wao, hivyo ndivyo nilivyotakiwa niseme.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe baada ya kusema hayo naakhirisha kikao mpaka kesho asubuhi saa tatu kamili.

(*Saa 02:16 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 11/05/2018 saa 3:00 asubuhi)*